Kikao cha Thelathini - Tarehe 25 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 90

Utokomezaji Dhidi ya Malaria

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa– Aliuliza:-

Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kupambana na malaria kwa zaidi ya muongo mmoja sasa. Hivyo, taifa limetoka kunako maambukizo ya asilimia arubaini (40%) kwa mwaka 2003 na kufikia asilimia moja (1%) mwaka 2012. Kwa kuwa serikali ina nia ya kuyatokomeza kabisa malaria Zanzibar, nia hiyo inaweza isitekelezeke kutokana na upungufu mkubwa wa kifedha kwa Mradi wa Malaria.

(a) Je, Wizara ya Afya mtatuhakikishia nini katika upatikanaji wa fedha ili kuthamini juhudi zilizochukuliwa na Washirika wa Maendeleo.

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mikakati gani wa kuhakikisha kuwa zoezi hili ufadhili wake unafikia kikomo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 90 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli, zaidi ya muongo mmoja umepita tangu kiwango cha maambukizo ya malaria kushuka Zanzibar kutoka ya asilimia arubaini (40%) hadi asilimia moja (1%), jambo ambalo limenusuru maisha yetu na wageni wetu tunaowategemea sana nchini kwa mapato ya uchumi wetu. Mafanikio hayo yametokana na nia ya dhati ya serikali yetu, watendaji wa Wizara ya Afya, viongozi waserikali, serikali za mitaa pamoja na wananchi kwa ujumla. Pia kwa ushiriki mkubwa wa Washirika wa Maendeleo kadha ndani na nje ya nchi yetu kwa kazi nzuri na kubwa iliyofanywa kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria.

Ni sahihi ugonjwa huu umeteremka kwa kasi kubwa kufuatia utekelezaji mzuri wa mikakati yote iliyopangwa. Ni ukweli usiofichika kuwa iwapo sera madhubuti na mikakati endelevu ya kuzuia kurejea kwa maradhi haya haikupangwa tunaweza tukajikuta tunarudi enzi zile za miaka ya 60 na 80. Hatari zaidi sasa inaweza kuwa hali mbayazaidi kuliko wakati ule, kwa vile kuna baadhi ya wananchi kinga zao dhidi ya ugonjwa huu sasa ni ndogo.

Kiwango cha kusambaa kwa malaria kinapopungua, wahisani huona kwamba malaria sio tishio tena, hivyo hupunguza mafungu ya fedha. Ni kweli historia ya Zanzibar inaonesha kupungua kwa kiwango cha kusambaa kwa malaria hubadilika na kuongezeka kwa ghafla pindi tu mafungu ya fedha kwa ajili ya jitihada za malaria yanapopungua au kusitishwa kabisa, kama Waswahili wanavyosema “kama hakionekani kinasahauliwa”.

(b) Kutokana na uzowefu huo na kuthamini juhudi zilizochukuliwa na serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Fedha wa Rais mstaafu (Bill Clinton) wa Marekani (*CHAI*) imeendesha uchambuzi yakinifu na kuishauri serikali juu ya njia mbadala wa kuweza

kupata fedha za hapa nchini kwetu ili kuweza kuimarisha utekelezaji wa sera ya kumaliza malaria.

Kimsingi kikao cha makatibu wakuu kimeupokea ushauri huo na kimeshakaa, na kimeyapeleka mapendekezo hayo katika kikao cha Baraza la Mapinduzi kwa ushauri na maaamuzi.

Hata hivyo, mikakati ya kuhakikisha Malaria yanapungua itabidi iendelezwe kwa kutumia vyandarua, usafi wa mazingira na kutia dawa kwenye (madimbwi) mazalia ya mbu,kupima malaria unapokuwa na dalili na kama umeugua kutumia dawa na dozi sahihi, kufuatilia wale waliougua katika sehemu walikotoka wagonjwa ili kuchunguza na kutibu wanaoishi na wagonjwa na kupiga dawa majumbani.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mbona mara nyingi kukiwa na tatizo linatakiwa kutatuliwa huwa kunaundwa Mifuko, kwa nini hatuanzishi Mfuko wa kumaliza malaria Zanzibar au hili haliwezekani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, anachokisema ni kweli Mifuko mara nyingi huanzishwa panapotokea matatizo na tatizo la maralia kama hatukulifanyia mkakati madhubuti kama tulivyosema itafika wakati malaria itakuwa ni tatizo upya. Pia nimezungumza katika majibu kwamba wenzetu hawa wa *CHAI* wameleta mapendekezo kujaribu kutushauri na kutuasa kwamba, kutokana na upungufu wa misaada iliyopo lazima tutafute utaratibu. Utaratibu ambao ulikuwa umependekezwa ambao Makatibu Wakuu wameupitia na ambao sasa hivi uko kwenye utaratibu wa kupelekwa serikalini, ili kutolewa maamuzi walikuwa wamependekeza njia mbili. Wanasema kwamba malaria ilikuwa ni moja ya tatizo kubwa ambalo lilikuwa linasababisha vifo vya mama na mtoto. Kwa hiyo kutokana na hilo, wao walipokuwa wanasaidia malaria walikuwa na mtazamo huo kwamba malaria ikipungua na vifo vya mama na mtoto vitapungua.

Ni kweli vimepungua sasa hivi hakuna mama au mtoto anayekufa kwa malaria. Lakini sasa sio hilo tu, malaria inakuwa ni tishio kwa wageni wengi ambao wanaingia katika nchi na ambao huwa wanapoteza fedha nyingi tu katika nchi zao wanakotoka. Sasa mara nyingi wageni wanapokujwa wakiona nchi ina malaria wanaanza kujitibu kule kwa kinga, tukasema kwamba kama malaria itakuwa nchini hakuna na tunaweza kuwakinga na mgeni akijua kwamba anakotoka akifika Zanzibar atakuwa hana tatizo la kuugua malaria atakuwa yuko tayari kuchangia.

Kwa hiyo, walichokuwa wamekipendekeza kwamba, tujaribu kuona utaratibu na serikali ikubaliane nalo na kimsingi kama limekubalika kwamba abiria wanapokuja katika ndege za kimataifa hapa Zanzibar, basi kuwa na angalau tozo ndogo watozwe ili kuweza kutengeneza Mfumo kwa ajili ya hayo Malaria. Hayo yameshawahi kutendeka Zimbabwe, Sierra Leone na nchi nyengine kwa utaratibu wa matatizo mengine yaliyoko huko.

Mhe. Naibu Spika, sio hivyo tu, wakasema basi kama ni hivyo tutengeneze hata Mfuko mwengine wanaita Mfuko wa Kibenki au *endowment fund* ambazo zinakuwa zinakusanywa, halafu cha kufanywa zinawekezwa, zikiwekezwa faida inayopatikana ndio inayotumika katika kutengeneza utaratibu huo wa kuzuia malaria. Kwa hiyo, hizo ndizo njia mbili zilizopendekezwa kimsingi na kama zitafanikiwa, kama zitapita na serikali ikitukubalia tunaweza tukawa na Mfuko wa Malaria nchini kwetu. Si kwa ajili ya hao tu, hata na sisi wenyewe, wafanyabiashara, sisi tunaoishi katika nchi hii, wenye uwezo tunaweza tukachangia kwenye Mfuko huo.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru na nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pamoja na majibu hayo naomba nimuulize swali la nyongeza. Kwanza naishukuru serikali pamoja na Washirika wa Maendeleo kwa juhudi kubwa ambazo wamefanya kwa kiasi fulani kuweza kupiga hatua kupunguza ongezeko la malaria. Lakini kwa kuwa malaria inasababishwa na mbu na sasa kunaonekana kujitokeza ugonjwa mpya unaosababishwa na mbu unaoitwa Dengue. Je, serikali ina mpango gani wa kuelimisha wananchi kuhusu ugonjwa huu hatari.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Zanzibar imeweza kutekeleza mradi wa malaria na tumefanikiwa, lakini tumepata matatizo mengine ambayo sasa hivi imekuwa kidogo ni tishio katika nchi yetu. Kweli ugonjwa wa Dongue hapa Zanzibar uliingia lakini uliingia kwa kasi ndogo sio kama Dar es Salaam ulivyokuwa. Tulijaribu

kuudhibiti na tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Ugonjwa wa Dengue umetokea katika ukanda wa Mashariki na nafikiri umekuja kupitia watu kwa maingiliano kutoka kule kuja huku. Sasa mbu walikuwepo lakini maambukizi yanapitia kutoka kwa mbu na Zanzibar dalili hiyo imeshaonekana, tulipata wagonjwa wawili katika wagonjwa ambao tulikuwa tumewatarajia tuliowapima na wawili waligundulikana kwamba ugonjwa wanao.

Kwa hivyo, serikali imechukua hatua kwanza kueleza ukweli hasa ugonjwa huo ni nini, kwa sababu sio watu wengi waliokuwa wanaufahamu. Wajue kwamba ugonjwa huo unasababishwa na mbu pia mbu wa ugonjwa huo hapa Zanzibar wapo mjini na vijijini ingawa wakati huo walikuwa hawana maambukizi hayo.

Pia wajue kwamba Dengue inasambazwa na binadamu kwa binadamu kwa kupitia mbu na sio njia nyengine wasifikiri, kama kuna njia nyengine lazima mbu wawepo na hayo maambukizi halafu wamtafune binadamu akisha aende kumsambaza kwa mgonjwa mwengine. Kwa hiyo, hiyo elimu ilitolewa na dalili zake pia zilitolewa. Kuna Dengue aina tatu, lakini iliyokuwa imejitokeza Zaidi ni ile ya maumivu ya kichwa, viungo, uchofu, hizo ndizo zilizokuwa dalili kuu.

Hata hivyo, kuna Dengue ambayo ni hatari zaidi ile ambayo inamsababisha mtu kutokwa na damu. Inaweza kuwa mgonjwa yule anatoka damu katika sehemu zinazoonekana, lakini pia inaweza kuwa katika sehemu ya ndani ambayo haionekani kwa hivyo, mgonjwa akapoteza fahamu bila ya watu kufahamu wasielewe anachoumwa ni kitu gani hatimaye akafariki. Kwa hiyo, hayo yalielezwa katika vyombo vya habari na wananchi walifahamishwa.

Mhe. Naibu Spika, isitoshe kama walivyo mbu wengine kwa hiyo yale ambayo yanasababisha mbu kuzaliana iwapo wananchi walielimishwa kwamba tufukie madimbwi, tukate majani katika nyumba zetu, tujifunike vyandarua, tuhakikishe kwamba maji hayatuami katika sehemu hata katika vikopo. Kwa sababu mbu wale wanazaliana katika maji yaliyo safi, kwa hiyo, maji yanayokaa kwenye vifuu, kwenye vikopo, kwenye mauwa tunayoweka humo lazima tuhakikishe kwamba maji yale tunayamwaga. Elimu imetolewa ya kutosha na tulijiandaa kama wizara kwa ajili hiyo, tulinunua vifaa vya kupimia kwa haraka, tulinunua vya kupimia *DNA* ya hao wadudu. Kwa hiyo, kama serikali tumejiandaa na elimu ya kutosha imetolewa na tumeweza kulidhibiti suala hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia mitaro yetu mingi kuziba kutokana na sababu ya wavuta unga kuchukua vyuma vya mitaro na kuviuza. Je, wizara yake itashirikiana vipi kuliondoa tatizo hili la kuziba kwa mitaro hiyo na kupunguza maradhi haya ya malaria.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nafikiri suala la mitaro liko chini ya Manispaa na Manispaa kuna wataalamu wetu wa afya na katika vituo vyetu vya afya vya mjini kuna wataalamu wetu pia wa afya. Tutajitahidi, tutakaa na wenzetu wa Manispaa pamoja na wataalamu wetu wa afya katika vituo tuone hilo tatizo linaondoka.

Nam. 79

Madaktari wa Zanzibar Kukimbilia Nje

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwa kuwa kusomesha madaktari ni gharama kubwa na hivyo daktari aliyesomeshwa na kwenda kufanya kazi nchi nyengine anasababisha pengo kubwa la wataalamu.

(a) Je, kumewahi kufanyika utafiti wa kujuwa ni madaktari wangapi waliokimbia Zanzibar kwenda nchi za nje kutafuta maslahi zaidi.

(b) Je, serikali imechukua hatua gani za kuwawezesha madaktari hao warudi nyumbani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 79 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, madaktari wanaondoka Zanzibar kwa sababu tofauti ukiachilia mbali maslahi; kuna wanaoondoka kwa kujiunga na mashirika mbali mbali ya kitaifa na kimataifa, kujiunga na wizara nyengine za serikali kama Jeshi na Polisi, kwenda kusomesha Vyuo Vikuu vya Madaktari Tanzania Bara, kuna wanaoolewa na

wanaoowa kufuata wenza wao, walioingia kwenye siasa na kuwa Wabunge na Wawakilishi na wako hawa ambao wanaokuwa hawaridhiki na mshahara kwa kulinganisha na maisha ya nchi nyengine.

Takriban kuna kama madaktari 25 ambao mimi ninaowafahamu kwa kipindi nilichokuwepo ambao waliondoka katika Wizara ya Afya. Kwa kweli nimejaribu kuangalia kama kuna rekodi yoyote kwenye wizara, hilo sikulikuta, kila awamu inayoingia madaktari nimejaribu kuwasiliana na wale ambao nimeweza kuwasikia kujua kama wanaweza kuja kufanya kazi Zanzibar. Sasa inategemea daktari kilichomuondosha na nini hivi sasa anafanya huko aliko na nafasi aliyonayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, swali langu la (b) halikujibika, nilichouliza je, serikali imechukua hatua gani ya kuwawezesha madaktari hao kurudi nyumbani. Alichoninijibu ni mawasiliano. Kama mawasiliano alikuwa aeleweshe Baraza hili jitihada walizozichukua madaktari wale kurudi. Sijui kanifahamu Mhe. Naibu Waziri! Serikali imechukua hatua gani za kuwezesha madaktari hao kurudi nyumbani kama kweli utafiti umefanyika kujua madaktari hao waliondoka kwa sababu zisizofaa, kwa nini serikali isilete jawabu za jitihada zilizofanyika kuwarejesha madaktari hao, badala ya kusema mawasiliano tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nimesema madaktari wanaondoka kwa sababu tofauti; kama kaolewa kamfuata mumewe, siwezi kumwambia aachishwe kwa mumewe arudi Zanzibar. Kama kaondoka kwa ajili ya maslahi; kapata kazi Umoja wa Mataifa huwezi ukamwambia rudi uje kufanya kazi Zanzibar wakati ana nafasi nzuri kule aliko. Kwa hiyo, inategemea nafasi aliyopo, kuna waliowasiliana waliokuwa wameondoka kwa sababu nyengine wamerudi, Katibu Mkuu wetu Dr. Mohamed Saleh Jidawi alikuwa kaondoka nchini, serikali iliwasiliana naye wakati wa Mhe. Salmin Amour Juma alirudi na tunae mpaka leo hii.

Kwa hiyo ni hicho tu tunachoweza kufanya hatuwezi tukawalazimisha kwa sababu kila mmoja anaondoka kwa sababu anayoifahamu yeye mwenyewe. Maslahi mbali.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mhe Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na yenye ufasaha mkubwa. Mimi nina swali moja tu dogo la nyongeza. Kuna hawa madaktari wetu mabingwa wengi wataalamu ambao Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu kasema wengine wameingia kwenye siasa. Je, wizara wamechukua jitihada gani kuwaomba madaktari wale ambao wako kwenye siasa wakati wa *part time* waweze kujitolea. Nitatoa mfano, kuna Dr. Sira Ubwa Mamboya, Dr. Mohamed Jidawi, ambao wamo katika nafasi za kisiasa kuweza kutoa muda wao kwa ajili ya kuwasaidia hawa madaktari wachache waliokuwepo katika kuwatibu wagonjwa wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ni kweli madaktari tuliopo kidogo na tunacheza ngoma zote mbili za siasa na za utendaji, inategemea wapi mtu yuko. Mimi ni daktari na ni mwanasiasa wakati huo huo, lakini muda wangu mwingi nafikiri nautumia katika udaktari kuliko hiyo siasa, siasa ninayokuja kufanya hapa ni kujibu maswali na kuhakikisha kwamba mambo wizarani yanakwenda vile yanavyopangwa. Dr. Mohamed Saleh Jidawi, Katibu Mkuu, Dr. Jamala Adam Said, Wakurugenzi sote tunafanya kazi *Mnazi Mmoja Hospital* na wale ambao wanakuwa wanasiasa wanapoacha uanasiasa wao huwa tunawaomba na kuna wengi tu ambao wameshaajiriwa kina Dr. Haji Mwita kwa hiyo tuko tunafanya nao kazi.

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea lakini kabla hatujaanza michangio nilikuwa naomba niseme suala moja.

Huku katika orodha yangu kuna Waheshimiwa saba, lakini Waheshimiwa watatu hawapo; wapo Waheshimiwa wanne. Na tumetegemea hii wizara tuichangie mpaka saa 7:00 mchana, jioni tuje tufanye majumuisho. Sasa

wachangiaji wanne hawafikishi saa 7:00. Kwa hivyo, naomba nikiwataja hao wanne kwanza wasitoke wachangie, na wenye haja ya kuchangia tuchangie ili tuweze kuimaliza wizara, ikifika saa 7:00. Wachangiaji ni haba sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, wakati jana jioni nachangia zilikuwa zimebakia dakika zangu kidogo. Mhe. Mwenyekiti, wakati anaendesha Baraza alisema kwamba nitamalizia asubuhi.

Mhe. Naibu Spika: Kwa bahati mbaya Mwenyekiti hakuniarifu lakini nakupa heshima hiyo dakika 10.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa angalau nafasi kidogo ya kumalizia sehemu yangu ambayo nilikuwa nimeibakisha jana.

Mhe. Naibu Spika, jana nilifikia katika Idara ya Nishati, nilikuwa nazungumzia suala zima la kampuni hii ya umeme wa jua ya Wachina wale Huawei. Mhe. Naibu Spika, nilisema kwamba kutokana na semina ambayo walitupatia ndugu zetu wale kampuni ya Kichina wanaonesha kwamba umeme wao ule utakuwa ni wa bei ya chini sana. Sasa nikajiuliza kwamba Wizara au Serikali imefanya bidii gani kuhakikisha kwamba ile kampuni inaruhusiwa na lini itaanza kuwekeza katika suala zima la umeme wa jua.

Kwa sababu wananchi wamekuwa wakipata tabu sana kutokana na tatizo hili la ulipaji wa umeme ambao *ZECO* wamekuwa wakiununua umeme huu kutoka kwa *TANESCO*. Sasa namuomba Mhe. Waziri akija atueleze ni mikakati gani ambayo imechukuliwa kuhakikisha kwamba kampuni hii inaendesha biashara hii ya umeme, kwa kutumia hii teknolojia ya jua.

Mhe. Naibu Spika, la pili ambalo nilikuwa nataka nimalizie nimpongeze Mhe. Waziri kama nilivyosema jana, pamoja na Katibu Mkuu na watendaji katika kubadilika katika utendaji wao. Lakini nasema kwamba kuna changamoto ndogo ndogo ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi kuhakikisha kwamba wizara inakwenda vizuri, kupeleka huduma kwa wananchi wetu katika masuala mazima ya huduma hizi za umeme, ardhi na mambo mengine yanayohusiana na wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, kuna uimarishaji wa miundombinu ya umeme mjini na vijijini katika ukurasa wa 65. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alitueleza hapa kwamba waliweza kununua vifaa vya umeme zikiwemo nguzo na *transformer* katika kufanya miundombinu ya masuala haya ya umeme, na waliweza kununua takriban nguzo 757 na *transformer* 3.

Mhe. Naibu Spika, katika Jimbo langu la Rahaleo eneo la Misufini kuna *transformer* inapata matatizo sana hususan katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhan. Unajua kwamba mwezi mtukufu wa Ramadhan utumiaji wa umeme unakuwa ni mkubwa hasa ikifika katika kipindi kile cha sikukuu. Sasa *transformer* ile nadhani inakuwa inazidiwa nguvu kutokana na utumiaji. Kwa hivyo, wananchi wanakuwa wanapata tabu sana katika kipindi hiki, mara *transformer* imeungua inakuwa tena kukimbizana kupiga simu kwa mafundi. Sasa ningeiomba wizara kuhakikisha kwamba *transformer* ile aidha inawekwa mpya, na kama haiwezekani basi inakuwa inafanyiwa marekebisho mazuri kuhakikisha kwamba umeme pale haukatiki katika kipindi kile cha mwezi wa Ramadhan au katika kipindi cha sikukuu.

Mhe. Naibu Spika, nimesema kwamba kuna changamoto ndogo ndogo. Kuna tatizo la wananchi wangu wa Jimbo la Rahaleo, Shehia ya Mwembeshauri ambao tatizo hili wameshalifikisha katika idara husika na mimi pia kuwasiliana na baadhi ya watendaji lakini tatizo lile bado halijatatuliwa.

Pia katika haya masuala ya miundombinu kuna nguzo ambayo ipo nyuma ya msikiti wa Ijumaa wa Mwembeshauri karibu na geti. Nguzo ile ni mbovu na kipindi ni kirefu, malalamiko yameshapelekwa, mafundi wameshakuja kuangalia, lakini kuiondoa au kuibadilisha nguzo ile bado imekuwa wanapigwa danadana. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri akawasiliana na watendaji. Nadhani Meneja wa Shirika la Umeme yupo ananisikia, kuhakikisha kwamba nguzo ile inabadilishwa, ili kuweza kuondoa matatizo kwa wananchi wetu katika Shehia ya Mwembeshauri.

Mhe. Naibu Spika, nguzo ile itakapoanguka hasara itakuwa ni kubwa; tutaathirika wenyewe na wananchi kwa ujumla. Kwa hivyo, niiombe sana wizara na shirika hili la umeme kuhakikisha kwamba nguzo ile inabadilishwa na kuwekwa nguzo nyengine.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu mchango wangu nimeshautoa toka jana, niiunge mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya Mhe. Waziri. Niwaombe Wajumbe wenzangu kuhakikisha kwamba wanaipitisha bajeti hii ili kuleta maendeleo ya nchi yetu, kwa wananchi wetu wa Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuchangia asubuhi hii. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kunijaalia kuamka salama na kuweza kuichangia hotuba hii ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote kwa kuweza kutuwasilishia hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nianze katika ukurasa wa 15 Taasisi ya Mahakama ya Ardhi. Mhe. Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kuwaongezea wazee wa Mahakama wa Zanzibar kwa Unguja kutoka 6 hadi 17, na kwa Pemba kutoka 5 hadi 6, ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa hukumu zinazotokana na migogoro ya ardhi na kusababisha kukiuka malengo na kufikia hali ya asilimia 179. Mhe. Naibu Spika, niipongeze sana Serikali na Mahakama kwa kuweza kufikia lengo hilo.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba waongeze bidii zaidi, ili kuendelea kuitatua migogoro hiyo. Kwa sababu migogoro hiyo bado ipo na inaendelea wafanye bidii ya kuipunguza ama kuzuia kuongezeka migogoro mipya.

Pia Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chake Mhe. Waziri alisema kwamba Mahakama ya Ardhi ya Mkoa wa Kusini ipo mwishoni kumalizika. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri achukue juhudi za makusudi ili Mahakama hiyo nayo imalizike na kupunguza msongamano wa kesi kurundikana katika vituo vidogo. Nadhani kama ikimalizika Mahakama ile ya Mkoa wa Kusini malalamiko ya Mkoa wa Kusini yatakuwa hayaendi tena kuhukumiwa katika Mahakama ile ya mjini, na pia kutazidi kuhukumu kesi hizo kwa haraka zaidi.

Mhe. Naibu Spika, pia nilikuwa na ombi kwa Mhe. Naibu Waziri kwamba wafanyakazi wa Mahkama ya Ardhi wana kazi kubwa kwani baada ya kupata taarifa ya migogoro hufuatilia katika maeneo mbali mbali ya migogoro. Kwa hivyo, naomba wafanyakazi hawa wapatiwe usafiri ili kuweza kufika katika maeneo ya migogoro kwa urahisi na waweze kuangalia maeneo hayo na kupata utatuzi wa haraka.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Mhe. Naibu Spika, naomba niseme Mhe. Waziri. Idara hii ya Mipango Miji na Vijiji ina mipango mingi mizuri. Mipango mingi ambayo imejipangia inavyoonesha hapa katika kitabu chake Mhe. Waziri anasema kwamba idara hii tayari imeshaandaa mpango kazi imo mbioni kutengeneza sera na sheria, kusomesha na kuimarisha vitengo vya utafiti. Lakini kila bajeti inapokuja inakuwa ni haya kwa haya. Nataka kumuuliza Mhe. Waziri. Ni lini hasa kazi hii itamalizika ili idara hii iweze kutupangia miji na vijiji vyetu kwa mpangilio?

Kwa sababu hivi sasa ukiangalia katika miji na vijiji vyetu hakuna mpangilio mzuri watu wanajijengea ovyo. Leo utapitisha gari labda unakwenda sehemu fulani, kesho ukipita tayari pameshajengwa njia haipo tena. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba kazi hii imalizike ili idara hii iweze kutupangia miji yetu kwa ajili ya kurahisisha watu kufika katika maeneo bila ya matatizo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Idara ya Ujenzi. Mhe. Naibu Spika, naomba kwa dhati kabisa niipongeze idara hii kwa ukamilishaji wake wa *flats* 24 za Mpapa na hivi sasa tayari zimeshahamiwa na baadhi ya wananchi wa maeneo yale wanaishi katika nyumba zile.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna matatizo mengi ya majengo haya; kwa mfano kuna majengo mengine mabovu Mtemani kule Pemba, kuna majengo yale ya Kengeja. Naomba Mhe. Waziri aifanye juhudi kwa makusudi katika maeneo yale, waingiziwe fedha ili waweze kuyatengeneza kwa sababu yapo katika hali mbaya. Majengo yale wanaishi watu na mengine hawaishi watu lakini pia yanaweza kuhatarisha kwa sababu yanaweza kuporomoka halafu yakaathiri

watu. Hasa jengo la Kengeja ni baya, na bovu kupita kiasi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri afanye juhudi za makusudi ili kuwaingizia fedha idara hii waweze kuyarekebisha yale majengo ambayo yana matatizo makubwa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe ukurasa wa 38. Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe katika maelezo yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba katika ukaguzi wao kuna nyumba 40 ambazo hazikaliki kabisa na wale wamiliki wa zile nyumba wanahamasishwa lakini bado hawajahamasika kuzitengeneza nyumba zile.

Mhe. Naibu Spika, naomba idara hii kupitia Serikali yetu ifanye juhudi za makusudi. Kwa sababu kuna baadhi ya majengo ya Mji Mkongwe yapo hatarini, halafu ni sehemu ambazo wanaishi au wanapita watu. Mwenyezi Mungu atunusuru linaweza likatokea jambo lolote katika majumba yale. Mhe. Naibu Spika, naomba idara itumie wataalam wake na izidi kuwahamasisha wale wananchi ambao wenye kumiliki majengo yale, lakini pia nayo Serikali itie mkono wake katika kuyatengeneza majengo yale ili yasije yakatuletea athari kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo Mamlaka ya Mji Mkongwe naomba nichangie Mradi wa Ukuta wa Ukingo wa Baharini. Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa kwenye Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi tulikwenda kule tukaoneshwa ramani, lakini hiyo ramani mpaka sasa hivi imekuwa ni muda mrefu na utekelezaji wake bado mpaka leo. Ramani hiyo kama itafuatwa vile ilivyo ni nzuri sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aniambie ni lini hasa ukuta ule wa ukingo wa bahari utajengwa, ili kuweza kuweka mandhari nzuri katika Mji Mkongwe, na ile dhana hasa ya uhifadhi wa Mji Mkongwe waoneshe mandhari nzuri.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Mamlaka ya Maji. Mhe. Naibu Spika, nimpongeze kwa dhati kabisa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji pamoja na watendaji wake kwa juhudi yao kubwa wanayoichukua ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama. Mhe. Naibu Spika, maeneo mengi yalikuwa hayana maji lakini sasa hivi maji yanapatikana iwe kwa mgao ama kwa vyovyote vile.

Mhe. Naibu Spika, nikiangalia ukurasa wa 43 katika jadweli namba 4 inaonesha kwamba katika maeneo ya Bambi, Bambi Uwandani, Bambi Matora, Matemwe Kigomani, Tunguu, Unguja Ukuu na Kilindi kwa hapa Zanzibar. Wanasema kwamba kazi hii imekamilika. Mhe. Naibu Spika, nataka kueleza kwamba kweli kazi hii imekamilika na sasa hivi wananchi wa Bambi na Bambi Matora wanapata maji vizuri.

Mhe. Naibu Spika, niwapongeze kwa juhudi zao hizi lakini naomba kwa hivi vijiji vyengine ambavyo kazi inaendelea wachukue juhudi ili kazi zimalizike na wananchi waweze kupata maji, hasa ukizingatia kwamba kesho kutwa mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia ule utaratibu wao wa kipindi cha mwezi wa Ramadhani wa kupeleka magari ya maji yale maeneo ambayo hayana maji uendelee. Kwa sababu mwezi wa Ramadhani ni kipindi ambacho maji yanatumika sana, halafu wananchi wanakuwa wamefunga, inakuwa tabu kwenda kutafuta maji.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba Mamlaka ya Maji tukishirikiana na sisi Wawakilishi tuweze kuwahamasisha wananchi ili wale ambao wanapata maji, kuweza kulipia huduma ili fedha zile ziweze kutumika kwenye mamlaka ili ziweze kutanua huduma hizi au kuipa nguvu mamlaka ili iweze kutekeleza kazi zake vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba Wawakilishi wenzangu kwa kushirikiana na wananchi na Masheha na Mamlaka ya Maji, pia tuwahamasishe wananchi wetu ili wasivamie vianzio vya maji ili maji yaweze kupatikana vizuri. Kwa sababu chanzo kikubwa cha ukosefu wa maji ni wananchi kuvamia maeneo ya vianzio vya maji, halafu sisi wananchi tunalalamika kwamba maji hayapatikani lakini kumbe chanzo ni sisi wenyewe. Hivyo, Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu naomba tuwahamasishe wananchi hao ili vianzio visivamiwe, ili maji yaweze kupatikana vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa Shirika la Umeme. Mhe. Naibu Spika, shirika hili kuna tatizo la wafanyakazi vishoka, ni tatizo kubwa. Wafanyakazi hawa huwa wanatega pale wananchi wakitaka kuingia pale, anamuuliza unataka umeme, unataka kuungiwa umeme. Kama mwananchi anataka kuungiwa umeme, vishoka wale wanakuwa wanawalaghai wanawaambia nitakutengenezea, ukenda huko ndani utapata matatizo, utachelewa. Kwa hivyo, wacha mimi nikakutengenezee. Lakini baada ya kwisha kuungiwa umeme wanakuwa hawapi risiti. Baada ya shirika

kugundua kwamba kuna watu hawalipi au hawakuungiwa kisheria, inakuwa ile adhabu inawapata wale kwa kukatiwa na kulipishwa faini kubwa wananchi wale.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba Meneja wa Shirika la Umeme aweze kudhibiti hawa vishoka. Vishoka hawa wanalivunjia hadhi shirika, wanalitoa thamani shirika kutokana na kazi hii wanayoifanya ya kuungiwa watu umeme bila ya utaratibu. Hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba sana Meneja wa shirika awafuatilie wafanyakazi hawa na awape adhabu, ili wengine wasiendelee na kadhia hii.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka kuchangia katika ukurasa wa 63 kwamba kuna baadhi ya sehemu bado mpaka leo zina upungufu wa umeme; umeme wake unakuwa ni mdogo. Katika kitabu chake cha Mhe. Waziri nambari 63 nimeona kwamba shirika limefunga mtambo wa *capacity bank* katika maeneo, ameyataja hapa pamoja na Mwera. Mhe. Naibu Spika, Mwera ni kubwa, bado kuna maeneo ya Mwera kule kule umeme wake ni mdogo, ikifika usiku taa haziwaki, matumizi mengine hayapatikani. Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, Meneja katika hayo maeneo aliyosema kwamba yametiwa *capacity bank* ayafanyie utafiti na maeneo mbali mbali ambayo pia yana matatizo ya umeme, ili waweze kuweka *capacity bank*, ili na maeneo yale yaweze kufaidika na umeme.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hiyo na ninaunga mkono kwa asilimia mia. Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante mheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea tumepata ugeni hapa juu, na ugeni huu ni timu inayoitwa *Villa Sports Club*, umaarufu wake Mpira Pesa ya Mwanakwerekwe. Imekuja na wachezaji 24. Wao ni mabingwa wa *Central league* katika Wilaya ya Mjini. (*Makofi*)

Kiongozi wao anayeongoza msafara ni *team manager* anaitwa Ndugu Abdul-rabi Khamis. Namuomba asimame. Ahsante sana kaa kitako, akifuatana na Ndugu Abdalla Khamis ambaye yeye ni *team manager*, kuna kocha Ndugu Mohammed Yussuf Dadi na Mshauri wa timu, Mhe. Dau Hamad Maulid. (*Makofi*)

Mhe. Dau Hamad Maulid, yeye ni mgonjwa lakini timu imekuja na vijana 24 wasimame. Hao ndio mabingwa wa *Central League* Wilaya ya Mjini kwa mwaka huu. Tunawapongeza sana, wamekuja na kombe lao.

Ahsanteni sana tunawapongeza, kaeni kitako. (*Makofi*)

Tunaendelea sasa ni zamu ya Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa baadae atafuatia Mhe. Mohammed Haji Khalid na baadae Mhe. Bikame Yussuf Hamad na Mhe. Fatma Mbarouk Said ajitayarishe.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwa asubuhi hii ya leo kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Azza wa Jaallah*. Pia nikushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Lakini shukurani zangu za dhati kabisa ziende kwa Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Makatibu pamoja na watendaji wote wa wizara hii, kutokana na kazi kubwa na nzito wanayoendelea kuifanya katika wizara hii. (*Makofi*)

Vile vile nitakuwa muhaba wa fadhila kama sikuwashukuru wana kamati wenzangu ambao kwa pamoja tunashirikiana kuhakikisha kwamba tunasaidiana, kuelekezana na kuongozana katika kuziongoza wizara hizi mbili; Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sasa vile vile ninapenda kutoa shukurani na pongezi maalum kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar, kutokana na kazi kubwa na nzito ambayo wanaendelea kuifanya katika kuhakikisha kwamba wanawasaidia wananchi wa Zanzibar kupata maji safi na salama ndani ya visiwa vyetu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na matatizo tuliyonayo, pahala popote pale penye maendeleo changamoto hazikosekani. Vile vile tukiangalia tulipotoka Mhe. Naibu Spika, miaka michache iliyopita tulipokuwa tunakuja hapa, kuja kuizungumzia bajeti ya wizara hii, ilikuwa mpaka Mawaziri wapo tumbo joto. Hawajui namna gani itaweza bajeti

yao kupita lakini tunashukuru sasa hivi bajeti hii inapokuja hapa, inakuwa kama bajeti nyengine za kawaida na wala Waziri pamoja na watendaji wake hawapati changamoto, kama ambazo walizokuwa wanazipata hapo nyuma.

Hii inatokana na juhudi, maarifa pamoja na uongozi mzuri unaosimamiwa na Mzee wetu Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kama waziri katika wizara hii. Ninampa hongera sana Mhe. Waziri na hapa palipobakia katika matatizo ambayo yanaendelea kutukabili, matatizo ya maji, *inshaallah* yamalizike na hususan katika Ramadhani hii inayokuja mbele yetu. Wananchi wa Zanzibar wapate maji ya salama na safi na kwa uhakika katika maeneo ambayo wanaishi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi leo sitokuwa na michango mingi hususan ukitilia maanani kwamba wizara hii ni moja kati ya wizara ambazo ninazisimamia. Kwa msingi huo basi, mimi mchango wangu ni mdogo lakini utakuwa na umuhimu kwa mantiki yake.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa, namuomba Mhe. Waziri atusaidie kuhakikisha kwamba katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani unaokuja, kwa yale maeneo ambayo bado hayajapata huduma za maji, tuhakikishe kwamba maji yanapelekwa na wananchi wanapata maji safi na salama na waondokane na dhiki na matatizo kwenye mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Yale maeneo ambayo yalikuwa yana matatizo ya kuharibika kwa mashine na kila kitu Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri pia ahakikishe kwamba kwenye kipindi hiki kifupi kilichobaki, maeneo hayo yanatatuliwa matatizo hayo na watu wanapata maji safi na salama.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa, nakuja katika suala zima ambalo linaniumiza kichwa baadhi ya nyakati. Juzi Mhe. Naibu Spika, tulipokuwa hapa tunapitisha baadhi ya bajeti kulikuwa kuna Wajumbe walichangia katika suala zima la upungufu wa nyumba katika maeneo yetu ya Zanzibar kwa baadhi ya viongozi.

Nikiondoka huko Mhe. Naibu Spika, nakuja katika ziara ambayo ilikuwa imechukua Wajumbe kadhaa kutoka Zanzibar ambao wakiongozwa na Makamu wa Pili wa Rais, walipofanya ziara kule Marekani. Katika ziara yao kule Marekani walipata kufanya mazungumzo na baadhi ya wawekezaji ambao wawekezaji hao walikuwa wanataka wapewe eneo huku Zanzibar kwa ajili ya kutusaidia katika ujenzi wa nyumba ambazo zitawasaidia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nina masikitiko makubwa sana, mbali ya viongozi ambao wanakosa makaazi ya uhakika katika maeneo ya Zanzibar kwa nafasi tulizowapa, lakini pia kunakuwa na matatizo ya nyumba zimetelekezwa pamoja na viwanda ambavyo umiliki wake na matumizi yake hayaridhishi kwa mujibu wa taratibu zetu za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa, katika eneo la Mazizini tulijaribu kufanya ziara na kufanya utafiti, tumegundua kwamba kuna nyumba zaidi ya 10 za serikali ambazo zipo maeneo ya Mazizini. Utaratibu wake wa matumizi haupo katika taratibu za kisheria. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie nyumba zile kwa nini zimeachwa kama zilivyo, hali ya kwamba serikali inahitaji nyumba. Wanaotumia nyumba zile ni watu ambao tayari sheria haikubali waendelee kuzitumia.

Tunaomba kwanza atuthibitishie nyumba hizo ni ngapi, wanaotumia ni akina nani na lini wataondoka katika maeneo hayo, ili serikali iweze kupanga mikakati na mipango mengine endelevu ya kuhakikisha kwamba mipango yake inakuwa mizuri kama ambavyo tunatarajia.

Baada ya hatua hiyo, sasa jambo jengine ambalo nilikuwa ninataka kuchangia Mhe. Naibu Spika, ni suala zima la umeme. Jana tulishuhudia nchi yetu kuingia katika kiza kwa muda fulani hivi. Tulipata matatizo ya umeme kwa Tanzania nzima kwa muda maalum. Mhe. Naibu Spika, tatizo hili ukiangalia linatokana na kwamba kuendelea kutegemea chanzo kimoja tu cha umeme.

Mhe. Naibu Spika, kuna ndugu zetu hawa ambao ni kampuni kubwa sana na imewahi kuja Zanzibar hapa na kutupatia semina sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, juu ya suala zima la kutusaidia katika suala la umeme wa jua. Kwa bahati nzuri Mhe. Naibu Spika, katika ziara ambazo unakuwa unatupangia, uliwahi kutupeleka China kule na kukutana na kampuni hii ya *Huawei*, kule China.

Kampuni hii kwa sasa ina ofisi zake Dar es Salaam ambapo pia tulibahatika kwenda. Lakini pia uongozi wa kampuni hii ulibahatika kuja Zanzibar na kuja kuonana na mimi, kama mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na kufanya maongezi ambayo yanaweza kusaidia suala la upatikanaji wa umeme wa jua ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar na kuwa na umeme wa uhakika.

Mhe. Naibu Spika, kwa tatizo ambalo liliendelea kujitokeza jana, naomba Mhe. Waziri atapokuja hapa anisaidie ni namna gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kuitumia kampuni hii kubwa ambayo ni ya tatu kwa ukubwa duniani, katika kuhakikisha kwamba inasaidia masuala ya upatikanaji wa umeme mbadala wa jua ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nilipofanya utafiti na kufanya mazungumzo na watu hawa, walinithibitishia kwamba wanaweza kutupatia umeme Zanzibar *megawatt 52* ambazo zinatosha kwa matumizi ya Zanzibar kwenye suala la umeme. Ukiangalia gharama za uendeshaji si zaidi ya dola milioni mbili za Kimarekani ambapo kama tukiangalia ni chini ya bilioni tatu za Kitanzania kwa gharama za umeme wa jua, kwa matumizi ya Zanzibar. Matumizi haya kwa gharama hizi unakuwa na uhakika wa kutumia umeme kwa muda miaka 25.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ningeliomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie, kwa sababu hata ukitizama umeme ambao tunaotumia kwa sasa hivi, *unit* moja si chini ya shilingi 312. Wakati kampuni hii ya Kichina kama watakubalika na kufuata taratibu za kinchi, tunaweza tukapata umeme ambao utakuwa chini ya shilingi 200.

Sasa naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie kutuelekeza ni namna gani serikali ipo tayari kushirikiana na kampuni hii kubwa kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanapata umeme mbadala na kwa manufaa ya maendeleo na maslahi ya nchi yetu.

Baada ya maelekezo hayo na kwa sababu mengi tumekwishakuyasema katika ripoti yetu, kubwa zaidi ambalo ninapaswa kuzungumza kwa sasa ni kuwaomba Wajumbe wa Baraza hili lako tukufu, waipitie hotuba ya bajeti ya Waziri pamoja na hotuba ya Kamati na wachangie, na hatimaye waikubali bajeti hii na kuipitisha kwa maslahi ya wizara na nchi yetu ya Zanzibar kwa ujumla.

Baada ya maelekezo hayo, ninakubaliana na hotuba hii na ninaunga mkono kwa asilimia 100 lakini hapo hapo nikitaka majibu yangu nipatiwe.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa. Sasa nafasi tunampa Mhe. Mohammed Haji Khalid, baadae Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Fatma Mbarouk Said na baadaye Mhe. Abdalla Mohammed Ali ajiandae.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi asubuhi hii kupata nafasi ya kusema machache sana katika Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha leo kufika hapa kuendelea na kazi zetu za kawaida. Aidha, nikushkuru na wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa hii nafasi na nimpongeze sana kweli kweli Mhe. Waziri wa wizara hii, Manaibu wake na watendaji wao wote kwa jitihada kubwa wanazochukua katika kuondoa matatizo ya nchi kupitia wizara yao.

Mhe. Naibu Spika, Wizara hii inaitwa ni Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Sasa kama si wizara hii, wizara nyengine zote zingelikuwa hazipo. Kwa nini? Kwa sababu wizara hii ndio yenye ardhi na vyengine vyote vimo humu ardhini. (*Makofi*)

Kwa hivyo, kwa kuwa vitu vyengine vyote vipo ardhini, wizara hii ndio wizara kubwa kuliko wizara zote. Matatizo yake ni makubwa pengine kuliko yakutoka wizara nyenginezo. Lakini kwa umahiri wa Mhe. Waziri aliyeopo anajitahidi kwa kima kikubwa kujaribu kupunguza na ikiwezekana kuondoa matatizo mengi.

Mhe. Naibu Spika, ardhi ina umuhimu wake, maji yana umuhimu wake na ardhi imeumbika kwa sehemu mbili kubwa. Ni ardhi yenyewe na maji. Inasemekana hii dunia, robo tatu ya dunia ni maji. Yakiwemo maji ya bahari, maziwa, mito na mengineo. Robo moja tu ndio hiyo ardhi ambayo tunaishi viumbe tunaoishi nchi kavu. Kwa hivyo, hapa tuone huu umuhimu wa ardhi. Hivyo kwa sababu ardhi ina umuhimu wake, mimi nianze mchango wangu katika usimamizi wa ukodishaji wa ardhi ambao ninataka niangalie kwenye ukurasa 12, nina masuala machache ambayo ninataka nichangie pale kwenye ukodishaji wa ardhi.

Mhe. Naibu Spika, hapa Mhe. Waziri katueleza kuwa, kuimarisha uwekezaji wa ardhi, katika kuendeleza mfumo mpya wa udhibiti wa ardhi, kumbukumbu za ardhi zikijumuisha uwekaji... Sipo nilipokusudia.

Mhe. Naibu Spika, tumesema hapa kuna wawekezaji kadhaa katika ardhi ambapo hii ardhi ni kama tumeikodisha. Sasa nataka kujua hii ardhi katika ukodishwaji wake, inakodishwa kwa muda gani na serikali inapata kiasi gani. Je, katika wawekezaji hawa kuna wazalendo na kama wapo ni wangapi. Pale muda unapomalizika kwa kuwa wawekezaji wengine huwa wameekeza katika ujenzi wa mahoteli na mambo mengineyo, ile mali iliopo na muda umemalizika, mali zile zinakuwa ni za nani.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Mahakama ya Ardhi; hapa nitakuwa na mchango mdogo na visuali vidogo vile vile. Hapa imeelezwa kwamba kesi zilizopokelewa ni 120 kwa Unguja na kesi zilizotolewa hukumu ni 147. Pemba zilizopokelewa ni 92 na zilizotolewa hukumu ni 104. Kwa hivyo, hapa naomba nipate ufafanuzi, kwa sababu hakuna kesi za nyuma zilizotajwa. Kama zingekuwa zimetajwa kesi za nyuma ningekuwa sina suali, lakini zimetajwa kesi chache lakini zilizotolewa hukumu ni nyingi. Je, zile nyengine zimetoka wapi kutolewa hukumu wakati ambao hazijatajwa kuwa zipo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu hii Mahakama ya Ardhi; niingie katika kuongeza hawa wazee wa Mahakama ya Ardhi. Hili ni jambo zuri kwa sababu inasaidia kuendesha kazi vizuri, lakini ningeomba nijuwe huu uwiano wa kuongeza baina ya Unguja na Pemba. Hapo mwanzo Unguja walikuwa wazee hawa ni sita na Pemba walikuwa ni watano, hapa uwiano haukuwa mzuri kwa sababu, kwenye uwiano unaonesha kuwa Pemba kulikuwa kuna watu wengi zaidi kuliko Unguja, ingawaje watano ni kidogo kuliko sita, lakini kiuwiano kwa sababu Pemba ni ndogo kuliko Unguja, hapa Pemba ilikuwa iwe na wengi zaidi kuliko Unguja, ingawaje ni watano kwa sita, lakini hao watano ni wengi kuliko sita ukitizama kiuwiano.

Pia Unguja imefika katika sita kuingia 17, kuna ongezeko kama la watu 11 na hawa wametoka kutoka tano hadi tisa, kunaongezeko la watu wanne pia hapa uwiano haukwenda vyema. Kwa hivyo, ningeomba serikali au wizara inieleze vyongeza hizi zimekwenda namna gani katika kuleta uwiano huu.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Mamlaka ya Maji; pale mwanzo nilisema kwamba dunia sehemu kubwa imefanyika kwa maji; robo tatu ya dunia ni maji. Lakini bado nchini kwetu tuna matatizo ya maji, pamoja na jitihada kubwa na juhudi nyingi zinazochukuliwa na serikali, lakini bado tunao uchache wa maji katika maeneo yetu mbali mbali. Nasema tuna uchache wa maji kwa sababu maji ni jambo ambalo linahitajika kila siku na kila wakati.

Leo kuna maeneo yana mgao wa maji katika wiki siku moja, eneo jengine katika wiki siku mbili na jengine katika wiki mbili siku moja. Kwa hivyo, katika mfumo huu inaonesha kwamba hata pale maji yanapopatikana ina maana bado maji hayajawa ya kutosha. Kwa hivyo, jitihada na juhudi zinahitajika zaidi, ili kuondoa tatizo la maji kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye tatizo la maji kwa eneo ambalo nalitumikia yaani Jimbo langu la Mtambile. Nianze kule niliko mimi Kengeja. Katika sehemu ambayo ina tatizo la maji kuliko sehemu nyengine zote basi ni Kengeja. Kengeja wana kisima kimoja ambacho kipo pahala tunapaita Mazrui na panaitwa Mazrui kwa sababu Mhe. Mazrui wakati ule alijenga kule Skuli ya Ufundi Kengeja. Kwa hivyo, kule Kengeja ile skuli inaitwa Skuli ya Mzrui, lakini sio jina la serikali ni jina la Kengeja. Jina lake ni Skuli ya Sekondari ya Ufundi ya Kengeja.

Kule kipo kisima cha maji ambacho hakikidhi haja ya watu wa Kengeja, ambapo barabarani kipo kisima chengine cha zamani, lakini visima vyote hivi viwili havikidhi mahitaji ya maji ya watu wa Kengeja. Hivi sasa mgao unakuwa pengine kwa wiki nzima watu wanapata maji mara moja katika sehemu zao, hii ni kuonesha kwamba maji Kengeja hakuna.

Mhe. Naibu Spika, uzoefu nilio nao kwa kule kwetu Pemba, zaidi kule Kengeja. Katika Mwezi wa Ramadhani inaonesha kama wafanyakazi wa sehemu hii wanawakomoa watu. Maana yake pamoja na kuwa maji ni shida, lakini Mwezi wa Ramadhani ile shida inaongezeka zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana mimi tulifunga Ramadhani hapa, lakini mara zote tulikuwa tunauliza maji maji, kuanzia siku ya kwanza ya Ramadhani maji hayakupatikana, yalikuja kupatikana Mwezi 29 wa Ramadhani, kwa mwezi mzima maji kwenye kisima yapo, miundombinu inafanyakazi, ugawaji wa kawaida upo, lakini katika eneo langu halikupata maji kwa mwezi mzima wa Ramadhani. Kwa hivyo, lengo la baadhi ya wafanyakazi ni kuwakomoa watu na huduma hii muhimu sana. Kwa hivyo, ningekuomba Mhe. Waziri suala hili ulione, ulisimamie na kama hakuna matatizo makubwa basi lazima mtindo huu ukome. Sijui nimetumia neno baya, basi mtindo huu usite.

Mhe. Naibu Spika, si vyema watu kupata matatizo kwa huduma ambayo uwezekano wa kupatikana upo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba katika mahangaiko yako yote ya huduma za maji, naomba uhakikishe ndani ya bajeti hii Kengeja unaitazama kwa jicho la kweli kweli. Wala usijekunijibu vyengine, kwa sababu watu wengi wanaona siasa ni uongo, siasa sio uongo bwana, watu wanasema atakujibu kisiasa tu, hapana. Mimi naamini kwamba siasa sio uongo, uje unijibu ki kweli kweli ni vipi tutaweza kupata maji ya kututosheleza watu wa Kengeja.

Tatizo kama hili pia lipo Mtambile, pamoja na kuwa pana visima wiwili; kimoja kipo skuli na chengine kipo njiani Kongeani pale, lakini bado havikidhi mahitaji ya maji ya watu wanaoishi Mtambile. Kangani kwa kiasi fulani tatizo la maji sio kubwa sana, sisemi kuwa halipo, lakini sio kubwa sana kama ilivyo Kengeja na Mtambile. Kangali ni kwa baadhi ya vijiji tu, yale maji miundombinu yake haijafika, lakini kama ikifika kwa maji yaliopo ni imani yangu yatatosheleza kwa wakaazi wa sehemu ile.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nije katika nyumba na nitasemea nyumba moja tu ile ya Kengeja. Mhe. Naibu Spika, nyumba ile ni mbovu kweli kweli. Katika bajeti ya mwaka jana ilitajwa kuwa itafanyiwa matengenezo makubwa, lakini haikufanyiwa hata tengenezo dogo. Mara hii katika idara haikutajwa, lakini imetajwa katika Ofisi Kuu Pemba kuwa ni miongoni mwa nyumba ambazo zitafanyiwa matengenezo.

Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri hili jumba mlipe kipaumbele. Pia namuomba na Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu ni mradi wa Pemba, ile Ofisi Kuu Pemba iingiziwe OC zake kwa mtiririko mzuri, ili waweze kuendesha kazi zao kwa kawaida. Kwa sababu kuwakwamisha kwa kutokuwatilia pesa ni kuwadumaza katika utendaji wao wa kazi.

Mhe. Naibu Spika, pia nizungumze kidogo kwenye Shirika la Umeme; hapa nina ombi maalum kutoka kwenye jimbo langu. Mhe. Naibu Spika, namuomba kwa heshima zote Mhe. Waziri anipatie *transformer* katika kijiji changu kimoja cha Mkungu. Kule Pemba kuna Mkungu mbili, sio Mkungu wa Ngwachani, ni Mkungu ya Kengeja. *Transformer* hiyo tukiipata tutaweza kutumia kwa vijiji kadhaa kama Jaani, Mitatuni na Kidutani. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri apande akishuka, apige mbizi azame akizuka anipatie *transformer* pale katika kijiji cha Mkungu.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri wajitahidi kufunga hizi mita za Tukuza, ili kupunguza matatizo ya madeni. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya mwahala wasoma mita huwa hawapiti, baadaye wanakisia tu kwa mwezi huu huyu anaweza kutumia shilingi 40,000, lakini kumbe matumizi yake ni kasoro ya hata 20,000. Unaletewa *bill* ukiitazama unatia mkono mdomoni, ilikuwaje na kwa matumizi gani, kumbe ni makisio tu.

Kwa hivyo, munawasababishia matatizo watumiaji wetu, lakini hili litaweza kuondoka pindipo tukifunga Tukuza, mtu kama hakulipa hana wa kumlaumu wala hafuatwi kuja kumkatia, kwa sababu kama hakulipa anakaa tu yeye mwenyewe ndiye anayekosa huduma. Lakini kumkatia pengine kachelewa kulipa na kwa mawazo yake lile deni halifiki kima kile, basi itakuwa hatukumtendea haki.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningeomba pale mnapotoa ahadi basi tujaribu kuzitekeleza ahadi zetu kwa kadiri ya uwezo wetu unavyoturuhusu. Katika sehemu mbali mbali zaidi ni maombi ya umeme na maji hivyo, tuyazingatie kwa kiasi fulani katika sehemu zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijamaliza nilitaka nioneshe kuwa wizara hii ni wizara kubwa na yenye mambo muhimu ya ardhi, ina maji, ina nishati, na ina majenzi. Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango Miji ningeomba isimamie kazi zake vizuri, kwa sababu watu tunaendelea kujenga kiholela na hatimaye inatokezea watu kuvunjiwa nyumba.

Kwa hivyo, serikali isingojee mtu mpaka akamaliza kujenga, iweje tumngoje ajengee pale ambapo haparuhusiki. Tukimuona mtu anajenga pahala sipo basi tumuambie. Hapa nataka kushauri kwa pande zote mbili, kwa serikali na kwa sisi wananchi.

Mhe. Naibu Spika, naomba watu tukumbuke neno hili fupi la Kiingereza linaloitwa *ask*, *ask* maana yake ni kuuliza. Lakini kuna watu wametafsiri kila herufi na maana yake. A ndio hiyo maana yake *ask* yaani uliza. Mimi nitakapojenga pahala sina uhakika niende nikaulize kunakohusika, kuwa ninataka kujenga pahala fulani vipi. Ukiuliza utajibiwa. *Ask it to be told,* kwa hivyo niulize nitajibiwa.*(Makofi)*

S seek tafuta, ukitafuta utaona au utaoneshwa na *K* ni *knock* hodisha utafunguliwa mlango. Sasa sisi wananchi na wizara sote tuwe na hisia hiyo. Mimi nataka kufanya kitu ili nisipate matatizo niulize. Serikali inamuona mtu anafanya kitu ambacho sicho basi wamgongee wakamuambie Sheikh hapa usijenge, pana chanzo chetu cha maji au Sheikh hapa usijenge ni sehemu ya kilimo. Kwa hivyo, tusingojee mpaka keshajenga halafu ndio tukatoka na *bulldozer* na kuambiwa umejenga sipo unavunjiwa, basi itakuwa bado pande mbili hizi hazijatendeana haki.

Mhe. Naibu Spika, kuna msemo wa zamani wa Kiingereza unasema "*If wishes were horses, beggars could ride"*. Sisi raia ni waombaji tunaomba wapi, serikalini. Sasa kama matakwa yetu yote tunayotaka serikalini yanakubaliwa basi waombaji tungefaidika sana. Hapa *horse* hajakusudiwa kuwa ni Farasi, kama matakwa yangekubalika basi waombaji wangefaidika sana.

Sisi serikalini tunataka mengi, kama serikali ingetutekelezea yale tunayotaka basi matatizo kwa kiasi kikubwa yangeondoka. Lakini baadhi ya wakati tunaomba kitu ambacho kinawezekana na kitakosekana, kwa hivyo baada ya kuwa hawa *beggars could ride* wangefaidika, sasa *beggars* tunageuka kuilaumu serikali. Kwa hivyo, pale ambapo lawama sio za msingi basi serikali ijitahidi kuwahudumia watu, ili watu wawe na imani na serikali yao.

Mhe. Naibu Spika, migogoro ya ardhi ipo na hii ndio wizara inayohusika, ijitahidi kadiri ya uwezo wake ijaribu kupunguza na kuondoa mizozo na migogoro ya ardhi, mbali ya kuwa ardhi ni sehemu ya mali ya serikali au ya taifa. Kwa kweli Zanzibar mara nyingi nasema kabla haijakuwa hivyo kila sehemu ndogo hata mita moja ya ardhi ya Zanzibar ina mwenyewe na mtu atakujia na waraka kwa siku hizo inaitwa hati kwamba pale ni pake au kwa babu yake.

Kwa mfano, hapa tulipo nina hakika yupo mtu anao waraka kuwa ni pake yeye hapa na hata uwe ume-*expire*, lakini ukionesha huko nyuma kila sehemu ya ardhi ya Zanzibar ilikuwa inamilikiwa na mtu na utawala uliokuwepo ndio ilikuwa hivyo na Bara haikuwa hivyo, wakati Mjerumani alipotawala tokea zamani ardhi ni mali ya taifa.

Kwa hivyo, kule mtu sehemu anayokatiwa ndio anakatiwa ikiwa haina mwenyewe, isipokuwa yule anayepewa anapewa kwa matumizi ya wakati ule na ikimshinda na serikali ikimnyang'anya haijafanya kosa, kwa sababu amepewa kwa matumizi na imemshinda.

Mhe. Naibu Spika, hata na sisi hapa hii dhana za serikali kwamba ardhi ni mali ya taifa itumike vyema. Kwa mfano, pale tulipompa mwekezaji na akashindwa kuitumia isiwe kosa kuichukua, "*should be satisfied so as to maintain justice*" tusione kuwa tumempa fulani na imemshinda, lakini kumnyang'anya tunaona tabu, sheria ifanye kazi yake, ili haki itendeke na wala tusione kuwa bwana fulani mwenzetu wa zamani hatuwezi kumfanyia hivi, nadhani ni vyema tuchukue hatua za kisheria, ili haki itendeke. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sitaki niseme mengine, lakini nifanye kama ripoti kwa maji, kwa sababu maji wako baadhi ya wana-*science* waliosema kwamba maji ni sehemu ya chakula na wengine walifanya kwa *Carbohydrate, Protein, Mineral Salt* na *Vitamin* na yuko mmoja peke yake ameongeza maji kuwa ni sehemu ya chakula hata kuwa hayaliwi, lakini hivi vyengine vyote bila ya maji havitokwenda.

Mhe. Naibu Spika, hivi vyakula wewe huna, isipokuwa maji unayo, ili tupike lazima tupate maji, ili tupike lazima tupate nishati, ili tupike lazima tupate pahala pa kukaa na kuweza kupika chakula chetu, ili tuishi lazima tupate nyumba. Kwa hivyo, kila kitu ambacho kinahitajika kiko juu ya mgongo wanko *pull up your socks*. Ahsante sana, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa fursa hii kwa ajili ya kutoa mchango wangu mdogo katika hotuba ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu pia kumtakia Mtume wetu Muhammad rehema na amani juu, kwa kuweza kutukutanisha hapa tukiwa katika hali ya afya njema na uzima na huko tunakotoka.

Vile vile nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa jumla kwa kazi ngumu na kubwa kama walivyosema wengi waliotangulia kuchangia katika wizara hii kwamba ni majukumu makubwa wanayopewa wizara hii.

Kwa hivyo, nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa kwa utendaji wao na mambo ya hapa na pale yanayowakuta, lakini changamoto ni jumla ya maisha. Kwa maana hiyo, na wao wanajitahidi na wanastahiki pongezi na tuwashukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu leo sitaki niende kwenye kitabu cha Mhe. Waziri, isipokuwa ninayo mambo yangu ambayo ninahitaji kupatiwa ufafanuzi kidogo, ili niweze kuridhika na yale mambo yangu ambayo nilitaka niyaseme katika wizara hii.

Kwanza niwapongeze katika kitabu chao hiki kwenye ukurasa wa 10 miongoni mwa changamoto ambayo hata hotuba ya maoni ya kamati ni kuhusu ukosefu au upungufu wa wafanyakazi, lakini kwenye kitabu chao hiki Mhe. Waziri ametueleza kuwa jumla ya wafanyakazi 65 ambao kuwa wameajiriwa ndani ya wizara yake. Kwa hiyo, ni moja ya faraja na miongoni mwa changamoto moja kufika pahala wakaonewa huruma wakapewa au wakaajiriwa hawa wafanyakazi 65, si jambo dogo ninawashukuru na tunaishukuru Wizara ya Nchi, (OR), Kazi na Utumishi wa Umma kwa kuwatekelezea hilo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine Mhe. Waziri naomba anipe ufafanuzi katika usimamizi wa ukodishwaji wa ardhi kwenye kitabu chake hiki ukurasa wa 12 amesema kwamba; jumla ya mikataba 70 inayokodishwa nafikiri katika kipindi hiki.

Vile vile huku mwisho kuna ukodishwaji mmoja kwa ajili ya skuli na hili pia nataka nipate ufafanuzi kama skuli hii ya *private* au ya serikali na kama ni skuli ya serikali kwa nini kuwe na ukodishwaji wa eneo hili la ardhi na lisiweze kununuliwa, kwa sababu skuli tunajua ukiikodisha ardhi kwa ajili ya kujenga skuli hatimaye itatakiwa ilipiwe kodi pale ambapo panahitajika, lakini kama ni skuli ya *private* tu hakuna tatizo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe ufafanuzi katika ukodishwaji huu, hivi ardhi hasa inakodishwa kwa miaka mingapi na utaratibu gani, ili tuweze kupata uelewa zaidi.

Suala jengine ambalo nataka kulichangia ni kuhusu Shirika la Umeme. Kwanza hapa nataka nichukue fursa hii kuwapongeza wizara kwa hatua yao waliyofikia katika mpango mzima wa kuwapatia wananchi umeme kwa njia ya mkopo. Kwa kweli ni jambo zuri kwa sababu umeme hatutegemei kwa ajili kuonea tu, isipokuwa umeme una matumizi mengine na matumzi makubwa ni kwa ajili ya uzalishaji, ili watu wapate mahitaji na matumizi yao; umeme unachangia kwa kiasi kikubwa kwa wananchi katika kutekeleza shughuli zao za kila siku.

Mhe. Naibu Spika, nimesikia juzi katika Wilaya yangu ya Micheweni kuna wananchi wengi wamepatiwa umeme kwa njia ya mkopo. Kwa hivyo, sina budi nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kufanya mpango huo, nadhani kwa kiasi fulani utasaidia watu wengi ambao wanaohitaji kuungiwa umeme kupitia njia hiyo.

Vile vile katika shirika hili, tunajua serikali inafanya juhudi kubwa na Shirika la Umeme katika kutusambazia umeme maeneo mbali mbali, mijini na vijijini. Hivi sasa kuna vijiji vichache sana ambavyo kwa Zanzibar vinakosa umeme.

Hata hivyo, Mhe. Naibu Spika namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze sijui mpango wao, kwa sababu kuna maeneo mengine ni muhimu sana kupata huduma hii ya umeme, lakini unaona *line* kubwa za umeme zinapita, cha kusukitisha maeneo haya huwa mengine hayafikiwi.

Kwa mfano, kuna maeneo ya Skuli ya Tumbe; wanakilio kikubwa cha kukosa umeme pale, karibu Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge wameshawaita pale kwa kutaka kusogezewa ile huduma ya umeme, ukiangalia skuli ile ina wanafunzi mpaka *Form IV*. Sasa skuli kama hiyo kukosa huduma ya umeme ambayo ni muhimu ni tatizo kubwa na inapelekea watu kukosa kufanya shughuli mbali mbali za kimasomo pale. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aje anieleze, hivi serikali katika maeneo haya ya skuli kama hizo zinazokosa huduma za umeme, wanao mpango gani wa kusaidia. Pia kama upo uwezekano ni vyema akatufanyia maarifa, ili kujua ni gharama ya kiasi gani watatusaidia shirika kusogeza umeme katika Skuli ya Tumbe. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala zima la ardhi. Mhe. Naibu Spika, katika eneo la Tumbe pale kuna viwanja vingi vya serikali, ambavyo viwanja hivi tayari vimeshavamiwa kwa kiasi fulani, lakini tulifika pahala tukasikia kwamba serikali kupitia Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wanao mpango kuhusu vile viwanja kuvikata vya *plan*, kwa ajili ya kuwauzia wananchi katika masuala mazima ya ujenzi.

Suala hili nasikia tetesi tu kwamba tayari kuna maeneo yameshaanza kukatwa viwanja na watu wameshaanza kwenda kuandikisha kupitia masheha wao. Kwa hivyo, ninataka uhakika wa hili suala na kama ni kweli utaratibu gani unaotumika katika kukata viwanja hivi na kuwapa wananchi na kiasi gani cha fedha ambacho anahitakija mwananchi kutoa, kwa ajili ya kupatiwa kiwanja kile.

Sasa nije katika suala zima la maji. Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni nilikwenda kutembea katika kijiji kimoja cha Kilindi hapa maeneo ya Unguja. Katika kutembea kwangu nimewakuta wananchi wa sehemu ile wanalalamika kutokana na ukosefu wa kupata maji safi na salama. Kwa bahati nzuri katika eneo lile nilisikia kwamba kuna visima ambavyo tayari vimechimbwa na tenki la maji lipo, lakini bado visima vile havitumiki katika kijiji kile.

Kutokana na hali hii, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, aje anieleze hivi ni kwa sababu gani ambazo zinazopelekea ukosefu wa maji katika kijiji cha Kilindi wakati visima vipo. Umetumia ardhi yao kwa ajili ya kuchimba visima, lakini maji yale yasianze kutumika pale na yaende yakatumike vijiji vyengine. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anipe ufafanuzi wa suala hili.

Mhe. Naibu Spika, ardhi tunaambiwa ni mali ya serikali na pale serikali itataka kutumia ardhi ile kwa shughuli za maendeleo, serikali inaweza kuchukua ardhi ile kwa ajili ya kutumia kwa shughuli za maendeleo. Vile vile tunajua kwamba serikali yetu inao mpango wa kutugaia viwanja kama vile Waheshimiwa pamoja na watu wengine, yaani serikali inao mpango huu wa kugawa ardhi kwa wananchi wake kwa kufuatana na masharti na matakwa wanayojiwekea.

Hata hivyo, ni masikitiko makubwa, kwa sababu ardhi yetu Zanzibar ni ndogo na ardhi tunatumia kwa ajili ya kilimo. Asilimia kubwa ya watu tulioko vijijini kazi zetu ni kulima, kuvua pamoja na shughuli nyengine ndogo ndogo. Kwa mfano, Mhe. Naibu Spika ile Micheweni yenyewe ukiangalia ile hali ilioko katika kile kijiji cha Micheweni na ardhi yao waliyonayo pamoja na unyonge wao walionao na wao ndio sana wanatumia ardhi kwa ajili ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, masikitiko yangu na niliwahi kuchangia wakati wa ripoti za kamati hapa kwamba kuna eneo la Mziwanda, ambapo kuwa eneo lile lilitolewa kihalali tu na akapewa mtu kwa ajili ya kufanya shughuli maalum ambayo ilitarajiwa ifanyike na kabla ya kupewa huyo mtu walikuwepo watu au wakulima karibu 80 na zaidi na kupewa huyo mtu, lengo na madhumuni ni kuwa anakuja kufuga mbuzi.

Sasa kwanza tuliangalie hilo la kuja kufuga mbuzi; mtu kutoka Unguja akasema anakwenda kufuga mbuzi Micheweni na wale wafugaji ambao wapo pale Micheweni kama wanayo mifugo yao, wao kwanza waende wakauze wapi mbuzi wao na kama suala hilo litafanikishwa, ina maana huku ni kuwaonea. Sidhani kama ni eneo la ufugaji mbuzi, kwa sababu tunapita wakati wote lakini bado sijaona eneo lile kama linatumika kwa ajili ya kufugia mbuzi.

Kwa hivyo, najua kwamba yule aliyepewa alipewa kisheria, lakini kisheria mtu apewe ardhi kwa madhumuni maalum. Kwa mfano, anapewa ardhi kwa ajili ya kujenga nyumba ya kukaa au kwa ajili ya uwekezaji ama atafanya kitu na ile jamii iliopo pale nayo ifaidike. Kwa kweli kumpa mtu ardhi na hatimaye ardhi ile ikadhibitiwa na kutiwa uzio pamoja na kila kitu wananchi wakaondolewa pale wasiendelee na shughuli zao za kilimo, halafu wakatafutwa watu wengine na kuekwa pale, si jambo la busara. Hivyo, kinachoendelea pale juzi ninapita nakuta kuna mahindi ndio yanayolimwa.

Mhe. Naibu Spika, hatuoni kuwa hatuwatendei haki wananchi ambao wapo maeneo yale na siku zote tunasema kwamba miongoni mwa watu wanaongoza kwa umasikini ni wilaya ile. Sasa leo iweje, itakuwa ndio hao wanaonewa na serikali kuchukuliwa maeneo yale ya shughuli zao za kila siku na halafu akenda akapewa mtu mwengine. Kwa hiyo, bado ile azma ya ufugaji wa mbuzi sijaiona mantiki yake.

Mhe. Waziri aje anieleze hiyo ndiyo mikataba iliyofungwa katika eneo lile, wakulima wakanyang'anywa wa kijiji kile akapewa huyo aliyepewa ndilo lengo lililokusudiwa, na kama ni hivyo sheria ya ardhi inasemaje. Kwa hivyo nitaomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa leo aje anipe maelezo ya kina kabisa kabisa, ili niweze kuridhika. Watu wanaoishi pengine ni walemavu na wanawake wajane wakenda wakanyang'anywa akaja kupewa mtu kwa ajili ya kuja kufuga mbuzi pale. Kwa hivyo mimi hotuba hii naiunga mkono lakini kama sikupata maelezo ya kina basi mkono wangu nauondoa.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mhe. Naibu Spika, niipongeze kamati pia kwa maoni yao ambayo yametusaidia kwa kiasia fulani kuona matatizo mbali mbali ya Wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa Idara ya Ardhi na Usajili; Idara hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli za ardhi Unguja na Pemba na mimi niseme Mhe. Naibu Spika, sitokuwa na mengi lakini niseme kwanza kama alivyosema Waziri alivyozishukuru kamati zako za Baraza kwa kutoa ushauri na kupokea ushauri, na mimi pia nachukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati yangu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii.

Pia kamati yangu teule ya Migogoro ya ardhi ningechukua fursa hii kumshukuru Waziri kwa kupokea ushauri mbali mbali, kwa kweli Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na mambo mengi katika sekta hii niseme ni changamoto na hasa hii ya ujenzi wa *jet* ni changamoto moja ambayo tulikuwa nayo, kwa maana hii kulikuwa na ukiukwaji wa sheria za uwekaji huu wa hizi *jet* na vile vile kukiukwa sheria za mazingira.

Ardhi ni rasilimali muhimu, ni lazima tuitumie vizuri ili iweze kutuletea faida kubwa sana na kukuza uchumi wa nchi yetu pale ambapo tutakuwa *serious* na uwajibikaji. Ni fedha nyingi sana ambazo tutazikosa katika *collection* ya mapato yetu tusipokuwa *serious*.

Mhe. Naibu Spika, sheria za ardhi ni nyingi sana lakini kama tatizo ni la utekelezaji ningeomba Wizara hii sheria hizi izitekeleze ipasavyo kama tunataka maendeleo ya sekta hii. Pia nimuombe Mhe. Waziri zile sheria zilizokuwa hazina kanuni basi zitungiwe kanuni kwani sheria bila ya kanuni ni sawa sawa na jembe lisilo mpini.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya umiliki wa ardhi utolewe kwani uelewa wa wananchi ni mdogo, wanaona ardhi kama ipo ipo tu na kila mtu anaweza kutumia anavyoweza. Migogoro mingi hutokea kutokana na kutokujua sheria. Hawajui kwamba ardhi ni mali ya Serikali. Mhe. Naibu Spika, tunapotaka ardhi lazima tupate umiliki wa ardhi yenyewe na tukitimiza wajibu wetu migogoro ya ardhi itaondoka na hata Mahakama ya Ardhi itakuwa haina kazi ya kufanya na tutaipunguzia mzigo Serikali.

Nikichambua ardhi tutafika kesho, kumbe ardhi inasajiliwa mimi mwenyewe nimesahau na najua kuna wenzangu watakuwa vile vile niwaambie tu wananchi kwamba vile vikataa vyetu basi vinahitaji kusajiliwa.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Idara ya Mipango Miji na Vijiji; niseme kwamba idara hii ina majukumu makubwa, lakini mimi nashangaa nikienda kwenye miji ya wenzetu kwa kweli nashangaa, sasa hivi mji wetu

umekuwa sijui namna gani, maana yake nyumba barabara hii hapa. Kwa kweli mji wetu hauvutii hata kidogo kusema kweli, tofauti na miji ya wenzetu. Karibuni hivi tulikwenda Zambia unatembea huoni nyumba ziko karibu na barabara, kwa kweli tunakwenda *airport,* ipo mbali sana huoni kwamba kuna mchanganyiko wa majumba, lakini leo ukija kwenye *airport* yetu hapa kwa kweli unatoka majumba unaingia *airport*.

Niseme mipango miji na vijiji ina jukumu la kupanga mji huu, ukweli mji wetu hauopo ki-*standard* na unapokwenda kwa wenzio ukija hapa unaona kama umeingia katika kisima. Tuna jukumu la kuupanga huu mji ingawa kwa muda huu tumeshakosea, kwa sababu si rahisi tena kusema kwamba unaupanga tena mji huu.

Mhe. Naibu Spika, niseme Idara hii imenidanganya; niliomba kiwanja ingawaje sikuomba moja kwa moja lakini kulikuwa na kiwanja hapa baadae nilikifuatilia kwamba hicho kiwanja baada ya kuona mambo ya kijamii (kujenga kituo cha Polisi) nikasema kwamba tunakitumia na baadae tutapeleka maombi, baada ya kuona hali hatarishi ambayo ilikuwepo ya kunyanyaswa vijana wetu ambao wako karibu na maeneo yale ya hatarishi, ili tuwakinge na matatizo yale. Lakini Idara ya Mipango Miji ilinambia kwamba pale pahala panataka kupita njia. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja hapa unambie hii njia ni lini hasa itajengwa maana yake nimeambiwa huu mpango tokea mwaka 2003 mpaka leo mwaka 2014 bado haijapita, kwa kweli huu ni udanganyifu.

Watu wanaingia na marungu saa nyengine wanawanyang'anya watoto halafu wanawake walikuwa wananyanyaswa sana maeneo yale pale. Ingawaje kulikuwa na matatizo mawili pale yalijitokeza kwanza ilikuwa kupita *cable* ya umeme na niwashukuru sana shirika la umeme, kwamba wao walikuwa hawana *objection* yoyote walinambia kama utagharamika wewe mwenyewe ya kuhamisha tu *cable* kupeleka mbele, basi wao walikuwa tayari watu wa Shirika la umeme, lakini Idara ya Mipango Miji ilikataa.

Mhe.Naibu Spika, kwa kweli ardhi ni kitu muhimu na ardhi kama nilivyosema inachangia sana katika pato letu la taifa, lakini wananchi wengi hawajui na wanaona ipo ipo tu ardhi, na kwa hivyo ni lazima sasa tuwe na msimamo na uwajibikaji, ili tuweze kufanikiwa.

Kama nilivyosema mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya PAC, huu ujenzi wa *jet* kwa kuwa ardhi ni pamoja na bahari, wenzetu hawa wawekezaji kwa kweli wanaitumia hii ardhi kinyume cha Sheria. Kwa hivyo ni lazima Sheria zipate utaratibu kwani ni pesa nyingi kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, tunazikosa kupitia sekta hii ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye kitabu hiki ukurasa wa sabini; kwanza nimeona mapungufu kwenye *vote book* hii kwenye fungu 0401 Mipango na Sera kifungu 211104 Malipo ya Likizo kwa mwaka, samahani nimechanganya Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, nasema kwanza lazima tuzingatie kuna mambo tuyazingatie, tumesema kwamba tupunguze safari za nje, lakini tusikatae zile safari ambazo zitakuwa na faida na mimi najenga hofu kuona kwenye fungu la 0301 Afisi Kuu Pemba, kifungu 220300 Gharama za Safari nimeona kwamba kuna safari za ndani zina 25,670,000/= lakini safari za nje ina nyingi. Kwa kweli naomba Mhe. Waziri anipe maelezo kwa fungu hili la *domestic* na *foreign* kwa nini fedha hizi hapa, kwa nini safari za nje, suala langu ni safari za nje. Tunaweza tukafanya safari za ndani, lakini zikawa kidogo afadhali. Lakini tukatumia safari moja ya nje ikawa imelega faida zaidi, waswahili wanasema usipoziba ufa utajenga ukuta. Nimeona kwamba kuna vifungu vinakuwa havitumii pesa na kwa sababu ya sisi wawakilishi tunashindikiza sana hapa, lakini mimi vile vile naona kwa upande mwengine itakuwa ni vigumu, kwa hivyo tutunze kidumu.

Kuna vifungu kama hujavitilia pesa basi inakuwa ni tatizo kwa sababu kuna mambo yanakuwa endelevu kama umeshajenga nyumba yako basi Mhe. Naibu Spika, itakuwa kila wakati unaishughulikia pengine rangi, labda kitu changine, sasa unakuta kifungu kwa kweli hakina pesa kabisa na kinakuwa pengine kwa muda mrefu; miaka mitatu kifungu kile kinakuwa hakitiwi pesa na hivi ndivyo tunavyofeli saa nyengine.

Tunafeli kutokana na mali za Serikali zinapotea kutokana na ugumu wa uchache wa fedha ile ya kufanyia matengenezo madogo madogo, na kwa sababu sasa hivi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana *VFM* (*Value For Money Auditing)* kwa hivyo hata ile thamani ya kile kitu chenyewe pia anakitizama. Kama hatutovipitia na kuvitengeneza zikwa endelevu maana yake kwa kweli tutakuja kugharamika sana.

Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kweli tunaisimamia Serikali lakini kuna vitu vitakuja kutu-*cost* sana, ni lazima tuvitizame na vitu vyenyewe, si vuziri kifungu kinakuwa hakina pesa hata kidogo inapotokea dharura hakuna la kufanya, hili lazima wajumbe wenzangu tulione.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa namba 70 unasema Idara ya Ujenzi; hii Idara ni muhimu vile vile kuna Idara ya Nyumba na maendeleo ya Makaazi kwa kweli hii Idara pia ni muhimu lakini ndio yale yale niliyosema kwamba hizi nyumba zinahitaji matengenezo. Nimetembea kwenye nyumba nyingi tunapokwenda na kamati, kwa kweli nyumba zimechoka, nafikiri kuna kodi ya nyumba Mhe. Waziri naomba anielezee. Kwa sababu kuna mambo mengine ya kutegemea kwamba fedha iende serikalini halafu itoke inakuwa ni ngumu. Nafikiri tungekuwa na *account* ambayo fedha hizi zinakaa zinatiwa pale na baadae zinatumika hizi hizi kwa matengenezo ya nyumba. Kwa sababu tunajua serikali yetu kwamba ina mambo mengi. Sasa kuna baadhi ya mambo niliwahi kumwambia Mhe. Waziri wa Fedha kuhusu mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Sasa kama Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ina jukumu la kuvisimamia viwanja vya ndege na kuwa vya kileo, ni lazima wawe wanashughulikia na pale hata ile *x-ray machine* ilikuwa haifanyi kazi; mbovu.

Kwa hivyo vitu kama vile kwa kweli vinazorotesha hata ule utendaji, kwa hivyo ningeomba labda Mhe. Waziri ukapata *authority* ya hizi pesa zina *account* maalumu ambayo itakuwa munaishughulikia kama Wizara kwa uadilifu ili ziwe zinasaidia katika kuzifanyia matengenezo hizi nyumba.

Vile vile kuna Mamlaka ya Uhifadhi wa Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Mimi niwapongeze sana hii Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe. Kwa kweli kama tunavyojua kwamba hii ni hifadhi ya Kimataifa ni lazima vile ulivyo usibadilike na ujenzi wake vile vile usibadilike. Na ni mwiko kujenga mji ule kwa matufali, na majengo sasa hivi yameshakuwa mabovu mengine yanaporomoka. Yale yaliyokuwa mabovu ninafikiri ni busara yangeangushwa kabisa, halafu tukatizama namna gani tutafanya kama kuyajenga tena kidogo kidogo, ili tusipoteze ile haiba ya Mji Mkongwe.

Mamlaka ya Maji ni Mamlaka iliyokuwa na kazi kubwa vile vile, na kwa sababu maji ni uhai ni lazima binaadamu apate maji. Wanao mkakati ambao sasa hivi na ni lazima niwaombe wananchi kwamba sekta hii ni lazima sasa hivi tuichangie kwa sababu kama kitu kiwe endelevu ni lazima tukichangie kwa kiasi fulani wala tusione tabu.

Kama tunavyojua kwamba serikali ina majukumu mengi ya kimsingi, lakini hii ningewaomba wananchi tukaichangia kwa sote ili huduma ziendelezwe. Kwa sababu kama tutakuwa hatuichangii na niseme kwamba hakuna nchi hata moja ulimwenguni ambayo unaikuta kwamba wananchi wake hawachangii huduma hiyo. Na kama tunataka iwe endelevu basi ni lazima tuichagie.

Vile vile, niwaombe Mamlaka ya Maji, lazima ile miundombinu iboreshwe kwa sababu sasa hivi miundombinu hii itakuwa ni chakavu na mengine kutokana na ile ile kwamba hatukujenga mji wetu vizuri unakuta miundombinu ile saa nyengine imeingia ndani ya ukuta wa mtu au imo ndani ya chumba cha mtu, kwa kweli athari hizi za kujenga ovyo ovyo. Kwa hivyo ni lazima kwanza kama wanataka mafanikio kwenye hii miradi yetu inayokuja kama misaada na mambo mengne basi tuboreshe miundombinu au ijengwe miundombinu mipya kabisa, ili sasa iweze kufanikiwa Mamlaka ya Maji watu kupata maji na kuchangia, lakini ni usumbufu ambao unajitokeza watu wengi wanalalamika kwamba maji wanakuwa hawapati lakini wanakatwa, lakini sifikirii kwamba inakuwa ni hivyo; ni maneno, kwamba wewe hupati maji halafu kwa nini unalalamika. Ningeiomba Mamlaka ya Maji badala ya kuchimba visima, kwanza wakashughulikia hii miundombinu ya maji.

Shirika la Umeme niwashukuru sana na wao kwa kazi nzito ambazo wanazifanya lakini kama Shirika linaenda kibiashara na wao watumie uadilifu sana. Muda mrefu nimekuwa nao nilipokuwa kwenye Kamati ya *PAC* tunapita halafu ile Kamati Teule ambayo tulipewa na Mhe. Spika, tumefanya kazi, najua zipo changamoto nyingi, lakini kwa kweli Shirika la Umeme linafanya kazi kubwa, wajitahidi kulifanya kwamba Shirika hilo liwe la kibiashara. Tunajua

kwamba tunadaiwa pesa nyingi, na jana baada ya kusema tu Mwenyekiti wangu hapa aliposema kwamba tunadaiwa deni kubwa nikaja nikaona umeme umekatika mji mzima, nikaona ehee sijui wamesikia, lakini kwa bahati umeme umerudi na nishukuru kwa kurudi tena umeme huo, lakini na wao vile vile wajitahidi kuliendeleza Shirika hili kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba baada ya hayo naunga mkono hoja.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Naibu Spika, na mimi ninashukuru asubuhi hii kupata fursa ya kuchangia Wizara ambayo kwa maoni yangu ni moja kati ya Wizara muhimu sana.

Kwa ujumla nisingependa kusema mengi kwani Mhe. Naibu Spika,Wizara hii katika bahati ilizozipata ni kuwa imepata kuundiwa Kamati mbili na Baraza lako Tukufu; Kamati Teule. Baada ya kuona Wizara hii ina changamoto nyingi Baraza lako liliamua kuunda kamati. Na nina imani kwamba yale yaliyoelezwa katika kamati hizo yangetosha kumfanya Waziri kwa muda huu uliobakia labda mwaka mmoja na miezi mitano au minne asikae kitako ayafanyie kazi.

Sasa ninahisi kwamba kuzungumza mengi na niliyojifunza katika kuundwa kwa kamati zile Mhe. Naibu Spika, ni ku-*create enmity* baina ya watendaji na sisi Waheshimiwa. Kesho ninatarajia nina nyumba yangu nataka niungiwe umeme, sasa nikizungumza mengi na tayari kamati ile ilishatoa maoni yake itakuwa kama kurejea yale kwa yale.

Mimi ningemuomba tu Mhe. Waziri ya kufanyia kazi anayo, kwa hivyo angeyafanyia kazi kwa maendeleo ya nchi hii na kwa maendeleo ya Wizara hii na kwa haiba ya jina lake, kila mmoja anamtaja kwa wema. Kwa hivyo utendaji wake pia utamfanya ajiongezee *merit.*

Mhe. Naibu Spika, lakini juu ya hayo itabidi japo kidogo tuchochee chochee, ninajua moto unawaka lakini kuni zikipungua pungua itabidi tuongeze ongeze kuni ili moto uwake haraka haraka na chungu kikolee mapema. Walaji ni wengi na walio na njaa ni wengi wanasubiri wapate kula kwa mapema zaidi.

Mimi kidogo nianzie Mhe. Spika, na Shirika la Umeme. Ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwamba mwaka jana alisema yeye hataki kusema maneno yaliyokuwa hayatekelezeki. Na katika hilo baada ya kumuuliza ni vipi atakisaidia kijiji cha Makoongwe aliniambia nisubiri bajeti hii. Kwa ujumla nimeiona bajeti Kuu ya Serikali na ninashukuru kwamba imetenga fedha kwa ajili ya kupeleka umeme katika Kisiwa cha Makoongwe. Kwanza ninampongeza kwa hilo kwamba zile fedha zipo au zimetengwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini naomba nimkumbushe tu Mhe. Waziri kwamba ule ni mpango lakini utekelezaji bado, na ninayo kumbukumbu kwamba katika utekelezaji wetu kunakuwa sio salama. Mwaka 2011/2012 tuliletewa hapa programu ya ununuzi wa meli kwa ajili ya uvuvi wa Bahari Kuu na mafunzo ya wavuvi. 2013 ukaja tena, 2013/2014 Kamati yangu ilikaa na Wizara ya Fedha na ikaomba rasmi kwamba fedha za *MDRI* za msamaha zipelekwe katika ununuzi wa Boti, lakini la kushangaza Mheshimiwa kwamba mwaka 2014/2015 mpango ule haupo tena.

Sasa ninamuomba Mhe. Waziri hilo alijue, asimamie na hawa wananchi kama walivyokwishatia tamaa katika kisiwa kile baada ya kusikia bajeti kuu ya serikali kwamba umeme wataupata basi asimamie wale wananchi waupate, kwa sababu wao ni watu wa kisiwa wanasumbuka sana. Kuna hospitali, kuna baadhi ya madawa yanahitajika yahifadhiwe kule na umeme haupo. Kama vile alivyoahidi kwa maneno sasa naomba aahidi haya kwa vitendo. Kwa sababu harakati nimeshaziona, lakini sijui harakati hizi zinatarajiwa rasmi zianze lini na labda zimalizikie lini.

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Umeme kama nilivyosema mwanzo kwamba liliundiwa Kamati Teule na mengi yameshasemwa, mimi kidogo nataka nikumbushe kwa sababu nahisi *potential* ipo katika Shirika la Umeme, lakini utendaji wao sijui ukoje.

Nilipokuwa nachangia Wizara ya Mhe. Haji Omar Kheri nilimuuliza je yule Mkurugenzi wa Baraza la Mji yeye naye amepatiwa ile fursa ya watendaji wakuu wa Serikali kwenda kujifunza nchini China. Jawabu sikuipata vizuri, lakini ninamuomba Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla kama itatokea nafasi ya hawa watendaji wetu wa Shirika la Umeme na wao basi wapatiwe fursa waende wakajifunze japo sio China, lakini waende sehemu mbali mbali ulimwenguni.

Ninajua Mhe. Waziri anajua kwamba *principle* moja ya kujifunza ni kuiga, tuna *learn through imitation.* Sasa na wao watakapokwenda kule watapata kuiga wenzetu wanafanya nini. Shirika ni la Biashara ninavyofahamu mimi, sasa biashara hutakiwi kwenda dukani ukamwambia nataka mafuta ya taa umeme umezima atakwambia hamuna. Unatakiwa unapokwenda pale ukamwambia nataka mafuta ya taa umeme umezima kibatari changu nipate kuona kidogo yawepo.

Hivi sasa lakini Mhe. Naibu Spika, unapokwenda katika Shirika wanajitahidi sana, lakini bado unatumia muda mrefu mwananchi kupata umeme na yanayohitajika yapo, sasa tatizo linakuwa nini hata mtu ajaze fomu mpaka fomu ipotee pale leo hajapata umeme maskini.

Kwa hivyo ninawaomba hawa watendaji unajua moja katika pia msingi wa kusoma ni kuwa-*readiness, readiness in learning,* huwezi kusoma kama hujajiandaa kuwa tayari. Sasa na wao wawepo tayari katika mabadiliko. Kama tulikuwa tunatumia sera za huko nyuma hivi sasa sera zile tuzibadilishe twende na wakati, tuangalie mtu anatoka Nungwi anakuja Shirika la Umeme mara kumi, mara kumi na tano, mara kumi na sita, kwa nini afanyiwe hivyo, kwa nini iweko hivyo? Kama ni wafanyakazi tunao vijana wetu waliopitia Mbweni tunaweza tukawaajiri katika utaratibu maalum, *temporary employment* wakatufanyia zile kazi, lakini tuhakikishe kwamba wanaohitaji huduma hii wanaipata kwa muda mfupi, sio tena kuhangaika mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, pia hivi sasa kuanzia Nungwi mpaka utafika Saateni kituo cha mauzo ya umeme kimoja, sijui hawajui kwamba maduka yakiwa mengi na ule upatikanaji wa ile huduma itakuwa sijui utakuwa mwingi. Leo tunataka kununua umeme na ukawa Bububu labda tunaokaa Kijichi na tunalazimika tuje huku. Sijui kuna utaratibu wowote hivi sasa wa kuona kwamba ipo haja ya hizi huduma za umeme kupatikana kwa njia nyengine.

Mhe. Naibu Spika, nilikwambia kwamba tuwapeleke wakajifunze. Wenzetu huko hivi sasa wananunua umeme kwa kutumia *mobile* zao. Sasa hata hili kubwa kuwa hatujafikia hatua hiyo ya kuwa sasa turahisishe upatikanaji wa umeme.

Mhe. Naibu Spika, jirani zetu hapo hivi sasa umeme unatumia njia tofauti, lakini leo kama hujaenda katika kituo cha umeme cha Shirika huwezi kupata umeme. Waandae utaratibu ninahisi na wao wataboresha mapato yao. Tunahitajika Mhe. Naibu Spika, Waziri hili Shirika ulifanyie *reforms,* si hivyo itakuwa hili deni linaongezeka kila siku na *potential* ipo ya kuzalisha na mapato yakaongezeka, lakini utendaji sijui kwa nini tunakwama? Mimi napenda uwape mafunzo wenzetu wakajifunze, waje waangalie jinsi gani wanaendesha mashirika kama haya. Hii ni *business,* kwa hivyo *business* hutakiwi kwenda dukani ukamkutia mtu muuza duka akakwambia nisubiri baba aje kaenda pale aje akujazie fomu hicho kitu unachokitaka. Mhe. Waziri ninafikiri umelifahamu.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokwambia sitaki niseme sana, lakini tunasema kwamba tunataka tuingie katika umeme mbadala na kwa kumbukumbu zangu mpango uliopita tulitajwa maeneo ambayo yameshafanyiwa utafiti; Matemwe, Nungwi na Micheweni, ambayo labda umeme wa upepo ingekuwa uwezekano wa kupatikana upo.

Mwaka huu sijaona ule utafiti umefikia wapi na serikalini tunakwenda kwa *program*, kwamba *program* hii tunaanzisha mwaka fulani tunaingizia kiasi fulani mwaka fulani tutakuwa tumefikia hatua fulani.

Hebu Waziri twambie hii *program* ya umeme mbadala inabakia katika vitabu tu hivi hivi au kuna *program* yake hasa iliyoandaliwa kwamba sisi *program* hii tunaianzisha mwaka fulani tunaanza wapi na tutaingiza kiasi fulani ili itakapofika mwaka fulani iwe *program* hii imesha-*mature* na wananchi wanaipata, lakini leo mimi nashangaa Mhe. Naibu Waziri kwamba katika kitabu tunaambiwa kwamba tunataka kuelimisha wananchi juu ya matumizi ya umeme mbadala wa nishati ya jua na upepo.

Hapa kuelimisha ina maana itahitajika fedha, mimi imani yangu Mhe. Naibu Spika, hapa hatuna haja ya elimu kama umeme upo mwananchi umeme wa upepo upo muungieni atumie, tunahitaji elimu ya nini, sasa haya maneno maneno ya kujaza vitabu Mhe. Waziri hebu yaondoshe siku nyengine, tuje tuwaambie tu umeme wa upepo tayari upo Nungwi, wananchi wa Nungwi mwaka fulani au keshokutwa watahitajika na umeme huu au *solar* ipo, wapi ipo Makunduchi, ipo pahali fulani wananchi watumie.

Hizi elimu ninafikiri Mhe. Naibu Spika, zitatupotezea fedha nyingi, watu wengine hula tu bila hata kunawa, hakuna ulazima wa kunawa, hizi elimu hazihitajiki tena hivi sasa kama huduma ipo mwananchi moja kwa moja anaihitaji, kwa hivyo tujiandae katika huduma isiwe ni maneno.

Matokeo yaliyotokea jana na siku nyengine na hivi sasa tunakaribia mwezi wa Ramadhani, na imekuwa kama kawaida yetu inapofika mwezi wa Ramadhani umeme kukatika katika, sijui mara hii kwa vile kuna hiyo *cable* mpya mambo yatakuwa vipi, lakini mwaka jana kuna Waheshimiwa wengine walikosa keki kwa sababu ma-*cooker* yao umeme ulikuwa ni mdogo. Kwa hiyo, Mhe. Waziri mara hii utuhakikishie hilo kwamba tutapata zile keki kwa wakati, kwa sababu umeme unakuwa wa kutosheleza.

Pia kwa hili ni utaratibu wa Wizara kwamba inapofika mwezi wa Ramadhani huwa wanawasaidia wananchi waliokuwa wana shida ya maji hasa katika maeneo ya Mjini ambapo hata utaratibu wa kuchimba kisima haupo. Basi mara hii wawafikishie huduma hii kwa wingi na mapema zaidi, sijui utaratibu wao mara hii ukoje.

Mhe. Naibu Spika, nagusia kidogo kwenye maji. Nashukuru tena kwamba hivi sasa vijiji vingi vinaendelea kupata miundombinu tayari imeshajengwa kwa ajili ya upatikanaji wa maji safi na salama. Na kuna kijiji kimoja ambacho hata ukichimba kisima cha kawaida basi maji inakuwa shida, lakini Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla iliiliona hilo na imeshaanza kupeleka miundombinu na kampuni iko na kijiji hiki ni cha Wambaa.

Mhe. Naibu Spika, lakini hivi karibuni nilipata malalamiko kwa wananchi kwamba walikwenda watendaji wa wizara na kwa ujumla ilikuwa mitaro imeshachimbwa ya kupelekea hiyo miundombinu, lakini wakaelezwa kwamba kuna utaratibu mwengine uliojitokeza na sehemu hizo hazitofikiwa tena na ile miundombinu.

Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri labda aje kunambia kuna utaratibu gani hapa ambao ulitokea, je huu mpango upo au umekufa njiani au labda ile *program* ilikuwa fedha kidogo na zitaongezwa fedha nyengine, ili wananchi wale ambao tamaa tayari wameshaijenga wapate huduma hii ambayo wameikosa kwa muda wote wa miaka 50.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana tulizungumzia kuhusu wafanyakazi ambao walipata ajali katika ujenzi wa mnara wa maji eneo la Machomane, karibu na Ofisi Kuu ya *ZAWA* Pemba. Sasa sijui kuna maneno kwamba wafanyakazi wale hadi leo sijui bima hakuna, fedha sijui zimepungua, sijui tuongeze nini. Hebu Mhe. Waziri tupe maelezo kidogo wale wafanyakazi ambao walibahatika hawakufariki je wao walishapata fidia yao au bado tunasubiri Mfuko Mkuu wa serikali utuingizie fedha na watu wale wapate haki yao.

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika hilo wametwambia kwamba *ZAWA* wamekusanya makadirio yao ni kupata karibu bilioni tatu lakini makusanyo yao yamekuja karibu bilioni mbili na hii ni asilimia kama 55. Moja katika sababu

wamesema sijui wananchi hawana uelewa, lakini kinachoelekea hapa yaani kuna wananchi ambao wanalipa na wananchi ambao hawalipi. Sasa nafikiri hiki si kizuri, kama ni kulipa basi wanaopata huduma ya maji sio walipe wakati hawapati, wanaopata huduma ya maji kama walipe basi walipe. Sasa je kuna sheria inayotulazimisha tufanye hivyo au tunakwenda kwa mazoea tu kwamba tunatakiwa tuchangie maji. Ikiwa hakuna sheria basi wakati ushafika tubadilike, tuweke sheria ya kumtaka mwananchi achangie, si hivyo basi mimi kwenda nikamwambia mwananchi unatakiwa ulipe wakati mmoja analipa na mwengine halipi hakufanywa kitu, aah Mhe. Waziri hilo sitolifanya.

Kuwe na sheria nijue nitapokwenda kumuelimisha mwananchi kwamba wewe unatakiwa ulipe na sheria inasema moja, mbili tatu hapo nitawaelimisha, lakini huyu halipi amefumbiwa jicho, yule analipa aendelee kulipa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache mimi naiunga mkono hotuba hii na namshukuru Mhe. Waziri.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika katika hali ya uzima na afya njema. Pia Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuchangia wizara hii ambayo imegusa jamii kwa jumla ni wizara nyeti, lakini nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao walimsaidia kwa namna moja au nyengine kufanikisha hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimpe pole kwa upande mwengine Mhe. Waziri kwa sababu hii wizara ni wizara mbayo kwa kweli ni ngumu sana. Ukiiangalia wizara hii toka huko inakotokea ina migogoro mbali mbali, hata awekwe waziri wa aina gani basi migogoro ile itakuja kumuangukia yeye. Nimpe pole lakini pia kwa imani yangu kubwa kwa waziri huyu ataweza kufanikisha mengi ambayo wananchi wanayahitaji.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niipongeze serikali kwa jumla kwa sababu Mheshimiwa tukitaka tusitake lazima tukumbuke tulikuwa na matatizo makubwa ya maji na hasa katika kisiwa chetu cha Pemba, lakini nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kutokana na Mradi wa *UNDP;* kwa kweli mradi huu umefanya kazi kubwa sana na unaendelea kufanya kazi. Kwa hivyo, niipongeze sana serikali jinsi mradi huu ulivyotumika.

Vile vile nipongeze kuna baadhi tu ya sehemu ambazo bado hayajamalizika mambo yake, lakini niseme tu maji yamefika Wambaa kwa mradi huu kujengwa matangi yale makubwa ambayo ni madhubuti ya kuweza kuwatosheleza wananchi wetu. Vikunguni, Gombani, Bahanasa na Wete Mjini.

Pia nichukue nafasi pekee ya kupongeza hapa Bahanasa, maana tunasema *sadaka huanza nyumbani*. Niishukuru sana lakini nitakuwa mwizi wa fadhila Mhe. Naibu Spika kama sikumshukuru aliyekuwa Afisa Mdhamini Pemba ambaye aliifanya kazi kubwa sana ndugu yangu huyu na mwanangu huyu, na mimi nilimbana kweli kweli maana alikuwa hanywi maji kuhakikisha kwamba ninapata maji Mtambwe.

Na aliifanya kazi tukashirikiana bega kwa bega, maana hayo maji mpaka kupatikana ilikuwa kazi kubwa sana, maana kulikuwa kuna bonde lakini alihakikisha pamoja na wanaohusika kwamba maji yale yanavutwa mpaka yanafika juu ili wananchi na wao waweze kupata maji. Kwa hivyo, nimpongeze, mtu akifanya vizuri mpe, kwa hiyo nimpongeze sana mtoto wangu huyu ambaye alisaidia sana kupata maji kwa Shehia ya Mtambwe.

Si Mtambwe tu ni sehemu nyingi maji haya yamefika kuanzia Daya, Bagamoyo mpaka Mkanjuni, si Mkanjuni ile ya Chakechake Mkanjuni ya Mtambwe, jina la Mkanjuni ya Chakechake jina hili linatokana na jina la Mtambwe, Mkanjuni wameiga kuchukua kwetu pale Mkanjuni. Kwa hivyo, ni Mkanjuni ya Mtambwe hii.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niseme kwamba nakumbuka Mhe. Waziri kama sikosei alituletea mswada hapa, mswada ambao ulikuja hapa wa kuanzisha Shirika la Nyumba kama sikosei, lakini kwa bahati mbaya mswada huu ukatiwa dosari za hapa na pale. Ni imani yangu kama umerudishwa nakuomba sana Mhe. Waziri kwa hali na mali murekebishe mule ambamo mnataka kurekebishwa ili tuwe na Shirika la Nyumba. Kwa nini nikasema hivyo?

Mhe. Naibu Spika, wizara hii kama nilivyosema mwanzo ni wizara ngumu sana, tuna nyumba ambazo zinawahusu wizara hii, na nyumba hizo kwa kweli nyingi zimeathirika hata nyengine haifai hata kuzitizama. Kwa hiyo, tutapokuwa na shirika hili la nyumba itakuwa ni rahisi kuweza kuzihudumia hizi nyumba.

Namuomba sana Mhe. Waziri kama mswada huu umeshakuwa tayari basi tunapokuja tukirudi tena kwenye Baraza hili nitamuomba sana Mhe. Waziri atuletee mswada huu ili tuweze kuupitisha na uanze kufanya kazi yake vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije na mimi nichangie kuhusu habari ya umeme. Mimi silaumu kwamba umeme unazimwa, jamani sisi binadamu na vyombo hivi tunavyovitumia navyo vina mambo mengi, vimekaa kama sisi binadamu. Mimi naweza nikatoka hapa nikaja hapa na mitandio yangu nikitoka hapo nje nikaanguka, Mwenyezi Mungu anihifadhi. Ni kwa sababu na vyombo vyetu hivi navyo vinafanya kazi kama binadamu, sasa kinapoharibika chombo tusilaumu hatujui kumetokea kitu gani Mhe. Naibu Spika. Mimi niombe tu ili kutokana na matatizo ya hapa na pale, basi nimuombe Mhe. Waziri atuletee umeme mbadala ili wananchi wetu waweze kulipa hisa ya umeme na bei kuwa nafuu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuna wananchi wetu uwezo wa umeme huu tunaoutumia ni ghali wengine hawana uwezo na wao wana haki ya kupata umeme katika majumba yao. Kwa hiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri pamoja na mambo yake yote na kusafiri kwake atutafutie umeme mbadala ili wananchi wetu waweze kumudu na wao kutia umeme katika majumba yao.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije kwenye suala la *plan* katika mji, miji na vijiji. Mhe. Naibu Spika, tatizo linalojitokeza katika mambo haya ni kwamba hatuwezi tukahangaikia mambo yetu ipasavyo. Kwa nini? Mjini hapa pana *plan* yake mimi niseme hili jiji letu la hapa Zanzibar lenye Manispaa kwamba kuna *plan* yake kwa nini hii *plan* hatuiweki vizuri.

Mimi namuomba Mhe. Waziri kwa sababu *mtaka uzuri sharti azurike*, haidhuru tupange *plan* yetu ya mji tutapata hasara lakini mji wetu utakaa vizuri na utavutia. Leo ukija hapa majumba mengine yameelekea Kusini aliyejenga mwengine ameelekea Kaskazi, karo zinampita yule aliyeelekea Kusini hazina mpango tunarudi karne ya nyuma sio karne ya 21 Mhe. Naibu Spika. Hata ile gari ya ng'ombe saa nyengine haiwezi ikapita, mgonjwa achukuliwe kwa gunia si karne ya nyuma hiyo Mheshimiwa. Kwa hiyo, ningelimuomba sana Mhe. Waziri *plan* ya mji huu iharakishwe na itekelezwe.

Mhe. Naibu Spika, hata huko vijijini hatujengi kwa *plan* sasa hivi mambo yamebadilika Mhe. Naibu Spika, tuko katika sayansi na teknolojia. Hata huko vijijini tuwaelekeze wananchi wetu namna gani ya ujenzi wa nyumba kama alivyosema Mhe. Fatma hapa kwamba ukienda kwa wenzetu unakuta nyumba zimezungukwa na barabara. Nyuma kuna barabara na mbele kuna barabara hukuti nyumba kwamba imezungukwa na mambo mengine ya aina yoyote, kwenye nyumba ni nyumba na kwenye mambo ya starehe ni starehe na *Airport* siku zote inakaa *far away from town* Mhe. Naibu Spika, kwa sababu uso wa *Airport* ndio uso wa nchi.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kwa heshima zote na taadhima wakae na watafakari na wahakikishe kwanza mji una *plan* yake, na kama kuna pahala panataka kuvunjwa nimeshasema mwanzo *mtaka uzuri huzurika*.

Pia hata huku vijijini leo Mhe. Naibu Spika ukiangalia ramani ya vijiji nayo sasa hivi imeshaanza kuharibika kwa sababu gani? Kwa sababu mwahala mwa kulima mnajenga nyumba, mule mwahala mwa kujengwa nyumba ukiomba viwanja havipatikani.

Namuomba Mhe. Waziri akae na watu wake, kwa sababu ana wataalamu wenye ujuzi apime upya mji wote na vijijini, nakusudia kwa Unguja na nakusudia kwa Pemba aorodheshe na ahakikishe hapa ndio pa kujenga, hapa ndio pa kulima. Atakayeingia sehemu ya ukulima akajenga huyo asisamehewe, lakini sasa hivi tusiwalaumu wananchi wetu Mhe. Naibu Spika kwa sababu hawajui wanavamia tu.

Kama juzi hapa Mhe. Ali Salum Haji alisema mabonde sasa yanavamiwa watu wanajenga. Kwa hiyo, ninamuomba Mhe. Waziri kwa heshima zote akae na atafakari kwa kipindi hiki tukishamaliza bajeti aangalie na wa-*survey* Unguja yote na Pemba yote ili agawe sehemu zake za ukulima mbali na sehemu za majenzi ya nyumba mbali.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, wenzangu mengi wameyazungumza na mimi niunge mkono hoja mia juu ya mia, na niwaombe Waheshimiwa wenzangu kwamba hii ni wizara ambayo imemgusa kila mtu, kwa hivyo tukosoe pale pa kukosoa, lakini pia tuipitishe ili wananchi wetu waweze kupata mahitaji yao. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi naomba kwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa hapa wazima. Pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Awali ya yote naomba sana nimpongeze Mhe. Waziri na nimpe pole kwa kazi nzito. Maana katika wizara zote zilizoko chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wizara nzito ni hii. Maana ni Wizara ya Ardhi, Makaazi ya watu, Maji na Nishati, hata hicho chakula tunachokula kinatokana na ardhi hiyo hiyo. Kwa hiyo, maji, chakula yote yamo chini ya wizara hii kupitia ardhi.

Kwa hiyo, naomba nimpe pongezi sana Mhe. Waziri maana amefanya mengi mpaka sasa hivi, ameyakuta mengi na anaendelea kuyatatua mengi akisaidiwa na Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao nawaona hapa leo wapo wakiongozwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo Alhaj Ali Khalil Mirza.

Naomba sana pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kumudu, maana miongoni mwa wizara zote wizara yenye na Mamlaka mbili ni hii, wizara yenye idara nane ni hii, wizara yenye shirika ndani yake ni hii, wizara ambayo ina Mahkama yake ni hii, wizara ambayo ina Afisi ya Mrajis ni hii, wizara yenye bodi nne ndani yake ni hii. Kwa kweli huu muundo tu wa wizara yenyewe unaonekana ukubwa wake na mambo ni mengi.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu utaelekea zaidi kwenye kupata ufafanuzi wa hapa na pale, pamoja na kutoa maombi kwenye maeneo ambayo mimi nahisi yanaweza kutekelezwa vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwetu sisi hapa Zanzibar tuna tatizo moja kubwa sana na tatizo hili linahusu zaidi Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Mipango Miji na Vijiji, Idara ya Upimaji na Ramani na Idara ya Ujenzi yenyewe; nayo ni katika sehemu ya ku-*plan* huu mji wetu.

Hivi sasa utakuta maeneo mengi ambayo hayatakiwi kujengwa yanajengwa nyumba na hususan maeneo ya kuzalisha vyakula. Sasa hivi ukipita kule maeneo ya Mwera hata ukiingia ndani kule kwenye minara ya simu utakuta ujenzi unaendelea, na hii inatokana na kwamba wale wananchi wanakuwa na maombi mengi ya nyumba au viwanja vya kujenga na maombi yao wanasubiri kwa muda mrefu mpaka wananchi sasa wanajiamulia kuingia kwenye maeneo mbali mbali. Sasa hapa kuna tatizo moja, sitaki kuwalaumu wizara moja kwa moja lakini kwa upande mmoja na wizara nayo inahusika.

La kwanza kabisa wizara inaonesha dhahiri kwamba wanaomba pesa humu ndani kwenye kitabu cha bajeti lakini wanapata *average* kwenye wastani wa asilimia 60, na hiyo asilimia 60 yenyewe wanakuwa kwenye *ceiling* ambayo wamewekewa hawapewi kile wanachokitaka.

Masuala ya ardhi haya idara hizi nne nilizozitaja kwa kweli zinahitaji fedha nyingi kuendesha mambo yake, naomba niwapongeze sana wakuu wa hizi idara nne; Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Mipango Miji na Vijiji namuona dokta yupo pale, Idara ya Upimaji na Ramani na Idara ya Ujenzi. Kwa nini? Kwa sababu wao wanafanya kazi katika *resource* ndogo sana hususan *resource* za kifedha na vifaa vyengine mbali mbali.

Sasa Mhe. Waziri namuomba atakapokuja hapa atueleze, maana wanajua mipango miji imeshapanga mambo mengi sana, ramani ziko nyingi sana na mambo mengi ambayo yameshafanyika ila utekelezaji ndio bado unashindikana, na huu ndio unaosababisha leo ukipanda ndege na kuzunguka katika mji wetu unaona ule ujenzi unavyofanyika sehemu mbali mbali hususan kwenye *green belt* ya Zanzibar maeneo ambayo yanatarajiwa kuzalisha chakula.

Mhe. Waziri katika ripoti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili ambayo ilifanyika *survey* inasema baada ya miaka 20 mpaka 30 hapa Zanzibar kutakuwa na uhaba mkubwa sana wa chakula, yaani ardhi ya kuzalisha chakula itakuwa ndogo sana na ardhi iliyojengwa majengo mbali mbali itakuwa ni kubwa. Hii inaonekana hata sasa hivi, popote utakapokwenda kwenye mashamba makubwa utaona watu wameshaanza kujenga katika maeneo hayo. Kwa nini haya yanatokea?

Mhe. Naibu Spika, haya yanatokea kwa sababu sisi tuna *plan* lakini hatuzitekelezi. Nitatoa mifano ya visiwa vichache ambavyo vimefanana na Zanzibar na vipi ujenzi wao unakwenda, vimefanana na Zanzibar kwa upande wa *size* ya kisiwa na vimefanana na Zanzibar kwa sababu vyote vimezungukwa na bahari. Leo ukienda kwenye Kisiwa cha Hong Kong wao wameweka sheria ujenzi wao sasa unakwenda juu, kwa hiyo hata serikali ikikupa kiwanja haikupi tena kiwanja kama vile Tunguu unapewa kwenye mawe aa, unapewa kiwanja ghorofa ya 22 au 57 unaambiwa wewe kiwanja chako sasa kitakuwa ghorofa ya 57 jengo namba fulani *title* fulani.

Najua sisi hatujafikia huko, lakini kama hatujaanza kufikiria kuanzia sasa hivi ujenzi wetu kwenda juu tukawa tunasambaa basi itafika wakati ardhi yetu yote itakwisha kwa ujenzi. Kutakuwa hakuna maji safi, hivi viwanda vya maji vyote vinavyozalisha Zanzibar vitafungwa, tutakuwa tunaagizia maji kutoka Mlima Kilimanjaro tunakunywa hapa. Na chakula pia sasa hivi Zanzibar ni *net importers*, takwimu juzi zimetolewa zote na Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pia kwamba tunaagizia mara kumi zaidi kuliko kile tunachokizalisha sisi wenyewe, kwa hiyo sisi ni *net importers*.

Mhe. Naibu Spika, tunaweza kwamba tusifikie kiwango hicho, lakini kuanzia sasa tayari *trend* ya wananchi wenyewe kiuchumi imeshaonekana kubadilika. Maeneo ya pale kwa Boko sasa hivi utaweza kuona kuna ghorofa mbili tatu zimeshaanza kuja juu, hii inatokana na kwamba mfumo wa kiuchumi pia unabadilika, wananchi wenye fedha wanakuja, wananunua zile nyumba nne, tano wanaunganisha wanajenga ghorofa. Mfano mzuri sana ni eneo la Kariakoo Dar es Salaam, sasa hivi Kariakoo nyumba za chini nadhani za kuhesabu hamna tena, ukipita hata kwa ndege unaona Kariakoo imetanuka na imekuwa mji mkubwa zaidi kuliko hata ule mji wa zamani; kule *Samora Avenue* na *Independence*, hii yote inatokana na *town plan* na ndio miji inavyokuwa.

Sasa ningependa sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atakapokuja ajaribu kutoa ufafanuzi wa hizi plani ambazo ziko tayari kwa maeneo ya mjini, maeneo ya Kariakoo pale, maeneo ya huku ng'ambo ambayo yalikuwa yakiitwa Ng'ambo, yote haya yatatekelezwa lini na yatatekelezwa vipi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kufanya haya masuala ya *monitoring and evaluation*, lakini wakati napitia hiki kitabu nikakuta kwamba Idara hii ya Mipango na Sera katika utekelezaji wake inashirikiana na *COSTECH*. Sasa kidogo nikawa najiuliza, hawa Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia kwa sababu nawafahamu kidogo wana utaalamu wa mambo ya ardhi, wana utaalamu wa mambo ya *town plan*, utaalamu wa *land issues* hizi, utaalamu wa kisheria zaidi. Kwa sababu ninajua mimi Tanzania tuna ma-*consultant* wazuri sana katika masuala ya ardhi na *planning*.

Sasa kidogo hapa ningeomba ufafanuzi hii *research* yao, *COSTECH* hawa wanatumika katika nini zaidi na kwa nini vile vyombo vyengine kama vile *ESRF, Inter-consult* na ma-*consultant* wengine ambao wako chini ya *CRB* na

wengineo ama *Architects Board* hawatumiki hao, ambao tayari wameshafanya kazi kama hizo kubwa, na naamini kazi hizo pia zimeshafanyika hapa Zanzibar kwa mambo mengi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana nimpongeze huyu Mama wa Idara ya Ardhi na Usajili. Kwa kweli amekuwa akifanya kazi katika mazingira magumu. Mimi siku moja nilifika pale ofisini kwake na ile ngazi Mhe. Naibu Spika, sijui hata kama waziri itaweza kumchukua, maana ukipanda zinadata ngazi zile na Mahkama nayo iko pale pale bahati nzuri Mahkama iko chini na kesi zinapoendeshwa watu wote wale wanaotoka shamba Matemwe huko kwenye kesi nyingi na maeneo mengine wanakuwa wanakaa nje pale Majestic mkururo mzima, kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Bahati nzuri panauzwa badia pale kwa hiyo wanapo pahala pa kula badia.

Ningemuomba sana Mhe. Waziri yeye wizara yake ndiyo inayoshughulika na ardhi, makaazi, ujenzi, nyumba, na mengineyo; kuna nyumba hizi za serikali ambazo ziko maeneo ya Jimbo hili la Kiembesamaki pale Migombani, ziko nyumba za *Eacrotanal*, ziko nyumba nyengine madirisha yake yanaendelea kutolewa, nyengine zinakuwa *vandalized* zinaibiwa usiku, kwa nini wasifikirie kama wizara hii Mahkama ni sehemu ya heshima, Mahkama ndio mtu anakwenda kudai haki yake, kwa nini wasifikirie Mahkama kuwapatia jengo moja ambapo majengo mengi yako chini yake Mhe Waziri na wizara yake pamoja na hii Idara ya Ardhi na Usajili wakapata sehemu.

Mhe. Waziri ile ngazi itakuja kuanguka siku moja, maana ni ngazi ya asili na kwa watu wazito kama mimi na wengine tukipanda pale siku moja tutakuja kuachia kile kibao kimoja kifuate chengine mpaka mtu afike chini. Kwa hiyo, ningeomba sana Mheshimiwa maeneo hayo ya ofisi zenye hadhi kubwa kama hizo wangepatiwa angalau sehemu nzuri zaidi za kufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, naelewa sana kwamba matatizo mengi pia ni ya kurithi, kwa sababu ni matatizo ambayo yametokezea miaka ya nyuma kama miaka mitano, kumi na kadhalika, lakini huu ujenzi unaweza kuendelezwa kutokana na hizi *plan* au makubaliano tuliyoweka. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri aje na semina kwa Wajumbe, kwa sababu sisi hatuna utaalamu wa ardhi tunachangia tu hapa, sio Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wengi wenye utaalamu wa ardhi, tunachangia tu kwa kutumia *experience* ya hapa na pale.

Tunamuomba sana Mhe. Waziri aje nazo hizi semina ambazo kuna sheria mpya hizi zinapitiwa za ardhi, kuna mapitio ya sheria za ardhi yanafanyika. Kuna sheria mpya ya uthamini nayo pia inaandaliwa, kuna *Land Tenure Act*, *Land Adjudication Act*, sheria ya usajili, sheria ya upimaji, yote haya Mheshimiwa tufanyiwe semina ili tuzipitie tuweze kupata taaluma ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, nilibahatika kupata hii ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ambayo iliundwa mnamo tarehe 10 Agosti, 2012. Nimebahatika kupitia maelezo mengi ya ripoti hii na mwisho yametolewa maoni ya kamati, na maoni ya kamati yanakwenda sambamba pia na yanayoelezwa katika kitabu cha Waziri.

Kwa hiyo, mimi namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atoe tu japo jawabu dogo kwamba ripoti hii imefikia wapi katika serikali kuifanyia kazi, je, haya maoni ya kamati hii tukufu wamefanya kazi kubwa sana, kamati hii inastahiki kila aina ya pongezi, maana wakati naipitia ripoti hii mimi mwenyewe nimeelimika kiasi kikubwa sana, na nadhani katika ripoti zote kwa historia ya Baraza za Kamati Teule hii ni ripoti nzito, ilikuwa nzito kweli kweli. Miongoni mwa maoni niliyokuwa nikiyapitia ya mwanzo kabisa ni wananchi kuelimishwa kuhusu dhana ya ardhi kuwa ni mali ya serikali, dhana hii tuelimishwe vizuri.

Kwa sababu hata huku eneo la *Airport* sasa hivi kuna mgogoro mkubwa sana wa viwanja vya wananchi ambao wanapingana na Mamlaka ya *Airport* katika utanuzi wa uwanja wa ndege, nafikiri na Mheshimiwa analijua hilo.

La pili katika maoni ya ripoti hii hii imesema watendaji wa wizara inayohusika na ardhi na watendaji wengine wa serikali kuelimishwa juu ya sheria za ardhi. La tatu, kwamba hizi sheria zenyewe nazo za ardhi zisimamiwe vyema.

Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee la nne serikali iongeze kasi ya utambuzi wa ardhi yaani *Land Adjudication* na ndio maana utekelezaji wa ripoti hii utaongeza kasi ya mambo yote yaliyowekwa ndani ya hii ripoti.

Mhe. Naibu Spika, namba tano ni mpango wa matumizi ya ardhi. Naomba tupatiwe, tuelimishwe, tufahamishwe na baada ya hapo utekelezaji ufuatie mara moja. Kwa sababu kama hatujayatekeleza haya ndio tunakwenda kwenye matatizo yale yale. Nambari Sita sheria zote na sera za ardhi zifanyiwe mapitio. Nambari Saba sheria ya *Social Decree* Sura ya 105 itekelezwe ipasavyo. Namba Nane uimarishaji wa Mahkama ya Ardhi, hili nimezungumzia kwamba jengo lenyewe hali ile.

Namalizia namba Tisa uratibu wa taasisi za serikali zinazohusika na ukodishwaji wa ardhi pafanyike uratibu. Kwa sababu migogoro mingi pia nayo inatokana na *ZIPA* kasema hivi, Wizara ya Ardhi huku imesema hivi, huku *authority* nyengine, Mazingira inasema hivi na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, nambari 10 ni kuwepo kwa *database* ya kuhifadhi kumbukumbu za ardhi kwa sababu kumbukumbu ni muhimu. Sisi sote siku moja tutakuwa hatupo watakuwa watoto wetu na wajukuu wetu, vita vijavyo kama havijatokezea kwenye maji vinaweza kutokea kwenye ardhi, watu kugombaniana ardhi, na sasa hivi tunaona tayari kwamba ndugu kwa ndugu wanagombaniana ardhi.

Nambari 11 viongozi na watendaji wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu masuala ya ardhi, hili nalo lina umuhimu wake.

Na la mwisho kabisa katika ripoti hii ni ufutaji wa haki ya matumizi ya ardhi ufuate misingi ya Katiba na kifungu cha 56 cha sheria ya matumizi ya ardhi. Hilo muhimu sana na ninaamini Mhe. Waziri kama shujaa, jasiri, alivyotajwa humu katika ripoti hii kwa ngome hii ya wananchi, naamini sana na yeye alikuweko toka siku ya mwanzo ya ngome hii inapoundwa kama ilivyoeleza ripoti hii mwaka 1980, naamini hilo atalisimamia vizuri na atakuja kutupa maelezo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia sasa kuna haja ya *survey* yetu ya nchi nzima kufanyika kwa sababu ardhi yetu inalika. Kila kukicha ardhi haiongezeki inapungua kwa sababu bahari ukanda huu wote unakula. Kuna nyumba zilikuwemo kwenye ardhi zamani sasa hivi nyengine zimeshazama ukanda wa Bwejuu kuja huku kusini kwenda ukanda wa mashariki wote unaliwa, ina maana ardhi yetu inazidi kupungua.

Bahari inaanza kuja sehemu ya katikati kufikia hadi Jozani, huku upande wa Uzi nako bahari inaingia ndio maana ile mikoko imeacha kukatwa kwa sababu angalau ardhi ipate kujijenga kidogo.

Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba sana na Pemba najua kuna tatizo kama hilo ifanyike *survey* ya nchi nzima wananchi waelezwe maeneo yepi ambayo yanafaa kujengwa au yataruhusika kujengwa. Maeneo yepi ni marufuku kabisa kujengwa, maeneo yepi yatakuwa ni ya kitalii yaani *zoning*, maeneo yepi yatakuwa ya wananchi wenyewe na maeneo yepi ambayo tutaruhusika kwenda juu zaidi ili misingi yetu chini tutakapochimba isianze kutoka maji ya chumvi.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa naomba sana kuwapongeza ndugu zetu hawa wa *ZECO* na *ZAWA*. Mimi nawaita watoto pacha hawa wawili ingawa wote wawili huwa wanakuwa na matatizo ya hapa na pale lakini ni watoto pacha; maana kama hakuna umeme maji hayatoki kwenye *pump* zetu, lakini na *ZAWA* nao kama hawajawalipa hawa pesa zao pia wanakuwa na madeni kule Bara tutakatiwa umeme.

Jana sijui ulikatwa kwa sababu gani lakini nasikia ilikuwa sehemu kubwa sana pamoja na Dar es Salaam umeme ulikatwa kwa kipindi fulani, maana watu walikuwa wanajitayarisha kuangalia Kombe la Dunia wakaingia hasara ya kukosa kuangalia televisheni zao.

Sasa namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja kutoa maelezo kidogo aeleze hawa *ZAWA* wana tatizo gani la kifedha kuwalipa hawa *ZECO*. Kwa sababu *ZECO* wasipolipwa kwa wakati deni lile linakuja kwa wananchi, na deni lile linapokuja kwa wananchi ndio gharama zetu za umeme zinapopanda, na zikipanda tunaumia sisi na wananchi ambao tunawawakilisha humu ndani. Sasa lazima na wao tuwatetee.

Bado gharama zetu ziko nafuu kidogo ukilinganisha na sehemu nyengine, lakini hawa wakilipwa kwa wakati basi na zile gharama kidogo zitakuwa nafuu.

Nawashukuru sana *ZAWA* wamebadilisha ule mfumo wao wa kampeni ya katakata maji walikuwa kila pahala wanaingia kijeshi, siku hizi wameanza kutoa matangazo mazuri ya kirafiki, wanaingia wanasema tunakuja kuwaelimisha wale waliokuwa hawajajisajili.

Naomba sana Mheshimiwa aendelee wakija na ile operesheni ya katakata watakuja kupambana na wananchi na itakuwa hatari. Wale wananchi ndio walipa kodi wao, ndio wanaowalipa zile pesa za *ZAWA*.

Kwa hivyo, lazima waende na *customer service*, waende na *customer care*, ziwe nzuri kama kwenye mabenki au makampuni ya simu ambapo sisi huwa tunakwenda tunapata huduma zile, basi na *ZAWA* nao waendelee na jitihada hizo hizo. Nawapongeza sana wameshaanza kubadilisha mwelekeo wao na wanakwenda kirahisi zaidi na wateja wao ambao ni wananchi wanaotumia maji ya *ZAWA*.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo, mengi niliyoyazungumzia hapa naunga mkono na mengine yaliyobakia nitasubiri ufafanuzi wa Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha. Namtakia kila la kheri, ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukakutana hapa.

Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii niweze kusema machache. Aidha, nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Naibu Waziri wake na watendaji wao wote kwa juhudi kubwa wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze mchango wangu katika ukurasa wa 36 Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe. Mhe. Naibu Spika, wanasema kwamba umefanyika ukaguzi wa nyumba zilizomo ndani ya eneo la Mji Mkongwe na ikabainika kuwa nyumba 40 zina hali ya uchakavu ambayo inahatarisha maisha ya watu.

Mhe. Naibu Spika, niiombe sana Serikali juu ya jambo hili kuona inachukua hatua za dharura ili kuweza kuwanusuru wakaazi na hata wale wapita njia. Ili yasije yakatokea madhara yakabomoka majumba yale wakaweza kuathirika walio karibu na pale lakini na hata pengine wale ambao wanapita njia tu. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri kuliangalia sana jambo hili, *hadhari ni bora kuliko athari*.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu niende katika Idara ya Upimaji na Ramani. Mhe. Naibu Spika, idara hii katika majukumu yake imeendeleza utoaji wa huduma za upimaji wa ardhi nchini. Pamoja na juhudi hizo lakini bado niiombe Serikali kuangalia sana na kuwa makini sana. Mchangiaji aliyemaliza kuchangia ameomba kufanywe *survey* nchi nzima. Pia Mhe. Asha Bakari Makame alizungumzia kuhusu jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, kuyapima maeneo ambayo bado hayajapimwa ni jambo la busara ili kunusuru ujenzi wa kiholela. Mhe. Naibu Spika, Serikali itakapokaa tu bila ya kuyapima maeneo, wananchi wetu wanyonge na wanaohangaika kutafuta makaazi hawatoweza kujua kama wao wakae wasubiri hali ya kuwa wao pahala pa kukaa hawana wanataka kujenga.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mkurugenzi, kuna eneo mimi kila mara nalitolea mfano na naendelea kulisemea, hata juzi nilikuwa katika eneo hilo Fukuchani/Kigongoni Wilaya ya Kaskazini 'A', kuna eneo bado kubwa, zuri halijavamiwa sana. Kwa hivyo, naiomba Serikali na nimuombe sana Mkurugenzi labda tukimaliza hii bajeti twende tukakae katika Halmashauri ya Wilaya ili tuweze kubadilishana mawazo na wenzetu pale pengine wanaweza angalau wakachukua hatua za kuona wanazuia ule ujenzi holela na baadae watu waweze kufuata mfumo mzuri. Kwa hivyo, naomba yeye kama Mkurugenzi atakuwa na elimu ya kwenda kutoa pale katika halmashauri na itaweza kuchukuliwa hatua.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika Shirika la Umeme. Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kupongeza sana kazi kubwa ya shirika ambayo inajitahidi, pamoja na changamoto zilizopo lakini tuweze kusema kwa kweli imefanya kazi nzuri, kwa sababu leo huwezi kutofautisha mji na vijiji. Vijiji ambavyo tayari vimepata umeme na maji yapo ni sawasawa na mjini tu. Kwa hivyo, nipongeze kwa kazi kubwa, na tunaelewa kama maendeleo hatuwezi tukayapata kwa siku moja wala siku mia moja, ni lazima tutaendelea kuyapata kidogo kidogo. Na tunafarajika tunasema tunaziona juhudi na tunatia matumaini makubwa kama tunaweza tukafikia pahala pazuri.

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Umeme lina mradi wake ule wa ufungaji wa mita za TUKUZA. Lengo hasa la kufunga mita hizi ni kutaka kuendeleza ukusanyaji wa mapato. Mhe. Naibu Spika, shirika lingeweza kupata fedha za kutosha za kuweza kufunga mita hizi, ni kweli zingeweza kuongeza mapato kwa sababu ingekuwa sasa tunatumia lipa utumie na sio tumia ulipe. Ingelikuwa lazima kwanza ulipe umeme ndio uweze kuutumia. Kama tunavyofanya simu, simu huwezi ukapiga kama wewe hujaweka vocha. Sasa mradi huu ungeweza kufanikiwa vya kutosha kama zingepatikana fedha za kutosha na wao naamini wangeweza kupiga hatua moja nzuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika changamoto za ufungaji huo wa mita za TUKUZA katika mawizara yetu. Mhe. Naibu Spika, wizara kama tunavyoelewa zote zinatumia umeme na zina jukumu kubwa kabisa la kuhakikisha wanalipa umeme. Kwani Waswahili wanasema "*Ukiona taa inawaka ujue mafuta yanateketea*." Kwa maana hiyo, Shirika la Umeme linapotupa umeme tukaona unawaka maana yake lazima tuweze kuulipia ili na wao waweze kuununua umeme huo.

Mhe. Naibu Spika, changamoto ya wizara katika ufungaji wa mita hizi za TUKUZA, kama tunavyoelewa mita hizi hazina uwezo mkubwa wa kuchukua umeme mwingi, kwa hivyo katika wizara inalazimika pengine iweze kufunga mita hata mbili au tatu. Kwa hivyo, naomba sana mawizara yetu yaweze kulisaidia Shirika la Umeme kulipa gharama hizi ili na wao waweze kukuza juhudi zao katika mradi wao huu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji. Mhe. Naibu Spika, kusema kweli naipongeza pia Serikali kwa juhudi kubwa ambazo inazifanya katika kusambaza maji mijini na vijijini, kwa kweli juhudi ipo lakini kwa sababu ya kuona bado pia penye neema na mabaya lazima yanaweza yakawepo. Kwa hivyo, pamoja na juhudi hizo lakini bado na changamoto zipo. Nataka niseme jinsi gani ya ukosefu wa maji huu tunapoupata hata kuna mshairi mmoja aliweza kutoa shairi na akasema juu ya umuhimu wa maji. Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu.

Mhe. Naibu Spika, mshairi alisema ;

" Maji yakiadimika viumbe tuko tabuni,

Chai haijapikika kwa sukari na majani,

Sharti maji kuchemka yawemo sufuriani,

Ndipo utapotosheka ukaitia bulini,

Maji yakiadimika viumbe tuko tabuni.

Tena si kwa mtu peke yake bali hata hayawiani,

Akila majani yake na maji yawe usoni,

Lazima uyakumbuke au mnyama haponi,

Maji yakiadimika viumbe tuko tabuni".

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuona mshairi alivyolalamika juu ya maji tunapoyakosa, basi naomba na mimi nielezee pamoja na juhudi za Serikali lakini nimuombe Mhe. Waziri hii bajeti itakuwa ya pili kukwambia kama Mkokotoni kuna tatizo kubwa la maji. Mhe. Naibu Spika, mimi naomba mara hii tukimaliza hapa bajeti basi twende na Mhe. Waziri tukaangalie ni changamoto gani ambayo inaikumba kijiji kile mpaka maji hayawezi kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wakaazi wa sehemu ile wanapata shida sana, wanasumbuka kwa maji, na hasa tukielekea sasa katika mwezi mtukufu wa Ramadhani. Namuomba sana Mhe. Waziri basi katika wale watu ambao atawasaidia katika kuwapa magari ya maji na kijiji cha Mkokotoni kifikiriwe kupatiwa msaada wa gari la maji ili na wao waondokane na usumbufu katika ule mwezi wa Ramadhani. Pia nimuombe Mhe. Waziri katika mradi wake wa uchimbaji wa visima basi afikirie kuchimba kisima pale Mkokotoni ili kiweze kusaidia changamoto hii ya ukosekanaji wa maji katika kijiji kile.

Mhe. Naibu Spika, pia namuomba sana Mhe. Waziri aangalie sana kwa sababu maji hayafiki mpaka lile eneo la Ikulu ambapo kule tunategemea kila mara kupata wageni wa aina mbali mbali, ukiachilia mwenyewe Rais anapotembelea katika mkoa ule hufanya mapumziko pale.

Kwa hivyo, aliangalie tatizo hili maji yanafika mpaka KMKM tu na kwa baadhi ya siku, inaweza ukapata maji wiki hii pengine mwezi hayajatoka au miezi miwili. Sasa mwezi huu mtukufu wa Ramadhani huwa kunafanyika mafutarisho pale, kwa hivyo Mhe. Waziri nikuombe sana juu ya hili uweze kulishughulikia.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu kwa leo haukuwa mkubwa sana, lakini nilitaka tu niseme changamoto hii ambayo inakikumba hichi kijiji cha Mkokotoni kuhusu maji, lakini pia kuhusu kupimwa maeneo ili wananchi wakaweza kupata kuyatumia maeneo hayo katika njia nzuri ambayo itaweza kuondosha usumbufu wa ujenzi holela.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naomba kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa na afya njema mchana huu. Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kutuwasilishia hotuba yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Pia niwapongeze watendaji wote kwa kazi zao nzuri wanazozifanya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitokuwa na mchango mkubwa nitachangia maeneo mawili matatu kwa ufafanuzi. Nataka nianze uhifadhi wa nyumba za Mji Mkongwe. Mhe. Naibu Spika, katika eneo la Mji Mkongwe kuna nyumba ambazo ni chakavu sana kama ripoti ilivyoeleza nyumba zipatazo 40 hazikaliki kutokana na uchakavu huo. Pia Mhe. Naibu Spika, nyumba hizi zinahatarisha amani katika maeneo husika.

Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu naiomba wizara iwaelimishe wamiliki hao kuweza kuzikarabati nyumba hizo. Pili, Serikali iweke sheria ndogo ndogo za kuwabana wamiliki ili waweze kuzifanyia matengenezo nyumba hizo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Sekta ya Ardhi. Mhe. Naibu Spika, wizara ndio ina jukumu la kutoa ardhi, lakini utaona kuwa kuna muingiliano wa majukumu baina ya Wizara, Masheha na Halmashauri. Namuomba Mhe. Waziri anieleze mwenye jukumu la utoaji wa ardhi ni nani? Hii itasaidia kupunguza migogoro ya ardhi ambayo kila siku inajitokeza.

Mhe. Naibu Spika, pia na mimi nichangie kuhusu maeneo yanayojengwa mabondeni. Mhe. Naibu Spika, kama walivyochangia wenzangu kwamba sasa wananchi wanajenga mabondeni maeneo ambayo yamepangiwa ni ya kulima. Labda Mhe. Waziri kwa vile yeye pia huwa anakaimu Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa hivyo suala hili atakuwa analijua vizuri, kwamba ni maeneo gani ambayo yanahusika kujengwa na maeneo gani yanahusika kulima. Kwa hivyo, naiomba wizara ijitahidi kusimamia matatizo haya wananchi kujenga katika maeneo ambayo hayahusiki ili kuona tatizo hili linaondoka.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika Sekta ya Maji nichangie chemchemu ya maji Mwanyanya. Mhe. Naibu Spika, chemchemu hii inachangia karibu asilimia 30 ya maji ya mjini. Chemchemu hii hivi sasa imevamiwa na hata kile kiwango cha maji kinachozalisha kimepungua.

Namuomba Mhe. Waziri aweke ulinzi katika maeneo hayo pia kujenga uzio ili kudhibiti eneo hilo lisiendelee kuvamiwa zaidi. Pia Mamlaka ya Maji iweze kufanya kazi zake vizuri kwa sababu inahitaji mapato yakiwemo malipo ya maji. Mhe. Naibu Spika, naiomba wizara isichoke kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ulipaji wa maji, kwani mapato hayo ndio yatakayosaidia upatikanaji wa huduma ya maji kwa maeneo ambayo yanakosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu katika Shirika la Umeme. Nalipongeza shirika kwa ubadilishaji wa mita katika maeneo mbali mbali, na naliomba shirika liweze kufunga mita za TUKUZA katika taasisi za Serikali ili kuweza kupunguza deni la umeme ambalo linaendelea kukua siku hadi siku. Naomba wizara zinazofanyiwa marekebisho ya kubadilisha mita hizo zijitahidi kulipa fedha kwa ajili ya marekebisho hayo, kwani wao wanatumia fedha nyingi kwa ajili ya kununulia vifaa mbali mbali ikiwemo TUKUZA. Tukizingatia baadhi ya wizara zinatumia zaidi ya TUKUZA moja. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Fedha itenge fedha maalum kwa ajili ya kazi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, pia nizungumzie suala la kero ya umeme katika nyumba za wafanyakazi. Mhe. Naibu Spika, kusema kweli nyumba nyingi za wafanyakazi hasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, kule kuna malalamiko kwamba wale wafanyakazi wanaohamishwa katika maeneo yale wanakuta madeni ambayo madeni hayo si yao wamerithi. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri naomba utakapokuja kutoa majibu uniambie suala hili mumeliwekea mkakati gani kuona matatizo hayo yanaondoka. Kwa sababu malalamiko haya yanapokuja ni kweli tukiangalia wale wanaohamia katika maeneo ambayo deni limekuwa si lao, ni kweli inakuwa ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile mimi nilisema sina mchango mkubwa. Kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi naunga mkono hoja hii asilimia mia juu ya mia. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa. Sasa nafasi tunampa Mhe. Hamza Hassan Juma baadae Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na kama muda tutakuwa nao Mhe. Amina kaomba dakika 10, tunaweza na yeye tukampa nafasi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi ninataka nikushukuru kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuzungumza katika kuchangia na kuiboresha hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza kabla sijaanza na mchango wangu huu, ninataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa umakini wake katika kufanya kazi, lakini vile vile katika ukweli wake katika kusimamia kazi. Pia katika kutujali na kututhamini Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, katika wizara ambayo ilikuwa siku ya bajeti yake, humu ndani munajaa basi ilikuwa ni wizara hii. Kila mmoja alikuwa ana hamu, kila mmoja anasema sijui niikamate wapi, leo Waziri sijui nimkamate shati, wengine nimkamate koti, wengine nimkamate mkono, viatu. Kila mtu alikuwa na hamu kubwa sana kuisubiri bajeti hii. (*Makofi*).

Lakini ninadhani Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri sijui kama hayupo katika ukoo wa Kisharifu. Maana yake Mhe. Naibu Spika, kule Mchangani kule, kuna Masharifu. Sasa ninadhani Mhe. Waziri huyu, bila shaka na yeye katika ule ukoo wake itabidi tufanye utafiti, tuutafute hasa asili yake Mhe.Waziri kama hana asili ya Usharifu. (*Makofi*).

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, katika bajeti hii, kikubwa zaidi ni kuboresha yale maeneo ambayo aliyokuja nayo, lakini vile vile kikubwa ni kumpa na ushauri wa ziada ili aweze kuufanyia kazi. Kwa kuwa Mhe. Waziri huyu ametuonesha kulithamini Baraza la Wawakilishi, tunapomshauri ushauri mbali mbali basi leo mchango wangu mkubwa utakwenda zaidi katika kumshauri Mhe. Waziri kwenye kuboresha hii wizara yake. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ninadhani Mhe. Rais huwa anasikiliza sana Baraza la Wawakilishi. Pamoja na kwamba hivi sasa hayupo nchini lakini ninaamini akirudi huwa anafuatilia *hansard* zetu, lakini vile vile pengine huwa anataka mpaka rekodi zetu. Basi ninadhani kutokana na umahiri aliouonesha Mhe. Waziri huyu, mimi ninaweza kusema ni kiraka. Basi ninadhani sasa hivi ipo haja akahamishiwa kule Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kule, akaenda akaziba. (*Makofi*).

Maana yake kule bado kuna mashimo mengi yanataka kuzibwa. Huku wizara hii kwa kweli ameshaziba. Ndio maana nikasema huyu ni kiraka, lazima mtu haki yake tumpeni. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sisi wengine kuna watu wanafikiria labda sisi tuna chuki na watu fulani, tuna chuki na mawaziri, hakuna, isipokuwa tunataka utendaji uliokuwa bora, utendaji uliotukuka. (*Makofi*).

Sasa mtu anapofanya kazi yake vizuri ni lazima tumpe haki yake. Sasa ninaamini akirudi safari Mhe. Rais atasikia hicho kilio na kuweza kwenda kutuzibia lile shimo ambalo hatuoni namna gani linaweza likazibika. (*Makofi*).

Baada ya hayo, sasa ninataka niende katika mchango. Mhe. Naibu Spika, mchango wangu leo nitauelekeza jimboni kwangu kwanza.

Mhe. Naibu Spika, nimeona kwenye hotuba ya Mhe. Waziri kwamba anakusudia kuboresha miundombinu ya maji katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi. Kwa kweli hiyo nia tu peke yake, mimi nimesharidhika. Isipokuwa tu ninaomba sana Mhe. Waziri kwa sababu sasa hivi baada ya bajeti hii, bajeti inayokuja Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu. Tunapokwenda kwenye uchaguzi mkuu wananchi hasa wa Mkoa wa Mjini Magharibi kama hawajapata maji ya kutosha, tutakuwa na kazi kubwa sana ya kuweza kuwaeleza na kuendelea kutupa ridhaa, lakini kama nilivyosema sifa nilizommwagia Mhe. Waziri, ninaamini atakaa na watendaji wake wa Mamlaka ya Maji na tunaona jitihada zao, ingawa wakati mwengine wananchi wanalalamika tunakatiwa maji, ndio

mambo, kwa sababu unaambiwa sasa hivi kula na ulipe, huwezi tu tena ukawa wewe unafanyiwa tu kila kitu. (*Makofi*).

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri basi katika kipindi hichi, ndani ya bajeti hii, basi mkazo wake mkubwa zaidi auelekeze katika kutatua tatizo la maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi katika fedha za mfuko wa jimbo, nimeamua nisitumie matumizi mengine yoyote, isipokuwa ni kuchimba visima vya maji. Kwa kiasi fulani hata lile jina langu sasa hivi, jimboni kule limeanza kutambulikana vizuri. Maana yake wengine walikuwa walisahau jina langu, walikuwa wananiita Mheshimiwa maji. Kila ukipita pahala Mheshimiwa maji! Mheshimiwa maji! Lakini alau baada ya kupata nguvu kidogo kupitia fedha zetu za mfuko wa jimbo, tumeweza kuchimba visima. Ingawa Mkurugenzi alikuwa hapendi sana kuchimba chimba sisi visima vya maji, tukamwambia Mkurugenzi bwana wewe mwenzetu umeteuliwa, sisi tumechaguliwa.

Wewe umeteuliwa huko hata kama maji huku hayapatikani utarudi, lakini sisi kama maji hayapatikani mzee hapa, jumba hili tutaliona hivi hivi. Kwa hivyo, kwa kiasi fulani tulikuwa tunambana lakini ilikuwa katika kuisaidia serikali katika kuwapatia wananchi wetu maji. (*Makofi*).

Ninashukuru ninadhani ndani ya mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani wananchi wetu kwa kiasi fulani watakuwa wanatumia zaidi visima tulivyovichimba sisi, lakini tunaamini mwakani kwa maelezo ya Mhe. Waziri tunaweza tukafaidika na huduma hii ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine sijaondoka jimboni bado. Nazungumzia kumkumbusha tu Mhe. Waziri pamoja na wasaidizi wake kuhusu kupatiwa hatimiliki kwa ile miradi ya wananchi ndani ya Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Naibu Spika, tumepeleka barua ya kukumbushia na ninaamini Mhe. Waziri, kwa sababu nilimwambia Katibu wangu kule wa jimbo, nikamwambia kwa kuwa Mhe. Waziri ana bajeti sasa hivi inawezekana hizo barua asiziangalie, lakini ninaamini baada ya kumaliza bajeti na mimi nitakumbushia kule basi tuweze kupatiwa ile hatimiliki ya miradi yetu.

Kwa sababu kama hivi sasa Mhe. Naibu Spika, tayari katika safari zangu mbali mbali nimetafuta wahisani wa kuweza kutusaidia kwenye ujenzi wa Chuo cha Amali kwenye Jimbo la Kwamtipura. Sasa eneo hivi juzi alimleta mtu wake, nimekwenda kumkaguza. Sasa hivi wanataka michoro. Sasa ninapeleka michoro, hati sina. Sasa nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri basi aweze kutusaidia na sio atupe bure hati, tutalipa kama utaratibu wa kawaida, tutalipa kama wanavyolipa wananchi wengine ili kuweza kusogeza huduma katika jimbo letu la Kwamtipura.

Mhe. Naibu Spika, ninafanya hivyo kwa sababu ukiangalia katika jimbo langu hivi sasa nina vijana ambao waliomaliza *form 11*, wengine wamemaliza *form IV*, wengine hata *form VI* lakini wamemaliza skuli tu hawana taaluma ya kazi za amali. Kwa hivyo, tukiweza kujenga chuo kile, na kwa bahati nzuri hao wahisani wangu ambao watakaokuja kushirikiana na sisi, wao wamesema katika hatua za mwanzo watatuingizia mpaka na vile vifaa vya kufanyia kazi. Mfano mashine za kufundishia masuala ya elektroniki, mambo ya *electrician*, hata na *carpentry* ninafikiri tutaweza kufaidika sana katika jimbo hili.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri kuna miradi mengine ambayo tumeshaijenga tunaitumia lakini hatuna hatimiliki, na unajua siku hizi kuna mambo ya *joint venture*, wakati mwengine hata unapotaka kwenda benki pengine kutaka kukopa unaambiwa ulete hatimiliki. Sasa utakuta *assets* ambazo za kuweza kuweka *guarantee* tunazo, lakini sasa tunakuwa hatuna zile hati. Kwa hivyo, nilikuwa ninamuomba sana Mhe. Waziri, naamini hili ataweza kunisikiliza ili kuweza kuondokana na tatizo hilo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka niingie katika Idara ya Ujenzi. Kuna suala tumelizungumza, suala la uanzishwaji wa Shirika la Nyumba. Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, wenzangu hapa wamesema kwamba mji wetu haujajengeka vizuri, mji haupendezi. Moja katika mji kupendeza, mji kujengwa kwa mpango. (*Makofi*).

Sasa kwa ujenzi tunaojenga sisi hivi sasa, leo umetia kuti moja, kesho tofali moja. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi ukija jimboni kwangu Kwamtipura, kuna nyumba haijapigwa rangi lakini utafikiri imepigwa rangi. Kuna tofali jeupe, kuna tofali jengine jekundu, kuna tofali jengine rangi ya kijivujivu, kwa sababu mtu kila baada ya miaka mitatu kapata matofali 10 kaweka, baada ya miaka mitatu kanunua matofali 20 kaweka. Kwa hivyo, utakuta ile nyumba utafikiri imepigwa rangi tofauti tofauti, kumbe yale matofali yameshaanza kuzeeka.

Sasa utaratibu kama huu Mhe. Naibu Spika, tusitegemee kama tutapata mji ambao unaopendeza na uliopangika, lakini tukiweza kuanzisha Shirika la Nyumba na wakaweza kutafuta *funds*, wakatafuta wabia, na sasa hivi kuna watu wengi tu, kuna mashirika mengi ambayo yana fedha nyingi, ninaamini wakianzisha utaratibu wa kutafuta wawekezaji kuweka ubia katika miradi ya *real estate*. Ninafikiri ndio itakuwa muokozi mkubwa kwa ujenzi wa nyumba hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nchi za wenzetu, sio wananchi wengi ambao wanamiliki nyumba zao wenyewe. Zanzibar hapa kwa utamaduni wetu tunamiliki nyumba zetu wenyewe, lakini kwa wenzetu kuna mashirika ya nyumba, yanajenga nyumba, yanakodisha na mengine yanakuwa yanauza yanawauzia wananchi. Tena yanawauzia kwa muda mrefu kwa *installment*; pengine miaka 10, miaka 15, miaka 20, mtu anakaa katika nyumba analipa kidogo kidogo mpaka anamaliza.

Kwa hivyo, mimi ninadhani Mhe. Naibu Spika, tumuombe Mhe. Waziri basi hili Shirika la Nyumba lianzishwe, liboreshwe, na apewe nafasi huyu Mkurugenzi wa hili Shirika la Nyumba aweze kutoka nje, kwenda kutafuta mitaji. Na mitaji ipo, na ninaamini shirika hili litaweza kuja kufanya kazi nzuri.

Kuna maeneo ya kupata fedha hili Shirika la Nyumba yapo, mfano hapa kuna Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, kuna *Islamic Bank* pale, lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, sasa hivi tumeanza kuwa na utamaduni wa wenzetu wa nchi za ulaya, makampuni kuuza *shares*, hata Wazanzibari ninaamini wapo wengi.

Sisi tulipokwenda Marekani na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ingawa sasa hivi hayupo, lakini vile vile tulipopita Falme za Kiarabu pale, hata Uingereza Mhe. Naibu Spika, wapo Wazanzibari, hata Oman kuna kipindi maalum kilirushwa na *Channel Ten*, Wazanzibari waliokuwepo kule wanazo fedha lakini wanatafuta makampuni ya kununua *shares* Zanzibar. Sasa Zanzibar bado hatujakuwa na makampuni ambayo yanauza *shares* isipokuwa wenzetu Tanzania Bara wameanzisha utaratibu huo.

Kwa hivyo, ninaamini Shirika la Nyumba likishaanzishwa basi maeneo ya kuweza kupata fedha kwa ajili ya kuweza kuanzisha huu mradi, kwa kweli maeneo yapo na wateja wapo wengi. Wafanyakazi wa serikali watakuwa ndio wateja wa mwanzo, wafanyabiashara watakuwa ni wateja wa pili, lakini hata Wazanzibari waliopo nje ya nchi watakuwa vile vile ni wateja wa kununua hizo nyumba. Hata sisi huko mitaani Kwamtipura, tunauza urojo, *chips*, mapapai na malimau tutakuwa na uwezo wa kukodi hizo nyumba, lakini vile vile baadae kuweza kuzinunua.

Kwa hivyo hili ninaliomba Mhe. Naibu Spika, tukiweza kuanzisha mradi wa *real estate* ninaamini kutajengwa nyumba za kisasa, nyumba zilizokuwa bora, halafu mji wetu vile vile utaweza kupendeza.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kuna mwenzangu hapa Mwenyekiti wa kamati, aliwahi kulizungumza suala la umeme mbadala. Tunashukuru sana Kamati hii ya Mawasiliano na Miundombinu kwa jitihada zao za kuweza kuzungumza

na wale wenzetu kampuni moja ya China, ambao wametuonesha nia ya kutaka kuja kuwekeza umeme mbadala hapa Zanzibar.

Umeme kwa njia ya *solar*, lakini vile vile kufanya utafiti na kuanzisha umeme kwa njia ya upepo. Tumeona wana uwezo wa kuzalisha mpaka *megawatts* karibu 100 ambapo sisi Zanzibar mahitaji yetu ni *megawatts* 50 mpaka *megawatts* 55 kwa hivi sasa. Kwa hivyo, tunaamini wenzetu wale wakiweza kuja kuwekeza katika mradi huu wa umeme mbadala basi tutaweza kulipunguzia Shirika la Umeme mzigo wa kununua umeme kwa bei kubwa.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika bajeti iliyopita kwamba umeme tunaonunua kutoka *TANESCO*, shirika letu linabeba mzigo mkubwa wa kulipa. Kwa sababu kuna umeme mwengine Mhe. Naibu Spika, niliwahi kukaa na wataalamu wa masuala ya mambo ya umeme, wakasema kuna umeme mwengine ambao unaopotea njiani kabla haujafika Zanzibar. Wanasema wenyewe katika hizi njia kuu za umeme kuna vikombe vile, vikikatika vile basi umeme unakuwa unavuja, lakini kule umeshasoma kwamba umekuja Zanzibar na umekuja unatumika.

Lakini tukiweza kupata umeme huu wa *solar* au umeme wa upepo, ninaamini tunaweza tukalipunguzia mzigo Shirika la Umeme. Vile vile kuweza kuwa na umeme wa uhakika. Kwa hivyo, nilikuwa ninamuomba sana Mhe. Waziri awaambie basi hawa watu wa Shirika la Umeme kuwasiliana na kampuni ile ili kuangalia namna gani wanaweza wakashirikiana ili shirika letu liweze kufanya kazi vizuri.

Vile vile, tunawapongeza Shirika la Umeme kwa sababu katika ripoti iliyokuja, ripoti ilikuwa kali, kuna maeneo mengi ambayo tulikuwa tumeyasemea wameyafanyia kazi. Tumejaribu kuangalia hata mapato ya shirika yamekuwa yameongezeka. Sasa tunawaomba isiwe yale ya mgema, mgema akasifiwa tena tembo kulitia maji.

Sasa nilikuwa naomba sana Mhe. Naibu Spika, wenzetu hawa waendelee na jitihada zao hizi, lakini vile vile kama kuna marekebisho mengine ambayo yaliyoagizwa na Kamati yako ya Baraza, kama hayajafanyiwa kazi basi yaweze kufanyiwa kazi. Ninaamini kama nilivyosema mwanzo Mhe. Waziri yale tunayoyasema mengi umejaribu kuweza kuyafuatilia.(*Makofi*).

Jengine ambalo hata wenzangu wamelisema lakini na mimi kwa kuwa linanikera inabidi niliseme.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma bado dakika 5 na wenzako wapate dakika kumi kumi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya basi nitakwenda haraka haraka. Kwenye Shirika la Umeme tulikuwa tunaomba sana haya ya vibandani tena kwenda kupiga foleni, wanawake wanaume yameshapitwa na wakati. Tunataka tulipe umeme hivi sasa kupitia kwenye simu zetu za mkononi. Kwa hivyo, ninadhani sina haja ya kuzungumzia sana hapo, ilikuwa hiyo *message* nataka kuileta.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie mambo matatu tu kwa haraka haraka. Nilikuwa ninamuomba sana Mhe. Waziri, umezungumzwa sana huu mradi wa kuweka ukuta wa pale Forodhani, yaani unazingia maji kuja juu.

Ukuta huu Mhe. Naibu Spika, mimi niliwahi kuwa Mjumbe wa Bodi kwenye Shirika la Bandari, tuliwahi kuzungumza na *Aga Khan Foundation* wakakubali kuujenga ukuta ule, lakini walikuwa wana masharti yao, yalivyokuwa masharti yao hayakutimizwa mradi ule waliuacha.

Sasa namuomba Mhe. Waziri amalize bajeti yake, akishamaliza bajeti yake wapo Wazanzibari ambao wameamua kutaka kuujenga ukuta ule, lakini wanataka kuujenga ukuta ule kwa masharti maalumu ambayo masharti hayo Mhe. Waziri tukija tukikaa na hao wananchi ambao ni Wazanzibari, ni wawekezaji ninafikiri tunaweza tukafika pahala tukaelewana nao. Kwa sababu mradi kama ule wanaotaka kuufanya wao, tulikuta hata kule Seattle Marekani ambao

kule wanaita *Sea Front*, ambao wanajenga ule ukuta, halafu wanaweka kitu kama ilivyokuwa ile gati ya zamani ya miguu, halafu wanaweka vi-*restaurant* pale kwa ajili ya viburudishaji, ambapo wanataka kuunganisha kutoka pale Forodha Mchanga mpaka kuja huku hii Forodhani yenyewe.

Kwa hivyo, hata ile mandhari ya pale Forodhani itaweza kuongezeka, kwa sababu patazidi kupendeza, lakini kwa kuwa hawa watu wapo hapa hapa Zanzibar, nitamuomba Mhe. Waziri akishapumzika baada ya bajeti yake aniambie nimpelekee wamuoneshe ule mradi wenyewe. Naamini watu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe pengine huo mradi wameshawahi kuuona. Mimi nitapendelea sana ikiwa huo mradi Mhe. Waziri atausimamia ili uweze kufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa ni suala la mwekezaji ambaye ni Mzanzibari, na mimi nafurahishwa sana na Wazanzibari sasa hivi wameamua kuwekeza.

Kuna mwenzetu ambaye anataka kujenga *deport* ya kuwekea ma-*tank* ya mafuta hapa Zanzibar. Mimi naomba sana Mhe. Waziri apewe mashirikiano na serikali, ameshafanya kazi kubwa, akiweza kuweka *deport* zile Zanzibar tutakuwa na mafuta ya uhakika, kutakuwa hakuna uchakachuaji, lakini vile vile mafuta yale yataweza kuuzwa hata nje ya Zanzibar ambapo itaweza kutoa ajira nyingi tu kwa Wazanzibari na pia pato kwa Taifa.

Mhe. Naibu Spika, suala hili nitamuomba Mhe. Waziri mradi huu kama bado hajaupata basi hao wawekezaji wapo Zanzibar nitawaita pamoja na yeye tumuoneshe, ili kuangalia uwezekano wa kuweza kuwekeza katika eneo hili.

Mwisho kabisa katika eneo la Mji Mkongwe kuna malalamiko kidogo hapa kwamba kwa upande wa Mji Mkongwe kuna wajenzi wengine wanaruhusiwa kuweka madirisha ya vioo, lakini kuna wananchi wengine hawaruhusiwi kuweka madirisha ya vioo. Sasa hili nitamuomba Mhe. Waziri aje anipe ufafanuzi kuna masharti gani Mji Mkongwe, ambayo wengine wanawaruhusu na wengine hawaruhusu.

Baada ya hayo machache kama nilivyosema naunga mkono hotuba hii, naamini ule ushauri nilioutoa Mhe. Waziri atauchukua. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma. Sasa nafasi tunampa Mhe. Amina Iddi Mabrouk na mwisho tumalizie na Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Mhe. Bihindi Hamad Khamis.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nidhati. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na uzima.

Pia nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuandaa hotuba hii ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wetu wa Zanzibar. Naamini kwamba kazi ya kuandaa hotuba hii sio kazi rahisi sana, wamepoteza muda wao, wameikalia na hatimaye wakaweza kutufikishia hapa ndani ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa sana kama ulivyoniambia kuwa nitumie dakika kumi tu, na pengine hata hizo dakika kumi nisizishe. Nilikuwa nataka tu na mimi nitie barka katika hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, nianze katika ukurasa wa 15 kuhusu Mahakama ya Ardhi. Kama alivyotwambia Mhe. Waziri katika kitabu chake hiki, alituelezea kesi mbali mbali ambazo wamezishughulikia za migogoro ya ardhi.

Mimi nasema tu kwamba pamoja na Mhe. Waziri alivyotwambia katika kitabu chake hiki kwamba bado malalamiko mengi ya malimbikizo ya kesi ya ardhi yapo, wananchi wanalalamika sana, kesi zinalimbikizwa katika Mahakama ya Ardhi.

Mhe. Naibu Spika, kama sote tunakumbuka hapa katika kipindi kilichopita tulikuwa tunapata malalamiko sana ya wananchi kuhusu ulimbikizaji wa kesi za ardhi. Pia kama tutakumbuka zaidi hata katika Baraza lako hili Tukufu tulisemea sana kuhusu malimbikizo ya kesi za ardhi na hii inatokana na kuwa kulikuwa kuna Hakimu mmoja tu ambaye anashughulikia masuala haya ya ardhi.

Mimi niipongeze sana wizara kwa kusikia kilio cha wananchi jinsi wanavyolalamika kuhusu ulimbikizaji wa kesi za ardhi na pia kuwasikia Waheshimiwa Wajumbe walivyokuwa wanazungumza na kulalamika kuhusu malimbikizo haya ya ardhi. Pia alileta mswada wa sheria mwaka 2010 na tukarekebisha masuala haya ya sheria ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mtizamo wangu pamoja na sheria ile tuliirekebisha na ikawa kwamba kila mkoa kuwepo na Hakimu katika Mahakama ya Ardhi, lakini bado mpaka hivi sasa malimbikizo haya ya kesi za ardhi yapo na wananchi bado wanalalamika.

Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri atwambie kwamba je kupitishwa kwa sheria ile kweli imefanya kazi, na katika kila mkoa sasa hivi yupo Hakimu wa Ardhi, kama yupo namuomba Mhe. Waziri aje kutwambia. Jengine atupe tathmini kwamba pamoja na kuwa tumepitisha sheria ile, matatizo ya kesi hizi za ardhi yamepungua kwa kiasi gani. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho anipe ufafanuzi huo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nimpongeze sana Mhe. Waziri, alitwambia katika kitabu chake kwenye ukurasa wa 19, kwamba anaendelea na kazi zake za kutengeneza *master plan* ya mji wetu. Hili ni jambo la faraja sana, lakini Mhe. Naibu Spika, kama tunakumbuka katika miaka ya 1980 hapa walikuja Wachina na walitengeneza hiyo *master plan* ya mji wetu, na kwa kweli *master plan* ile ilikuwa ni nzuri, ilikuwa inapendeza, na kama serikali tungeifuata *master plan* ile basi sasa hivi tusingekuwa na haja ya kutayarisha *master plan* mpya.

Nasema hivyo, Mhe. Naibu Spika, kwa sababu *master plan* ile ambayo ilitayarishwa katika mwaka wa 1980, yalikuwa mambo yote yamejieleza namna mji wetu utakavyokuwa mzuri, ilikuwa inaonesha sehemu muhimu za huduma za afya zikae wapi, ilikuwa inaonesha sehemu za makaazi yawepo wapi na pia *master plan* ile ilikuwa inaonesha barabara zinatakiwa zipite wapi. Kwa masikitiko makubwa sana serikali kwa asilimia 90 *master plan* ile haikuweza kutekelezeka kwa sababu mbali mbali. Hatimaye maeneo mengi ambayo pengine kipindi kile yalikuwa ya wazi ingewezekana sana *master plan* ile kutekelezeka, lakini hatimaye maeneo yale ya wazi yalivamiwa na kujengwa majumba, na hatimaye kufikia *master plan* ile isitekelezeke.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri sasa hivi ametwambia kwamba anaendelea na matayarisho ya hiyo *master plan*, na *master plan* ili itekelezeke inahitaji nguvu za Serikali Kuu. Kwa sababu kipindi kile ambacho kulikuwa na maeneo mengi ya wazi lakini haikutekelezeka *master plan* ile, sasa sijui Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze katika maandalizi ya *master plan* hii, amejiandaa vipi katika utayarishaji wa *master plan* hii hata serikali iweze kuitekeleza. Kwa sababu *master plan* yoyote inahitaji fedha, kwa sababu ndani ya *master plan* ile pengine kutakuwa kuna mali za watu kama majumba, majumba yale inabidi yavunjwe na hatimaye wale wahusika walipwe fidia, na tunafahamu kwamba sasa hivi serikali yetu ina kipindi kigumu sana cha fedha, na sote tunafahamu Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, si hilo tu, ukiangalia sasa hivi hakuna maeneo yaliyowazi, maeneo yote ya mji huu kwa kweli yamevamiwa na yamejengwa. Sasa kuna kazi kubwa kwa Mhe. Waziri labda pengine amejipanga, lakini kwa mtizamo wangu mimi binafsi sidhani kwamba *master plan* hii ambayo anaitayarisha itafanikiwa.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, mimi naamini kwamba katika utayarishaji wa *master plan* fedha nyingi tu zitagharimu katika utayarishaji wa *master plan*. Kwa hivyo, isijekuwa tunatayarisha *master plan*, na kama mtu atakuja kuiangalia *master plan* ile itakuwa inapendeza kwa sababu ya rangi nzuri zilizotiwa, lakini hatima ya *master plan* ile itakuwa haitekelezeki ukitizama kwamba serikali imeshatumia pesa nyingi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie vizuri ili tusije tukapoteza fedha za serikali.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa wa 43, kuhusu Mamlaka ya Maji. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ametwambia hapa katika kitabu chake kwamba ana mipango mingi ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar anawaondolea tatizo la usumbufu wa maji kwa asilimia kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika labda niseme jambo moja. Mimi nawawakilisha hapa wanawake wa Mkoa wa Mjini na Magharibi. Kama tunakumbuka sisi Mhe. Naibu Spika, katika kipindi kilichopita kulikuwa na mradi hapa mkubwa tu ambao ulifadhiliwa na Wajapani, mradi ule uligharimia sizaidi ya dola milioni 10 na mradi ule wananchi walikuwa wana matumaini makubwa kwa mradi ule.

Kama tunakumbuka sote ulizinduliwa Mabluu, na hata mimi mwenyewe nilishiriki katika uzinduzi ule, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walishiriki, na ulizinduliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar wa Awamu ya Sita.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wa Mkoa huu wa Magharibi walijenga matumaini makubwa sana kwa mradi ule, na waliambiwa kuwa kukamilika kwa mradi huu, kwa kweli tatizo la maji katika Mkoa huu wa Mjini litakwisha na wananchi wote wa Mkoa wa Mjini watapata maji. Kulikuwa kuna matangi ya maji pale mengi tu yamewekwa pale Mabluu.

Sasa Mhe. Waziri sijui mradi ule ulifikia vipi, hatuna taarifa wala katika kitabu hiki hakioneshi chochote kuhusu mradi ule wa Japani, lakini si hilo tu Mhe. Naibu Spika, bado tatizo la maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi lipo, wananchi wa Mkoa wa Mjini Magharibi wanasumbuliwa sana na ukosefu wa maji.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika kitabu chake ametuonesha miradi mingi, sasa mimi nina hofu Mhe. Naibu Spika, isijekuwa tunakwenda mbele tu ya nyumba hatuyajui wala hatufanyi tathmini. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho atwambie mradi ule umekwendaje hata ikawa wananchi wa Mkoa wa Mjini Magharibi bado wanasumbuliwa na tatizo la ukosefu wa maji.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nije hapo hapo katika mradi wa maji. Mara zote katika kipindi cha Ramadhani basi maji ndio yanakuwa tatizo na tumebakisha kama siku nne tu au tano kuingia katika mfungo wa Mwezi wa Ramadhani. Sasa Mhe. Waziri namuomba atwambie kuwa amejipangaje katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar, hasa katika kipindi cha Ramadhani watapata raha vipi kwa kuhakikisha kwamba wanapata maji safi na salama, na sio kuhangaika kwa suala la maji.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika mchango wangu nije katika Idara ya Nyumba. Mhe. Naibu Spika, kitabu hiki kimechanika na karatasi zimetawanyika, lakini labda nielezee tu kwa kifupi, ametwambia katika utekelezaji wake amesema kwamba ametengeneza mitaro, amezibua mitaro katika hizi nyumba.

Mhe. Naibu Spika, mimi bado sijaona, umuhimu upo lakini bado sijamuelewa Mhe. Waziri, kwa sababu kuna mambo muhimu na ya msingi sana katika utengenezaji wa nyumba hizi za maendeleo, bado nyumba za maendeleo zinavuja, zina ufa. Mimi nilitegemea Mhe. Waziri atwambie hapa kwamba ni nyumba ngapi pengine amezifanyia ukarabati na matatizo ya kuvuja maji yamepungua kwa kiasi gani, kuliko kila mwaka kitabu kinatwambia kwamba

amezibua makaro na huku nyumba zinaendelea kuharibika, na inapelekea kupoteza fedha za serikali nyingi sana Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri ili kumuenzi aliyejenga nyumba hizi basi ni kuhakikisha kwamba tunazikinga ili zisiporomoke, pamoja na kwamba mitaro nayo ina umuhimu wake, lakini mimi namuomba Mhe. Waziri atwambie amejipanga vipi katika kuona kwamba zile nyumba ambazo ni mbovu, zinavuja na zimepata ufa anazitatua vipi.

Mhe. Naibu Spika, kama ulivyoniambia umenipa dakika 10. Kwa hivyo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini nasema kwamba Mhe. Waziri akinijibu na akinipa ufafanuzi wa kuniridhisha basi nitaiunga mkono hotuba yake kwa asilimia mia kwa mia. Sasa hivi nasema kwamba naiunga mkono kwa asilimia 95, nakushukuru Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Amina Iddi Mbarouk kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, kwanza niwashukuru kwa mashirikiano ya tangu asubuhi mpaka sasa hivi, naomba nitoe maelezo yafuatayo.

Jioni nimebakia na mchangiaji mmoja ambaye ni Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Mhe. Bihindi Hamad Khamis na baadae Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, halafu baadaye tunamuita Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Tunafanya majumuisho tukisha tunaakhirisha kikao, tutamalizia vifungu siku ya Ijumaa, tunategemea *quorum* yetu itakuwa nzuri na wenzetu watakuwa wamesharudi kwenye Mkutano Mkuu.

Kesho lakini tutaendelea itasomwa Wizara ya Fedha na tutachangia kutwa na hii tutaimaliza jioni siku ya Ijumaa, na Jumamosi tutamaliza mswada wetu na mambo yatakuwa yamekamilika. Baada ya hayo naakhirisha kikao hadi saa 11:00 za leo jioni, tuje mapema kusikiliza majumuisho.

(Saa 6:58 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo hii kuweza kuchangia hotuba hii. Vile vile, napenda nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini Pemba kwa kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Pia, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mchango nianzie kwenye miradi ya maji. Kwa kweli naipongeza sana wizara pamoja na serikali, sababu ya kusema hiyo ni kwamba kwenye Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba miradi ya maji imefikia hatua nzuri na vijiji vyote vya wilaya mbili, yaani Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu kwenye miradi ya maji na mimi ni Mwakilishi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Tukianzia Wilaya ya Micheweni naipongeza sana serikali pamoja na wizara kuweza kuondoa tatizo la maji Shumbamjini pamoja na maeneo yote ya Wilaya ya Micheweni na hasa Jimbo la Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la umeme. Vile vile, niipongeze serikali pamoja na Mhe. Waziri, kwa kuweza kushughulikia suala la umeme Wilaya ya Micheweni na hususan Jimbo la Micheweni. Kwa kweli Micheweni walikuwa na tatizo la umeme kwamba ilikuwa hauna nguvu, lakini niipongeze serikali pamoja na

wizara kwa kuweza kuliondosha suala lile na hivi sasa wananchi wanapata umeme kwa ajili ya familia na hata biashara. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kuhusu suala la nyumba.Naomba nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa kufuatilia kwa ufanisi zaidi kwa kushirikiana na Katibu Mkuu na Afisa Mdhamini Pemba pamoja na Wakurugenzi wake wote walioko Pemba, pamoja na hapa Unguja.

Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu wafadhili, kwa sababu hivi sasa tunao wafadhili wengi ambao wanatujengea misikiti ambayo iko kwenye vijiji vyetu. Serikali sio kama haifuatilii, isipokuwa inafuatilia vya kutosha na wananchi wanaweza kufanyiwa mambo yao pale wanapoomba, lakini nikiwa Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, pia ni Mwakilishi wa Viti Maalum Wanawake, niko kwenye serikali na mkoa. Hivyo, naipongeza sana serikali pamoja na wizara. Micheweni kuna vijiji mbali mbali ambavyo vimefikiwa na mahitaji ya umeme, lakini umeme kwa Micheweni umefikia nyumba za *flats* mpaka sokoni Chamboni.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kuna vijiji vyengine kama vile vya Kijiji cha Jichwagumu na Kipangamize, Mhe. Waziri, sehemu hizi bado umeme haijafika. Nampongeza Mhe. Waziri pamoja na serikali, lakini katika hili Mhe. Waziri, naomba alichukue kwa ajili ya kulifanyia kazi, ili kuwafikishia wanavijiji wale na waweze kupata mahitaji. Waheshimiwa Wajumbe, kama tunavyojua, kwa mfano Mhe. Bikame Yussuf Hamad, amezungumzie kuhusu kukopeshwa umeme, lakini pale utakapofika umeme ukiwa ni karibu wananchi wanaweza kukopa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli serikali imechukua hatua za kutosha kwa ajili ya kushughulikia miradi mbali mbali inayohusiana na wizara hii. Pia, namuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali iweze kukaa na wananchi kwa ajili ya kuweza kupata mahitaji yao vizuri pamoja na serikali. Pia, kuna msikiti umejengwa maeneo ya Maziwang'ombe karibu na kufika Radio Jamii, wamepata mfadhili na wamejengewa msikiti, lakini Mhe. Waziri, tatizo lao ni umbali wa nguzo za kufikishia umeme kwenye eneo lile la msikiti, sababu ya kusema hivyo ni kwamba kijiji cha Micheweni Chamboni umeme umefika, lakini kama watasogezewa nguzo na takribani nguzo tano mpaka sita umeme utafika kwenye msikiti wao huo wananchi wa Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, naipongeza wizara tena, wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wote kwa juhudi wanazozichukua na mimi ni mwanamke ambaye ni Mwakilishi tena ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, serikali naipongeza sana kwa juhudi zake kwa kuweza kufuatilia miradi mbali mbali ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu, sasa naomba nizungumzie kuhusu matatizo ya ardhi.Kwa mashirikiano ya Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, suala hili wanalifuatilia vya kutosha, kama vile kuwakusanya wananchi na kuweza kutatua matatizo ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, naipongeza serikali kwa juhudi hizo na kuweza kutoa ufafanuzi wa kina na kila mmoja akapata haki yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ninachangia upande wa serikali, naunga mkono hotuba hii kwa upande wa serikali, pia ni Mwakilishi Viti Maalum Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.Kwanza kabla sijachangia, naomba nitoe shukurani zangu kwako wewe Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kunipa ushirikiano mzuri katika wizara hii, lengo kuu ni kuhakikisha kuwatumikia wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba pamoja na kujenga mustakbali mzuri wa wizara yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, vile vile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote pamoja na watendaji wote wa wizara hii, katika kukaa pamoja na kuipanga bajeti hii na hatimaye leo kuifikisha katika kikomo ndani ya Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe ufafanuzi mdogo tu, kwa sababu Mhe. Waziri ndiye atakayekuja kutoa ufafanuzi kwa urefu.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nianze na Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, yeye kwanza ameipongeza wizara yetu, tunasema kwamba pongezi hizi tumezipokea na tunamshukuru. Pia, ameelezea suala zima linalohusiana na mchango katika nguzo za *line* kubwa ya umeme. Suala hili kweli lipo na hili linaiathiri serikali kupitia Shirika la Umeme, kwani watu wasioitakia mema Zanzibar ndio wanaofanya kazi hii na bila ya kufikia kwamba pindi itakapotokezea athari waathirika ni Wazanzibari wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano jana kwa bahati mbaya tumepata tatizo la kuzimiwa umeme kutokana na matatizo yaliopo *TANESCO*.Aidha, hapa Zanzibar, Dar-es-Salaam na baadhi ya mikoa mingine lilitokezea tatizo kama hilo la kiufundi na hatimaye tukakosa umeme kwa muda.Kwa kweli suala hili kama tutajikumbusha na kulizingatia na huu ni mtihani mzito sana. Sasa kama kuna wananchi ambao wanafanya vitendo vya makusudi kuhujumu miundombinu hii, wajue athari si ya serikali tu, isipokuwa mpaka wananchi wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, malalamiko mengine sana tumeyapata leo kwamba kuna watu wamepoteza baadhi ya vitu au vifaa vyao baada ya kutokea tatizo hilo la jana. Kwa hivyo, nawaomba sana wananchi suala hili wasifanye na sote tuwe walinzi wa miundombinu yetu, ili Zanzibar tufikie pahala pazuri katika suala zima hili la umeme. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, vile vile, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, yeye amelipongeza Shirika la Umeme na pongezi hizi tumezipokea na yeye pia tunampongeza sana kwa jitihada na hatua anazozifanya za kushirikiana na wizara hii. Hata hivyo, Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu nguzo mbovu katika maeneo ya Pete. Napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe, pamoja na Baraza lako kwamba tatizo hili tumelipokea na tunalichukua kwa ajili ya kulifanyia kazi. Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme imesikia na itafuatilia na wala si muda mrefu tatizo hili tutalirekebisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia, Mhe. Mjumbe, alizungumzia kuhusu suala la kuongezwa vituo vya kuuzia umeme. Suala hili tumelipokea na katika jitihada za Shirika la Umeme tumeongeza vituo viwili, kwa hivi sasa ninavyo ni Kituo cha Makunduchi na Gamba. Vile vile, tunao mpango ambao tayari tumeshakaa na wenzetu wa Kampuni ya *Zantel*, kwamba si muda mrefu huduma hii tutauza kupitia simu za mkononi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi ashirikiane na sisi na lengo la serikali hii ni kuhakikisha wananchi, kuwa hawasumbuki kwa huduma zote, aidha, ikiwa huduma ya umeme pamoja na huduma za maji safi na salama.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salma Mussa Bilali, yeye alitoa pongezi kwa wizara na tunamshukuru kwa pongezi zake na tumezipokea. Pia, alizungumzia kuhusu tatizo la umeme mdogo inapofika wakati wa Magharibi, suala hili ni kweli, isipokuwa nataka nimthibitishe Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako kwamba wizara yangu kupitia Shirika la Umeme inalichukua suala hili na italifanyia kazi na *Inshaallah* baada ya muda litakaa sawa, kwa sababu suala hili mara nyingi linasababishwa kutokana na kuzidi kwa watumiaji wa umeme hususan kutokana na *transfomer* wanayotumia. Kwa hiyo, tutakwenda kuangalia katika maeneo hayo na tuone *transformer* ambayo ipo ni *size* gani, inatumika kiwango gani na imezidiwa vipi, tukeshalijua hili tutajitahidi sana na kama ikiwa ni suala la *transformer* tutajitahidi kubadilisha *transformer* na kuondoa ndogo na kuweka *transformer* ambayo itakayoweza kuhimili matumizi ya wananchi katika eneo husika.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, yeye alizungumzia kuhusu suala la kukatiwa mifereji 100 ambayo iko ndani ya kijiji cha Jambiani. Suala hilo ni kweli limefanyika na hadi hivi sasa Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) inaendelea na zoezi hili la kupunguza baadhi ya mifereji ndani ya vijiji. Namuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako wafahamu kwamba Mamlaka ya Maji haina nia mbaya kufanya hivyo, isipokuwa inafanya hivyo kwa malengo mazuri ya kuwasaidia wananchi ambao wako vijijini kupata huduma hiyo ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, katika uchunguzi tuliofanya kuna baadhi ya mifereji katika vijiji haikuwekwa kitaalamu isipokuwa imewekwa tu kwamba mimi nahitaji hivyo uwekwe hapa. Kama tutaangalia mifereji inapoongezeka katika hali kama hiyo kwa kupitia bomba moja, hatimaye hata miundombinu hiyo inaweza ikakosa kabisa kutoa maji kutokana na kutobolewa pasipokuwa na utaalamu wa kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi kwamba tushirikiane na sisi, tuko pamoja na yeye katika suala zima hili la kusambaza maji vijijini, tena tunampongeza sana kwa sababu amejenga mashirikiano makubwa hususan katika kazi zinazofanyika ndani ya jimbo lake. Kwa kweli mara nyingi ni mtu ambaye yuko makini sana, anajali na mara zote yuko tayari kuchangia kwa hali na mali, ili jimbo lake lifanikiwe katika huduma hii ya kuwaenezea wananchi huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwakilishi, pia, katika Jimbo la Muyuni ametuelezea kwamba kuna baadhi ya vijiji bado havijapata huduma hiyo au vinapata huduma, lakini haitoshelezi. Suala hilo ni kweli tunalielewa na tunalifanyia kazi na katika jitihada zilizofanywa na wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ni kulifuatilia pango la Kitogani, kwa ajili ya kutaka kuongezea katika mradi ambao upo ambapo kwa hivi sasa ni kweli kuwa hautoshelezi kuwasambazia wananchi wote wanaoishi katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, tumefanya utafiti, ili tupate kuongezea nguvu ya maji. Sasa kwa bahati mbaya baada ya kufanya utafiti wetu tumegundua kwamba lile pango maji yaliyokuwemo hayakidhi haja kutokana na chumvi ambayo imo ndani ya pango hilo. Kutokana na hali hiyo, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji, bado inaendelea na juhudi za kutafuta njia ya kuongeza huduma hiyo hususan katika Jimbo la Muyuni, Hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe, atustahamilie na serikali iko makini katika hili na inaliangalia Jimbo la Muyuni pamoja na majimbo mengine, kwani lengo la serikali ni kusambaza huduma ya maji safi na salama katika vijiji vyote vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kutoa ufafanuzi kuna suala la wananchi wa Kilindi kukosa huduma ya maji na hili lilizungumzwa na Mhe. Bikame Yussuf Hamad. Tunamshukuru Mhe. Mjumbe, kwamba suala hili tumelipokea na ninataka nimthibitishie kwamba suala hili lipo, lakini sababu inayosababisha wananchi wa Kilindi kukosa huduma maji safi na salama wananchi wa Kilindi. Katika kijiji cha Kilindi Nungwi kuna mradi ambao umeelekea Nungwi na mradi huo kisima chake kimechimbwa Kilimani Tazari na tangi la mradi huo limejengwa Kilindi Nungwi, ambapo chini ya tangi hilo kuna visima viwili, kisima kimoja kinasaidia kupandisha maji kwenye tangi kikiungana na kisima cha Kilimani Tazari, kwa ajili ya kuwapelekea maji wananchi wa Nungwi.

Mhe. Naibu Spika, Kisima chengine hicho maalum kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Kilindi, kwa bahati mbaya kisima hichi si muda mrefu kimeungua *pump*, baada ya kuungua *pump* tumekaa na watendaji wetu tumelijadili suala hili na hivi sasa tuko katika hatua za kutafuta *pump*, ili kuirejesha *pump* na wananchi hao wapate huduma hiyo, lakini pamoja na hayo, Mamlaka ya Maji kushirikiana na Wizara yetu hii tulichokiamua ni kwamba baada ya kuirejesha *pump* hiyo kile kisima vile vile nacho tukielekeze kwenye tangi ili visima vitatu vyote vitapandisha maji kwenye tangi, basi tutakuwa na uwezo wa wananchi wa Kilindi na wao kuwaunganisha kwenye tangi, tunaamini kwamba tutakapofanya hivyo, basi wananchi wa Kilindi na wao hawatosumbuka tena na tatizo hili la huduma ya maji safi na salama.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile, tulitaka tuonane na wananchi wa Kilindi tufanye mazungumzo yanayofaa kwa sababu katika maeneo ya Kilindi kuna wawekezaji wengi tu kutoka katika kijiji cha Kendwa wameunganisha bomba zao kupitia mradi ambao unaosambaza maji katika maeneo ya Kilindi. Sasa huu mradi wa Nungwi si mradi wa wawekezaji ni mradi wa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, tunachotaka kukifanya ni kwenda Kilindi tukakae na wananchi wa Kilindi watuthibitishie na watuhakikishie kwamba watakuwa pamoja na Mamlaka ya Maji katika suala zima la kulinda mradi wa Maji ili wawekezaji wasiunganishe maji katika mradi huo. Kwa sababu lengo la serikali kuhakikisha kwamba mwananchi kwanza ndiye anayefaidika na huduma hii ya maji safi na salama na hatimae ndipo tuwape wawekezaji. Kwa hivyo, kwa mradi mdogo kama huu basi nataka kwanza waendelee kupata wananchi ikesha mradi mkubwa unaofuata ndipo wapate wawekezaji, kwa hivyo Mhe. Bikame hili suala tumelichukua na *Inshaallah* tutalifanyia kazi na wananchi wataondokana na tatizo hilo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la kuwasambazia wananchi huduma ya maji katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani, Mhe. Raza, Mhe, Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Hamza na Mhe. Amina, tunasema kwamba hili suala tumelipokea na *Inshaallah* tutalifanyia kazi, kama kawaida ya Wizara hii kupitia Mamlaka ya Maji kwamba kila ifikapo Mwezi mtukufu wa Ramadhani, huwa tunapeleka huduma ya maji safi na salama katika yale maeneo ambayo miundombinu yetu bado haijafikia, huwa tunatumia magari yetu na magari ya kukodi ili kuwasambazia wananchi huduma hiyo kwa kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani, tunajua mwezi huu kila Muislam

anatakiwa akae atulie avute pumzi asipate matatizo yoyote. Kwa hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeliona hili kupitia Wizara yangu tutajitahidi kuwasambazia wananchi hao na vile vijiji vyote ambavyo tunajua kwamba huduma yetu kupitia miundombinu haijafika, basi tutajitahidi kuwapelekea huduma hiyo katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani.
Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile, tunaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tushirikiane katika hili kwa sababu wananchi macho yao wanatuangalia sisi.

Mhe. Naibu Spika, nimesema kwamba sitaki nichangie sana isipokuwa nimeomba tu nijibu baadhi ya hoja. Kwa hivyo, niseme baada ya hayo machache kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nungwi naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa tena pumzi tukakutana tena wakati huu hapa kuzungumzia mambo ya maendeleo ya wananchi wa nchi yetu katika masuala mbali mbali kama Waheshimwa Wajumbe walivyosema, Wizara yangu hii ni Wizara ambayo imegusa mambo yote muhimu masuala ya ardhi, masuala ya majengo na majumba, masuala ya maji na masuala ya nishati, ni masuala muhimu ambayo lazima katika maisha uende nayo, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa hili.

Mhe. Naibu Spika, michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe ni mingi baadhi ya michango ile inahitaji kupokelewa na kwenda kufanyiwa kazi na baadhi ya michango inahitaji kupatiwa majibu hapa hapa. Nitawaomba Waheshimiwa Wajumbe kwa yale mambo ambayo itabidi yachukuliwe yakafanyiwe kazi na ndio kujenga unapotoa rai kuna baadhi ya wakati inabidi kuna jambo likafanyiwe kazi na kuna jambo itabidi ulitolee jibu pale pale kama limeshakuwa linatekelezwa, lakini tu uelewa kidogo haukuwa mkubwa kujua kwamba kitu gani kinaendelea.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe waliozungumza katika Wizara yangu hii ni 20, nashukuru sana ni idadi nzuri sana, mmoja yeye amezungumza kwa maandishi ameleta michango yake kwa maandishi. Napenda niwatambue watu hao 20 waliochangia kama ifuatavyo:

Mhe. Marina Joel Thomas yeye amezungumza kwa niaba ya Kamati kumuwasilisha Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, wa pili Mhe. Mohammedraza Hassanali, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Nassor Salim Ali, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Salma Mussa Bilali, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mhe. Abdalla Mohammed Ali, Mhe. Bihindi Hamad Khamis na Mhe. Haji Makame Mwadini Naibu Waziri wa Ardhi, Majenzi, Maji na Nishati.

Mhe. Naibu Spika, inaweza kuwa kuna mtu mmoja nimemsahau au jina lake limetajwa vibaya, lakini nafikiri kama yupo namuomba radhi sana kwa sababu jina lililotajwa humu hamna humu Fatma Mohammed Ali hayumo, lakini pia, yumo Mhe. Asha Bakari Makame katika waliochangia, aliyechangia kwa maandishi ni Mhe. Mgeni Juma Hassan huyo ndiye aliyechangia kwa maandishi.

Mhe, Naibu Spika, maneno mengi yamezungumzwa kwa kweli ni maneno ya maana sana yanatutia moyo sana na yanatuvutia sana, kwa kweli ni changamoto au ni kitu kinachokufanya tuendelee kufanya kazi zaidi, lakini napenda niseme tu kwamba nasoma kunako kitabu changu hii Wizara kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe ni ngumu, ni nzito na ngumu kwa sababu ina mambo yanawagusa wao, lakini tunajitahidi sana katika kuona kwamba mambo mengi ambayo tumepewa katika Wizara hii tunatekeleza na yanaendelea vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo kubwa kabisa ambalo ni muhimu na linamgusa mtu kila siku ni suala la maji, tuna miradi ya maendeleo ya maji na tuna miradi yetu wenyewe tunayoishughulikia kuhusu maji, kwa sababu hatutegemei miradi ya maendeleo tu, lakini pia, tunachukua miradi ile tunaishughulikia sisi wenyewe katika maeneo mbali mbali, ndio maana katika hotuba yetu tukasema katika mwaka huu tunataka tukifika mwisho wa mwaka huu mwaka wa kalenda, sio mwaka wa bajeti tatizo la maji kwa Zanzibar liwe limepungua sana.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ndio nia yatu na ndio maana tuna miradi, kwa mfano kuna mradi wa Nungwi ambao upo Unguja huu tunakusudia ufanye kazi katika kijiji cha Nungwi, Kilindi, Mgunda, Tazari Kiungani, Kidoti, Potoa na

Fukuchani mradi huu ushughulikie eneo hilo, huu mradi nimeutembelea mimi mwenyewe na uko katika hali nzuri matangi tayari yameshajengwa na bomba tayari zimeshasambazwa litakuwepo tatizo dogo tu ambalo kama mita kama mia sita hivi au tuseme wasatani wa kilomita moja ambayo hiyo tutaifanyia sisi wenyewe kuhakikisha kwamba maji yanaenea katika eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi wa Matemwe, huu tunakusudia ufanye kazi kwa ajili ya wananchi wa Matemwe, Pwanimchangani, Kiwengwa, Kijini na Mfurumatonga huko ndio ufanye kazi mradi huu nao uko katika hatua nzuri sana matangi yameshajengwa ya rizavu yale, mabomba baadhi ya maeneo yameshasambazwa tayari yako ardhini yamekaa na visima vimeshachimbwa, tunachongojea sasa hivi kufanikisha ufikishwaji wa umeme katika maeneo hayo kwa ajili ya kupiga maji katika maeneo haya husika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi uliopo Machui, huu tunakusudia ufanye kazi Machui, Kidimni, Koani na Mwera na mradi huu kusema kweli ukeshajengwa pale ni rahisi sisi wenyewe kuja kuendeleza ukafika katika maeneo mengine zaidi, kwa sababu kitu muhimu ni kuwa na miundo mbinu hasa kuwa na *reserves* nzuri na kubwa, matangi yaliyomo katika maeneo haya ni makubwa yanaweza kuchukua kama hivyo lita milioni moja, milioni moja unusu, milioni mbili, milioni tatu mpaka milioni nne za maji zinazohifadhiwa katika *reserves* ya juu, maji yakiingizwa katika *reserves* hizi usambazaji wa mabomba ukienda vizuri, basi tatizo la maji litakuwa limepungua sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maradi wa Tunguu ambao huu utahudumia Tunguu, Fuoni, Fuoni Kibondeni, Jumbi utahudumia mradi huu na tumeuweka makusudi ili ufanye kazi katika maneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba, kuna mradi wa Kambini Pemba, huu unakusudiwa kufanya kazi Kambini, Mchangamdogo, Vumba, Kinyasini, Mtondooni, Bahanasa, Kisiwani na Piki, huu ndio mradi utakaofanya kazi katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maradi wa Ndagoni ambao ni Ndagoni, Buyuni, Jangini, Bikau na Wesha upo tayari na umeshajengwa kwa kweli muda si mrafu wajenzi wa miradi hii watatukabidhi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maradi wa Vitongoji ambao utakuwa Vitongoji, Changuo, Kibokoni, Furaha, Uwandani, Vikunguni huu vile vile matangi yameshasimama ukenda huko utakuta matangi yameshasimama.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi wa Wambaa ambao utakuwa Wambaa, Chumbageni, Ngelema na Tumbi. Tayari mradi huu upo na umeshajengwa, umeshajengwa sio utajengwa umeshajengwa kazi iliyopo ni kujaza matangi maji kutizama *linkage* na mambo mengine na baadae yaongezwe maji kwa ajili ya wananchi waweze kuyatumia.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maradi wa Wambaa ambao umeshatajwa wa Wambaa, Chumbageni, Lelema na Matumbi.
Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi wa Mizingani ambao huu utafanya kazi Mizingani, Mgagadu, Kwa Mkoba, Ngezi, Kuyuni, Kalami na Ngomeni huu utafanya kazi katika meneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi wa Miji, Miji ya Pemba yote imeshughulikiwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maji Pemba yanapatikana kwa uhakika na huo ni mradi wa Pemba Chake Chake maeneo yote ya Mji wa Chake Chake na huu utakuta kwamba wajenzi wapo katika hatua za mwisho, Wete vile vile wajenzi wapo katika hatua za mwisho matangi yameshajengwa tayari na Mkoani wajenzi wako katika hatua za mwisho vile vile tunategemea muda sio mrafu sana tatizo la maji itakuwa tumelipunguza sana katika visiwa vyetu viwili vya Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kuna miradi midogo midogo ambayo hii huwa tunaishughulikia wenyewe ya kuchimba visima na kutumia pesa kwa shughuli zetu za kawaida kwa ajili ya kununua mambo ya *pump* na mambo mengineyo, tumeagiza *pump* za kutosha katika kipindi hiki ili kupunguza tatizo la maji hapa Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo kwa kweli tunajitahidi sana katika wizara, ni suala la kwamba hii Wizara pamoja na kwamba inafanya kazi kwa kupeleka huduma, lakini lazima pia iwe inaongeza mapato, tukitizama *data* zetu zinaonyesha kwamba Idara ya Nyumba Maendeleo na Makaazi hii inakusanya mapato kutoka katika kodi takwimu zinatuonyesha kwamba mwaka 2010/2011, walikusanya milioni 128,043,000/=, lakini mwaka 2011/2012, wamekusanya milioni 118, wameshuka kidogo ukilinganisha na ile pale, lakini mwaka 2012 baada ya kufanya *review*, wamekusanya wameshuka kidogo milioni 116, lakini hadi mwezi mei baada ya kupandisha kodi tumepata

milioni 364, 875,000/=, yaani hapa tumepiga buu kubwa sana na tutaendelea kupiga buu kubwa sana kwa sababu tumeshafanya *review.*

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Umeme walikuwa wakikusanya bilioni mbili, hivi sasa hivi wako mbali wanakusanya bilioni tano, wanazikusanya katika kiwango hicho.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ardhi na usajili nayo vile vile imeongeza mapato hii ni kazi ambayo inafanywa na Maidara yetu mbali mbali kwa kuonyesha kwamba mapato nayo yanaongezeka na sio tunakaa hapo hapo. Kwa hivyo, tulikuwa tuna bilioni moja, tukaja bilioni mbili, tukenda bilioni mbili tena, tukaja bilioni 6,006,075,000/= hadi mwezi wa Mei juzi tulipomalizia.

Mhe. Naibu Spika, kuna hili suala la kusaidia maji katika mwezi wa Ramadhani ambalo Mhe. Naibu Waziri amelizungumza tunalijua kwa sababu tumeshalifanya kwamba ni letu na tunalishughulikia kila siku na tumepanga hata maeneo ya kupeleka maji tayari tumeshapanga na yakaitokea mengine ambayo hatukufika, basi ni vizuri watueleze kwamba maeneo fulani nako kuna tatizo, kwa mfano tumepanga kwamba keshokutwa Ramadhaini mosi, tuanze kusambaza maji Shehiya ya Kilombero, Mtopepo, Bubwini, Machui, Sebleni, Koani, Jangombe, Kwamtipura, Muungano, Nyerere, Kidimni na Mtoni, hizi ni kwa Unguja kuwafanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa Pemba tusambaze Changawe, Ng'ombeni, Mfikiwa, Kwale na Mapofu hayo ni maeneo ambayo tutakuwa tunasambaza maji. Sasa ni vizuri na nadhani tumeshatayarisha zamani kwa ajili ya kufanya kazi hiyo, tuna magari maalum tumeshayapanga kwa kufanya kazi hiyo katika mwezi wa Ramadhani ili kuweza kuwasambazia watu maji. Sasa kama kuna eneo ambalo tumeliacha ambalo lina matatizo ya maji, ni vizuri watu wakatufuata *ZAWA* na wakaeleza kwamba na eneo fulani nalo linahitaji maji tutafikisha bila ya tatizo lolote.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa umeme tunajitahidi sana kama tulivyosema katika hotuba zetu vile vile tunataka tusambaze umeme Unguja kila mtu mwenye uwezo wa kutumia umeme atumie umeme na ndio maana tumeweka utaratibu wa mkopo, mwaka huu tunategemea kwamba tusambaze umeme Kandwi, tupeleke umeme Matemwe, tupeleke umeme Bubwini Kiongwe, tusambaze umeme Paje, tusambaze umeme Bwejuu maana upo, lakini unataka kusogezwa tunataka tupeleke Bwejuu, tusambaze umeme Mbuzini, Tunguu Mji mpya upo, lakini nako tufanye kazi ya usambazaji ili kueneza zaidi Masingini, Kwarara, Makunduchi Kaskazini, Kizimkazi Mkunguni, Unguja Ukuu Tindini, Ubago Uwandani, Fuoni Kipungani, Fuoni Kitogani maeneo hayo tutayashughulikia safari hii katika bajeti hii katika kusambaza umeme kwa wananchi uwafikie.

Mhe. Naibu Spika, kwa Pemba umeme upo, lakini tunataka tuzidi kuusambaza Wete/Bopwe, Wete/Uchozini, Mwambe/Kwasanani, Limani, Mjanaza, Kinazini, Uwondwe, Chaka ni Ngao na Mtakuja hayo ni maeneo tutakuja kuyafanyia kazi, ni maeneo ambayo tunataka tuendelee kusambaza umeme na yafike katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, katika hili tumejipanga na tunataka tutekeleze kwa sababu ni jukumu letu kutekeleza katika maeneo hayo watu wapate umeme, watu wapate maji. Bila shaka yatakuwepo maeneo ambayo yatakuwa yamebakiwa. Kuna utaratibu wa kwamba kwa maeneo ambayo kuwa yana matatizo *very crucial* na kwa ghafla hatuwezi kuwa na mradi wa kupeleka, basi lile eneo ambalo tunatafuta *centre* ile *centre* tunaichimbia kisima. Nasema hivi kwa *pumps* zetu ndogo zile za *single phase*, tunachimba visima pale na tunaweka na tangi moja la lita kama elfu tano, elfu kumi, watu eneo lile wafatie maji katika eneo lile.

Mhe. Naibu Spika, hii ni kazi tunaifanya katika Wizara yetu na mifano ipo. Hii kazi kwa kweli waliotuonesha hasa ni Waheshimiwa Wawakilishi na Waheshimiwa Wabunge, maana wao ndio walichimba visima katika maeneo haya wakawa wanaweka matangi tu, alaa, kumbe na sisi *ZAWA* tunaweza tukafuata utaratibu ule pahala kwenye tatizo *crucial*, tukachimba kisima tukaweka na tangi na watu wakapata maji kwa urahisi pale, hii tunafanya sisi wenyewe hapa kivyetu vyetu. Kwa upande wa mjini tumeichukua Chumbuni palikuwa pana mtambo wa *radio* pale na tunapapanda miti.

Mhe. Naibu Spika, nitaomba sana majirani wa eneo lile wasituombe kwa kujenga kitu chochote, pale ninajua litakuwepo tatizo la watu kujificha kwa madawa ya kulevya na mengineyo, maana ile miti ikikua ninajua litakuwepo tatizo, lakini bora tulilinde, lakini tupate maji. Pale tumeshachimba visima karibu 5, sasa hivi vipo tayari pale na

ukenda sasa hivi tangi la Ras el Khaima linajengwa liko juu na Mhe. Hamza ninafikiri na wewe utajiunga katika eneo hilo la tangi lile kwa ajili ya kuingia katika Jimbo lako la Kwamtipura.

Mhe. Naibu Spika, lakini sio hiyo hata Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge wamechimba visima vyao pale katika eneo lile na hatukuwakataza na tayari wanawafikishia maji wananchi kutoka katika eneo lile. Mimi nimefurahi sana kwamba jambo hili tunalishughulikia kwa pamoja kabisa na isiwe *ZAWA* peke yake, lazima wafanye kazi tushughulikie kwa pamoja katika maeneo haya ili kuona kwamba wananchi wanapata huduma hii muhimu ya maji. Kwa hivyo, la kumuomba hapo ni kuwa Mwenyezi Mungu atuwezeshe katika kufanya mambo hayo.

Mhe. Naibu Spika, niende kidogo katika hoja ya mtu mmoja ya Wajumbe wa Baraza waliotoa michango, nimesema michango ni mizuri.

Mhe. Marina kwa niaba ya Kamati amesema kwamba Wizara ijiandae kuchukua jukumu la kuendeleza kazi ya utambuzi pindi mradi wa *SMOLE* utapomaliza muda wake rai nzuri kabisa na tunaipokea. Serikali inafahamu fika kuwa mwezi Disemba 2014 ni mwisho wa mradi wa *SMOLE* katika shughuli za ardhi hususani Utambuzi na Usajili wa Ardhi. Wizara imeshawasiliana na Wizara ya Fedha ili shughuli hizi ziendelezwe na SMZ na ili kazi hiyo muhimu isikwame. Aidha, kwa vile Katibu Mkuu wa Fedha ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozo wa Mradi huo (*SMOLE*) natumai mikakati kupokea kazi hizo zitakwenda vyema *(Transition).* Mikakati hii *(phasing out strategy)* tayari inafanyiwa kazi na Idara zote zilizo chini ya mradi wa *SMOLE*.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mvutano uliopo katika utoaji vibali vya ujenzi kati ya Idara ya Mipango Miji na Halmashauri. Ni kweli kwa kipindi kirefu kulikuwepo na maingiliano katika suala la utoaji vibali kati ya taasisi zilizopewa kazi hiyo, serikali imeliona tatizo hilo. Wizara yangu, kupitia Idara ya Mipango miji tayari imeshatayarisha Kanuni mpya zitakazosimamia masuala ya utoaji vibali vya ujenzi. Kanuni hizi tayari nimeshazitia saini na hivi punde zitachapishwa katika gazeti rasmi la serikali.Kanuni hizi zitaweka mfumo mpya wa utoaji vibali, utakaoshirikisha taasisi zote zinazuhusika na suala la ujenzi chini ya usimamizi wa Mkuu wa Mkoa.

Mhe. Naibu Spika,Mhe. Nassor Salum, ametueleza kwamba Mikakati ya Ukodishaji wa Ardhi. Wawekezaji kukaa na Ardhi kwa muda mrefu. Serikali kupitia Wizara ya Ardhi imechukua hatua ya kufuta *Land Lease* ambazo wawekezaji hawajaziendeleza kwa muda mrefu. Kwa kuanzia jumla ya miradi kumi na mbili (12) imefutwa. Aidha, ardhi kama zilizopewa Hati za matumizi nazo zimefutwa kwa kutokuendelezwa kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, hili kama nilivyosema katika bajeti iliyopita linakuja. Kwa hivyo, aliyeweka kiwanja kwa muda mrefu sisi tunakuja huko kuja kukifuta. Kwa sababu ardhi tunataka itumike, hatutaki ardhi ikae vile vile *idle*. Kwa hivyo, hii miradi tumefuta na hii tunafanya katika miradi kwa kushirikiana na *ZIPA* wamesha-*approve* miradi ambayo tuifute kwa sababu imeshakaa muda mrefu na tutaendelea kuifuta. Hii ni hatua ya mwanzo tu na tutaendelea kuzirejesha ardhi zote zilizohodhiwa iwe kwa wawekezaji wageni na hata wazalendo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba, amezungumza juu ya kushirikisha mawilaya katika kupanga na kugawa ardhi. Taasisi za Ardhi zimeanza rasmi kutumia mipango Shirikishi katika kupanga na kushauriana katika upimaji na pia ikiwezekana Wilaya zitahusishwa katika ugawaji. Hivyo, suala la ardhi litakuwa la uwazi kabisa ili kuondoa manunguniko yasiyo ya lazima hii kazi tutaifanya. Ametaka kujua kwa nini wazee wa Mahakama ya Ardhi wamechelewa kulipwa posho zao kwa miezi mitano sasa.

Mhe. Naibu Spika, ikumbukwe kuwa katika mwezi wa Julai mwaka jana, serikali iliongeza Mahakimu kutoka watatu hadi watano hii ilisababisha vile vile kuongeza wazee wa Mahakama kutoka 6 hadi 17 kwa upande wa Unguja. Ongezeko hili la wazee wa Mahakama kwa upande wa Unguja pamoja na ufinyu wa fedha tunazozipata kutoka Serikalini, ndio sababu inayosababaisha wazee hao kuchelewa kulipwa posho zao.Hata hivyo, kwa mwaka huu wa fedha tayari bajeti hii imelizingatia ongezeko hilo na mara tu Wizara itakapopata fedha kutoka Serikalini wazee hao watalipwa posho zao zote wanadai fedha na tutawalipa. Nasema *within three months* tu pengine tutakuwa tushawalipa pesa zao zote, hatutaki tuendelee kudaiwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Nassor Jazira, ameeleza kuhusu hatua zilizochukua kwa wawekezaji waliochukuwa maeneo kwa muda mrefu ambayo tayari nimeshalijibu.

Halafu kuna Mhe. Mohammed Haji Khalid, mikataba inasemaje au sheria zinasemaje iwapo Muekezaji atafutiwa kumaliza mkataba wake?

Mhe. Naibu Spika, Sheria ya Haki ya Matumizi ya Ardhi nambari 12/1992, pamoja na mikataba ya ukodishwaji wa Ardhi imetambua kwamba mwekezaji atakapofutiwa mkataba, ardhi hiyo inarudi Serikalini moja kwa moja. Pia, Sheria na Mikataba ya ukodishwaji wa ardhi inaruhusu kuingia mkataba mpya iwapo mkataba wa mwanzo unamalizika mwaka mmoja kabla ya kumaliza muda wake. Iwapo atapendelea na kutakuwa na Makubaliano baina ya serikali na mwekezaji huo.Aidha, kuhusiana na idadi ya miradi iliyokodiswa ardhi hapa nchini kwa wageni na wenyeji ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, jumla ya miradi ni 700 kwa sasa, ambapo 511 imekodishwa kwa wageni na 189 kwa wazalendo. Hili ni suala la Mhe. Fatma Mbarouk Said, Sheria zitekelezwe na sheria zisizo Kanuni zitungiwe na pia "*awareness*" huyu ndie alieandikwa Fatma Mohammed Ali, samahani Mhe. Fatma wewe ndie Fatma Mbarouk Said. Kwa hivyo, hapa kuna suala lako nimeliona na nimekumbuka kwa ile *nature* ya suala lako.

Mhe. Naibu Spika, mnamo mwezi wa Aprili na Mei mwaka 2014, Wizara ilimuajiri mshauri mwelekezo wa kusaidia kuziweka sawa sheria za ardhi. Sambamba na mapitio ya sheria tumeandaa Kanuni kwa sheria zote za ardhi ikiwemo sheria ya umiliki wa ardhi namba 12/1992. Hali kadhalika mpango mkakati umeandaliwa wa kuelimisha wananchi juu ya sheria ya ardhi. Hili ni jukumu letu na tutaendelea nalo.

Mhe. Naibu Spika, Ujenzi wa Jeti, Wizara imeanza hatua ya kuingia suala la Jeti kwenye sheria za ardhi ili kuwe na muongozo thabiti wa kusimamia masuala ya Jeti. Aidha Wizara itaandaa Kanuni za kusaidia utekelezaji wa sheria hio ya na kusimamia masuala yahusuyo Jeti.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza, kuhusu hati miliki ya miradi ya wananchi ya Jimbo la Kwamtipura. Idara ya Mipango Miji na vijiji inayafanyia mapitio maeneo yote aliyoyataja Mhe. Hamza, yaliyokusudiwa kuwa ni ya miradi ya wananchi. Baada ya hapo, michoro ya mapendekezo ya "*land use Plan'* yatakabidhiwa Idara ya Upimaji na Ramani ili kupata *"Site Plans"* ambazo ni viambatanisho muhimu sana katika kutengeneza hati za matumizi ya ardhi *(Certificate of Right of Occupancy*). Tunategemea kwamba hatua hizo zikikamilika, Mheshimiwa Atapata Hati zote zinazohusu miradi ndani ya Jimbo lake, maana yake tuiweke. Siku hizi unajua utaratibu Mhe. Hamza, ni *computerize*, kila kitu lazima kikae vizuri, asije akatokea mjanja mmoja akasema hapa ni pangu, hii Hospitali umeijenga kwa katika ardhi yangu, lakini tukiiweka vizuri na tukitoa na *sight plan* na kila kitu pale, basi hawezi akatokea akasema hapa ni pangu hata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Omar Ali Shehe, alisema kuzingatia udogo wa ardhi yetu, Mheshimiwa aliipongeza Wizara katika juhudi zake za kutengeneza Mipango ya Matumizi ya ardhi, anaiomba Wizara kuharakisha utayarishaji wa mipango hiyo.Wizara yangu inamuahidi Mhe. Omar Ali Shehe, kuwa ifikapo mwishoni mwa mwaka huu, Mpango Mkuu wa Matumizi ya Zanzibar utakuwa umekamilika. Sambamba na hilo, Wizara tayari imeshaanza kutengeneza Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Mikoa yote Mitano ya Zanzibar. Lengo letu ni kuwa ifikapo mwaka 2015, mikoa yote mitano iwe na mipango yake ya utumiaji bora na endelevu. Nadhani pengine kuanzia kwenye mwezi wa Septemba mtaanza kuona hawa maofisa wa mipango miji wanapita sasa katika maneo kwa kutoa taaluma kuelewesha hiyo, mipango yenyewe iko vipi ili waweze kuijua. Kwa sababu hatuwezi kwenda kuvamia maeneo tu tukasema aaa hapa tushapanga tujengeni, lazima kwanza itanguliwe na elimu itolewe.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salma Bilal, anasema lini hasa kazi za mipango miji zitakamilika ili kuondosha hali liyopo hivi sasa. Serikali kwa kuona umuhimu wa mipango bora ya miji yetu, imeamua kuunda taasisi hii ya kupanga miji ili kuondoa kero nyingi zinazosababishwa na ujenzi holela. Wizara kwa kupitia Idara imeshaanza kutengeneza Mpango ya Kitaifa, Mipango kwa Mikoa yote Mitano ya Zanzibar na Mipango ya miji midogo midogo. Mipango mitatu ifuatayo, yaani, Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi Zanzibar, *(Zanzibar National Land Use)*, Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Mji wa Zanzibar *(Zanzibar Master Plan)* na Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, yote hii itamlizika ndani ya mwaka huu 2014. Mipango ya matumizi ya ardhi ya mikoa minne iliyobakia itamalizika mwakani 2015.

Mhe. Naibu Spika, Mhe.Mohammed Haji Khalid, anasema watu wanaendelea kujenga kiholela sehemu mbali mbali; Idara ya Mipango Miji isisubiri mpaka watu wajenge na wahamie ndiyo iwavunjie. Mheshimiwa anashauri Idara

iwazuie watu hao wakati wanapoanza ujenzi na iwakataze kujenga sehemu zisizokubaliwa, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanafuata taratibu zote za ujenzi na kuepusha uvujanji. Kama nilivyotangulia kueleza hapo awali; Wizara kwa kupitia Idara Mipango Miji, imetayarisha Kanuni mpya za kusimamia suala la ujenzi. Ndani ya Kanuni hizi utaratibu wa ujenzi utarahisishwa na utasimamiwa na taassisi moja chini ya uongozi wa Mkuu wa Mkoa. Ni Imani yangu kuwa chini ya utaratibu huu tatizo la uvunjaji halitakuwepo. Hata hivyo, Wizara inapenda kuweka wazi kuwa mwananchi yeyote atakae livamia eneo la serikali bila ya kibali, Wizara itamtaka aondoke. Akishindwa kufanya hivyo, Wizara itamchukulika hatua na ikilazimika itamvunjia.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Fatma Mbarouk Said, anasema mipango yetu ya miji si mizuri, mfano *Airport* yetu iko karibu sana na sehemu za makaazi. Kwenye makaazi yenyewe, ujenzi wa nyumba na barabara hauko vizuri. Aidha, lini ile barabara inayotoka njia ya Amani (Uwanja wa demekrasia) kuelekea Mwembenjugu itajengwa.

Mhe. Naibu Spika, nasema kama Zanzibar ina mipango Miji mizuri ya maendeleo ya miji yake, lakini ni kweli kuwa kwa kipindi kirefu utekelezaji wa mipango hiyo umekuwa mdogo sana. Hata hivyo, serikali umekusudia kuondoa kabisa kasaro hizo.Wizara yangu kwa kupitia Idara ya Mipango Miji, imekusudia kuweka mipango ya Mikao yote mitano ya Zanzibar, ambayo nimeshajibu kue mwanzo. Aidha, miji yote mikubwa na midogo nayo itakuwa na mipango yake. Ili kuondosha kasoro za utekeleza,Wizara yangu kwa kushirikia na Wizara inayosimamia Serikali za Mitaa, tutaweka mfumo mpya wa usimamizi na utekelzaji wa mipango yetu. Kazi hii itaanza ndani ya mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika, ama kuhusu ujenzi wa Bararaba inayotoka njia ya Amani (Uwanja wa Demokrasia) kwenda Mwembenjugu, azma ya serikali bado iko pale pale. Serikali kwa kupitia Wizara ya Miundo Mbinu, tayari imeshaanza kujenga barabara za mijini. Ni Imani yangu kuwa barabara hii nayo itajengwa mara tuu, Serikali itakapopata uwezo wa kufanya hivyo. Ama kuhusu ujenzi wa kituo cha polisi, Serikali kwa kupitia Wizara yangu, suala hili tayari imeshalifanyia kazi na eneo mbadala tayati lipo. Nadhani Mhe. Fatma, hebu fuatilia pengine eneo hukulipenda au vipi, lakini ninafikiri tuzidi kushauriana katika suala hili, kwa sababu nimegundua kwamba unalalamika kwa muda mrefu sana juu ya suala hili. Tangu sijaja mimi kwenye Wizara nimekuta unalalamika juu ya kituo hicho. Kwanza kalitizame lile eneo mbadala kama hukulipenda rudi nieleze mimi, ndio mwanasiasa mwenzio. Sasa sisi inatubidi wakati mwengine tufanye uamuzi. Kwa hivyo, ni vizuri katizame hilo eneo kama hukulipenda njoo tuzungumze tutizame tunafanya utaratibu gani.

Mhe. Naibu Spika, Mhe Asha Bakari, *plans* za miji yetu zifanywe vizuri. Mji hauna mpangilio mzuri hasa nyumba zake. Hata *Airport* yetu, ambayo ni kiyoo cha nchi, nayo haikukaa pahala pazuri. Ni kweli kabisa kuwa suala la upangaji miji na utekelezaji wake limekuwa ni changamoto kubwa. Hata hivyo, napenda kumuhakikishia Mhe. Bi Asha, kuwa Wizara tayari imeshachukua hatua za kuweka taratibu mpya za suala zima la mipango miji na vijiji. Ndani ya mwaka huu, Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi utakamilika, *Master plan* ya Mji wa Zanzibar nayo itakamilika na mipango ya mikoa nayo itaanza. Mipango hiyo itaweka bayana matumizi ya shughuli zote, makaazi, uekezaji, huduma, maeneo ya wazi na maeneo ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara inakubalina na Mheshimiwa kuwa kupanga ni kuchagua na tukitaka uzuri lazima tudhurike. Wizara imekusudia kupanga upya miji yote ya Zanzibar ili nchi hii iwe na miji yenye haiba na mizuri zaidi kuliko leo. Zaidi katika kupanga Mipango ya kimikoa, Wizara yangu kwa kupitia Idara ya Mipango Miji inafanya "*survey*" kujua hali halisi ya maeneo hao kabla ya kuyapanga. Hapa nataka kukumbusha kitu kimoja, kupanga mji ni gharama na wakati mwengine mnalazimika kuchukua hatua ngumu ili muweze kuupanga mji, mfano mzuri ametuonesha Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Mzee Abeid Amani Karume alipotaka kujenga majumba ya Michenzani palikuwa na nyumba pale na watu walikuwa wakiishi mle ndani, lakini aliamua kwamba hata tunataka tujenge nyumba za kisasa na barabara pana na uamuzi ule atautia kwenye vitendo wale walioko pale aliwahamisha, aliopata mahala pa kuwabanza akawapeleka wakajibanza na baadae akawarudia kwa kuwalipa zile nyumba zao katika maeneo yale ya Michenzani.

Mhe. Naibu Spika, ndio leo Michenzani tunapaona vile hapakuwa na uwanda na wala hapakuwa na pori ila palikuwa pana nyumba pale, zimepangana zimekaa pacha pacha kweli kweli, lakini wale wote sasa hivi wameingia mle. Ninashukuru sana kwamba na Mhe. Rais wa awamu ya sita nae alipokuja akaona kumebakia madeni machache akamliza jumba lile namba kumi na akawaingiza waliobakia katika jumba lile. Kwa hivyo, tufikirie kwamba madam tunazungumzia *master plan* tusifikiri kwamba tutakwenda katika uwanda, tutafanya humu humu tunamoishi, tutapanga miji vizuri, tutafanya kazi vizuri hatutawabughudhi watu, lakini tutawaomba wastahmili kwa sababu

tusichukuwe hatua ngumu ili kuujenga mji na ndio miji yote duniani inavyojengwa.Miji yote ndivyo inavyojengwa ukiikuta leo imebadilika ni kwa sababu mnachukua hatua halafu mnafanya uamuzi mgumu mnajenga mle nyumba za kisasa.

Mhe. Naibu Spika, Mji wetu una matatizo hauna *parking*, unafikiria kwamba nafasi ya wazi ndio *parking*, hapana. Watu leo katika miji wale wanaofanya biashara na *private sectors* kama wapo waje wachukue kazi hii, mradi huu unanunua nyumba zako tano, sita unawalipa wenye nyumba unajenga pale nyumba ya ghorofa tatu, nne tano, ni *parking* watu wanaweka magari katika jengo lile na tunaona mambo haya. Kwa hivyo, wale *private sectors* nao wajaribu kuona hivyo, miradi hii ipo. Unanunua nyumba zako tano, sita unazivunja, madam unaambiwa hapa unaweza kutumia kwa *parking*, unajenga jengo la ghorofa nne, tano, sita, gari zinapanda juu zinakwenda.

Mhe. Naibu Spika, gari inakaa ghorofa ya sita juu huko, hata hapo Dar-es-Salaam utakuta majumba yameshafanywa namna kama hiyo. Tuwe *serious* katika kufanya kazi hizi, miradi hii ipo na kwa kweli ukijenga miradi hii utapata *parking* nzuri badala ya sasa hivi tunabanana, tunaumizana, tunahangaika. Mara leo Darajani, mara leo twendeni kwa binti Hamrani, mara twendeni wapi. Hebu wawekezaji *private factors* wachukuwe hatua wawahi mradi huu una fedha nje nje kabisa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, anasema Mhe. Waziri, afafanue ni vipi itatekeleza mipango ya matumizi ya ardhi ya Zanzibar. Aidha, jinsi gani Wizara itajipanga kuhakikisha wananchi hawajengi maeneo yasiotakiwa. Je, suala la ujenzi wa nyumba za ghorofa, Wizara imejipanga vipi?

Mhe. Naibu Spika, niungane na Mhe. Mahmoud na kukiri kuwa ni kweli utekelezaji wa mipango yetu haujawa mzuri, ndiyo maana bado watu wanajenga katika maeneo yasiyofaa kujengwa. Kwanza naomba nisisitize kuwa katika suala la mipango miji serikali imekuja na mikakati mipya kabisa. Ukiachia mbali ule mpango wa matumizi ya ardhi ya nchi nzima *(National Land Use),* kuanzia mwaka huu, kwa mara ya kwanza kabisa, Mikoa yote ya Unguja na Pemba itakuwa na ramani za matumizi ya ardhi. Lengo letu ni kuwa ikifika mwaka 2015, mipango ya mikoa yote mitano iwe imeshakamilika.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya Mipango hii, miji yote mikubwa na midogo nayo itakuwa na ramani za kina za kuonesha maendeleo ya miji hiyo. Zaidi, ili kuhakikisha utekelezaji wa mipango hii, Wizara inakusudia kuwa na mifumo mipya, mwepesi wa ujenzi katika miji yetu. Kufanya hivyo sio tu kutaondoa kero kwa wananchi, bali pia kutapelekea kupunguza ujenzi holela.

Mhe. Naibu Spika, aidha, kuhusu suala la ujenzi wa nyumba za ghorofa maeneo ya Mijini, Serikali na Wizara inalifanyia kazi suala hili. Wizara imeshaanza *"pilot project"* kuona jinsi gani itawasaidia wananchi katika ujenzi wa nyumba za ghorofa. Kwani Wizara inaamini kuwa suala hili linahitaji umakini ili lisilete matatizo amabayo tutanyaona leo hata katika eneo la kariakoo, Dar-es-Salaam.

Mhe. Naibu Spika, ili kuepusha hayo, Wizara kwa kupitia Idara ya Mipango Miji, imeanzisha *projet* ya Ng'ambo Tuitakayo, katika eneo la kisimamajongoo kuonesha jinsi gani suala hili linaweza kufanyika, kwa ujuzi zaidi. Mwezi wa pili mwaka huu tulikutana na wananchi wa eneo hili, kuongea nao na kupata fikra zao juu ya suala hili. Nachukua furasa hii, kumualika rasmi Mhe. Mahmoud katika maonesho ya awali ya kazi tuliyoifanya katika sehemu ya Kisimamajongoo, ndani ya wiki hii, katika eneo la Kisimajongoo tutakapokwenda kuwaonesha wananchi. Lengo letu ni kuhakikisha ujenzi wetu sasa unakuwa ni wa ghorofa katika maeneo yote ya mjini. Hili ndio nililosema mwanzo kwamba kama tunataka kujenga nchi Mhe. Hamza, Kwamtipura ibadilike, sio tukae na nyumba zile huyu kateremka kikono kauza duka, huyu kateremka nini pabadilike pale, ndivyo tutavyofanya.

Mhe. Naibu Spika, hoja kuhusu uhusiano wa *COSTEC* na masuala ya *Research* za Wizara, jibu ni kwamba hii na taasisi ya Sayansi inayoshughulika na masuala ya utafiti Tanzania. Taasisi hii kupitia Tume ya Mipango Zanzibar imeshirikiana na Wizara zetu kwa kuandaa *Research Agenda*.Taasisi hii inayo fursa ya kupata fedha kwa ajili ya masuala ya utafiti kupitia kwa wafadhili mbali mbali na wana nafasi ya kuitumia fursa hiyo kwa kutangaza kazi za utafiti kwa maeneo mbali mbali yatakayoweza kuainishwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Panya Ali Abdalla, wizara iyapime maeneo kabla hayajavamiwa. Aidha, wizara ifanye jitihada kulilinda eneo la Fukuchani. Wizara imepokea fikra za Mhe. Panya. Aidha, wizara kwa kupitia Idara ya Mipango Miji tayari imeshaanza kupanga matumizi ya ardhi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja. Ndani ya kazi hii maeneo yote ya Mkoa huu yatapangwa na eneo la Fukuchani nalo litapangiwa matumizi mazuri na kulindwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, wizara ipange mipango mizuri na kuainisha maeneo ya kilimo na yale ya makaazi ili wananchi wasijenge katika maeneo ya mabonde. Wizara tayari imo katika kukamilisha mipango ya matumizi ya ardhi ya Mikoa yote na miji kama nilivyojibu. Mipango hiyo itabainisha wazi matumizi bora ya Mikoa hiyo na kuonesha maeneo yote yasiyofaa kujengwa. Aidha, utekelezaji wa mipango hii nayo itafanywa upya na kufanya sheria za ujenzi, ili uwe rahisi utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, anasema Mhe Waziri, atueleze jinsi gani *Master Plan* yetu mpya itatekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa mwaka 1982, Serikali kwa kushirikia na wataalam wa China ilitengeza *Master Plan* ya Mji wa Zanzibar. Ni ukweli kuwa kwa kiasi fulani mpango ule haukutekelezwa wote. Kwanza naomba nieleza kuwa utengenezaji wa *Master Plan* ni suala endelevu. Hata kama *Master plan* ya mwaka 1982 tungeitekeleza yote, kwa asilimia mia, bado tunahitaji *Master Plan* mpya, hivi sasa. Hivyo, kazi tunayoifanya kwa sasa ni inayohitajika ili kuondosha changamoto zilizopita.

Mhe. Naibu Spika, aidha, sambamba na suala la utengenezaji wa *Master Plan,* wizara imetengenza Kanuni mpya za usimamizi wa maendeleo ya Mji wa Zanzibar. Mpango huu mpya una lengo la kurahisisha utekelzaji wa *Master Plan* mpya. Zaidi suala la utekelezaji wa mpango huu mpya halitegemei serikali peke yake. Kwa kutumia mfumo wa *PPP,* Serikali itatumia uwezo wake kuwakaribisha wahusika wengie na wawekezaji wengine ili kurahisisha utekelezaji wa *Master Plan* mpya.Hapa pia ndio linakuja lile suala la Mhe. Hamza, alilosema kwamba wako watu hasa tayari wanataka kushiriki katika masuala hayo ya *PPP*, sisi tunasema ni ruhusa waje tuwaelekeze nini wafanye wajenge.

Mhe. Naibu spika, nikisema hivi haina maana kwamba serikali ndio itaujenga mji wa Zanzibar na miji mengine, hapana. Wananchi ndio wataujenga mji huu kwa kufuata maelekezo ya serikali, ndio watakaojenga mji huu wenye uwezo kwa mashirikiano na watu mbali mbali. Vile vile, serikali itashirikiana na mpango wa *PPP* na watu wengine ambao najua sasa hivi sera yake na sheria zinatayarishwa *consultancy,* yuko tayari inafanya kazi hiyo yakuona kiasi gani *PPP* itafanya kazi katika masuala hayo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, anasema ukodishwaji wa ardhi, kwa nini skuli zikodishiwe ardhi?

Mhe. Naibu Spika, Taasisi ya Elimu imekusudiwa kujenga chuo kikuu, mradi huo uko katika Kijiji cha Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja na wekezaji wake ni Kampuni ya *VIGOR* inayomilikiwa na mzalendo, hii ni *private company,* sio ya serikali. Sasa wewe ukijenga *private company,* madhali una mradi pale, sisi tunataka ulipe kodi. Kwa hivyo, utafanya biashara pale na ikiwa unawalipisha watu pesa, wanakuja kusoma, utafanya biashara. Kwa hiyo, ulipe.

Mhe. Naibu Spika, Ugawaji wa ardhi ya Mziwanda, Mhe. Bikame anahisi wananchi wa Mziwanda wameondoshwa kwenye ardhi yao asilia ya kilimo. Mwananchi aliyepewa eneo hilo ni Mzanzibari, Sheria ya Ardhi inaruhusu kutoa ardhi katika Kisiwa chochote Unguja na Pemba. Aidha, mwananchi huyo alifuata taratibu za upewaji wa ardhi ya kilimo. Hata mwenyewe Mhe. Bikame, alisema hivyo kwamba ile ardhi imetolewa, lakini nasema katika hati ya matumizi ya ardhi imeandikwa matumizi ya ardhi ni namna gani, inaandikwa mle na hatakiwi mtu abadilishe. Kwa hivyo, mimi nikwambie tu Mhe. Bikame, nadhani hii hati nimejaribu kuiuliza tangu juzi niione ili nijue imeandikwa kwa kitu gani ili niweze kuifanya hii kazi.

Mhe. Naibu Spika, hii kazi lazima niione, ile hati ya asili imeeleza ardhi hii itumike, kwa nini, halafu kama hapatumiki ni suala la kuirejesha serikali ni lazima, kwa sababu tangu hapo ardhi yenyewe ilikuwa ya serikali ilikuwa ni ya Wizara ya Kilimo ile. Kwa hivyo, kuirejeshea serikali itakuwa ni lazima, lakini nipe nafasi niitafute hii hati niipate imeandikwaje, kwa sababu hati zenu zote mlizopewa za ardhi mkitizama mna madhumuni ya hiyo ardhi

mliyopewa imeandikwa mle. Ukiisoma vizuri mna madhumuni na ukibadilisha matumizi, basi akitokea mtu akisema huyu kapewa ardhi kwa jambo fulani na ametumia kwa jambo fulani, basi inakuwa ushaingia makosani.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Haji Khalid, muda wa ukodishaji wa ardhi umegawika vipi, wazalendo ni wangapi? Hii nimeshatoa hesabu kule nyuma.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, kuna mkanganyiko juu ya nani au taasisi gani inajukumu la kugawa na kutoa ardhi.

Mhe. Naibu Spika, Sheria ya Ardhi, Nambari 12/1992, jukumu la kusimamia na kugawa ardhi ya Zanzibar limepewa kwa Mhe. Waziri, mwenye dhamana ya ardhi. Masheha, Madiwani na viongozi wengine hawana jukumu hilo kisheria, kama wanafanya hivyo ni uvunjifu wa Sheria ya Umiliki ya Ardhi Nambari 12/1992.

Mhe. Naibu Spika, narudi tena kwa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Teule umefikia wapi?

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti, wizara imeanza kuchukua hatua madhubuti katika maeneo mbali mbali yaliyoguswa na Kamati kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na *ZRB, ZIPA, Tourism Commission* na Sekta ya Ardhi imeandaa *Data base* ambayo taarifa zake zitatumika na serikali kwenye mfumo wa uwekezaji na ukusanyaji wa mapato. Kwa kuwa kazi hii ilidhaminiwa na *Mradi wa SMOLE*, kwa sasa SMZ imejiandaa kikamilifu kuchukua dhamana hii, kazi hii itaendelezwa kwa nguvu za serikali kupitia "*Internal Financing*".

Mhe. Naibu Spika, kuna maeneo 12 ambayo yameshafanyiwa au yanaendelea na hatua za utambuzi. Maeneo hayo ni Mji Mkongwe, N'gambo, Jan'gombe, Paje, Chawaka, Nungwi, Jendele, Limbani, Wara Kiungoni, Chokocho na Mkoroshoni.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu dhana ya ardhi, ni mali ya serikali. Hivyo, serikali kupitia wizara yangu imo katika mpango madhubuti wa kuelimisha wananchi juu ya dhana hiyo. Baadhi ya mbinu zinazotumika ni semina katika ngazi mbali mbali za viongozi na wananchi. Pia, tumeanzisha JARIDA LA ARDHI kama sehemu za juhudi hizo. *Radio,* vipeperushi, *TV* na maigizo, vikundi vya wasanii navyo hutumika.

Mhe. Naibu Spika, uanzishwaji wa *Data base* ya Ardhi. Kutokana na kuanzishwa kwa *Data base* ya Ardhi, wizara inakusudia kuweka bayana taarifa hizo ili wananchi na wawekezaji waweze kuzipata na kuzitumia kwa uwazi. *Zanzibar Land Information System (ZALIS)* ni programu ya taarifa za ardhi inayoendeshwa chini ya Mradi wa *SMOLE*, ikiwa na madhumuni hayo hayo ya kuelimisha wananchi juu ya taarifa za ardhi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, umakini na kufuata sheria katika kufuta hati, kufuatia mapendekezo ya Kamati Teule, wizara imeanza kuwa makini sana juu ya matakwa ya sheria katika suala la ufutaji wa Hati za *LAND LEASE AGREEMENT*. Kama nilivyoahidi wakati wa vikao vya Kamati ya mawasiliano na ujenzi, tutatekeleza mpango wa kutoa elimu ya masuala ya ardhi na hasa sheria zake kwa Waheshimiwa Wajumbe wote. Hata hivyo, suala hili linakwazwa na uwezo wa kifedha.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, hapa nina daftari ambalo lina sheria za ardhi ambazo zinapitiwa, sasa kama ulivyopendekeza Kamati ile ya masuala ya ardhi, ndio maana hili daftari lipo na linapitiwa tumeligawa katika maeneo mbali mbali wanazipitia sheria zile za ardhi ili zikae vizuri kupunguza haya matatizo ya kuhodhi ardhi bure, ndio maana yake.

Mhe. Naibu Spika, umezungumza suala la kutafuta jengo jengine Ofisi ya Mrajis wa Ardhi. Jengo la Ofisi ya Mrajis wa Ardhi, serikali tayari imeliona hilo na sasa Ofisi hiyo inatafutiwa jengo mbadala badala ya hii tuihamishe pale ili ikae mahala pazuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salma Mussa Bilali, tunamshukuru kwa kutupongeza Mahakama ya Ardhi kwa kuwa lengo la kuamu kesi kwa asilimia 179. Vile vile, Mhe. Salma, ameomba ujenzi wa Mahakama ya Koani ukamilike ili

Mahakama hiyo ianze kazi pamoja na upatikanaji wa usafiri kwa kuweza kufika kwa urahisi kwenye sehemu za migogoro.Wizara inapenda kumuhakikishi Mhe. Salma, kwamba Mahakama ya Koani imebakia kazi ndogo za kumalizia na tunategemea katika mwaka huu wa fedha Mahakama hiyo kuanza kazi.

Mhe. Naibu Spika, narudi kwa Mhe. Mohammed Haji Khalid, anataka kupata ufafanuzi, kwa nini idadi ya kesi zilizopokelewa Unguja na Pemba ni kidogo kuliko zote zilizotolewa hukumu? Je, hizi nyengine zimetolewa wapi?

Mhe. Naibu Spika, vile vile, Mhe. Mohammed, alitaka kujua, kwa nini idadi ya wazee wa Mahakama walioongezwa kwa upande wa Pemba ni kidogo kuliko wale walioongezwa Unguja?

Mhe. Naibu Spika, lengo la Mahakama ni kuwa na wazee wa Mahakama watatu kwa kila Wilaya na kufanya wazee 18 kwa Unguja na 12 kwa Pemba. Hata hivyo, kwa bahati mbaya mzee mmoja kwa upande wa Unguja amefariki dunia na wazee 3 wameomba kupumzika kutokana na hali ya afya zao kwa upande wa Pemba. Aidha, idadi ya kesi zilizopo Pemba ni kidogo kuliko zile zilizopo Unguja.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, ametaka kujua, je, baada ya marekebisho yaliyofanywa ya Sheria ya Mahakama ya Ardhi ya kila Mkoa kuwa na Hakimu mmoja? Je, Hakimu huyo yupo kwa kila Mkoa?

Mhe. Naibu Spika, mabadiliko ya sheria yaliyofanywa, lengo lake ni kuwezesha kila Mkoa kuwa na Mahakama ya Ardhi ili kusogeza huduma hizo karibu na wananchi. Kwa upande wa Pemba tayari Mahakama hizo zimeshafunguliwa na kuanza kazi na kwa upande wa Unguja tayari majengo ya Mahakama yameshapatikana hapo Gamba Kaskazini Unguja na Koani Kusini Unguja na baada ya matengenezo Mahakama hizi zitaanza kazi. Vile vile, Mhe. Amina, alitaka kujua tathmini ya mwenendo wa kesi baada ya ongezeko la Mahakimu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuongezwa Mahakimu, mwenendo wa kesi umebadilika na kasi ya usikilizaji wa kesi imeongezeka, hapo mwanzo kesi moja ilikuwa ikitajwa mara moja baada ya miezi mitatu ambapo kwa sasa kesi moja huitwa tena kila baada ya wiki mbili au tatu na hii hupelekea kesi hizo kuamuliwa mapema zaidi tofauti na hapo mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Mawasiliano ilikuwa na hoja nyengine hapa Kamati inaamini kuwa kuongezeka kwa viwango vya kodi kutaongeza ukusanyaji wa mapato. Ni kweli kuwa kuongezeka kwa viwango vya kodi kutapelekea mapato yatokanayo na kodi za nyumba za serikali kuongezeka na mafanikio hayo tayari yameshaanza kuonekana katika makusanyo ya mwaka huu unaoishia ambapo hadi Machi, 2014 shilingi 316,136,000/- tayari zimekusanywa kama ni kodi. Lengo la serikali ni kuona kuwa wananchi wa visiwa hivi wanaishi katika makaazi yalio bora.Kamati inapendekeza ukarabati wa jengo la Kengeja upewe umuhimu.

Mhe. Naibu Spika, ukarabati wa jengo la Kengeja bado umepewa umuhimu mkubwa na wizara yangu itafanya jitihada ili fedha za matengenezo zipatikane ili jengo lianze kufanyiwa matengenezo. Ni kwa nini hakuna maongezeko ya mapato katika Kiwanda cha *Furniture* cha Saateni?

Mhe. Naibu Spika, Kiwanda cha *Furniture* cha Saateni hapo miaka ya nyuma kilikuwa kikiingiza mapato mazuri serikalini kutokana na kazi za hapo kiwandani na sababu kubwa ya kushuka mapato hayo ni kutokana na uchakavu wa mashine zake ambazo hizo mashine nyingi ni za zamani sana hata upatikanaji wa vipuri vyake kwa kuzifanya matengenezo havipatikani na kupelekea baadhi ya mashine hizo kuuzwa. Sababu nyengine ni ongezeko la viwanda vya aina hiyo vya watu binafsi ambao wameunga mashine mpya za kileo na kupelekea wateja wetu wengi kupeleka kazi zao huko. Sababu nyengine ni kukosa kazi zinazotoka Taasisi za Serikali ambazo hapo nyuma taasisi hizo zilikuwa zikileta kazi zake za kutengenezewa hapo katika kiwanda. Kwa nini hakuna maongezeko ya mapato katika viwanda vya kokoto?

Mhe. Naibu Spika, kupungua kwa mapato kwa upande wa Kiwanda cha Kokoto kunatokana na Idara ya Ujenzi kumiliki kiwanda kimoja kiliopo Makunduchi Wilaya ya Kusini Unguja, mashine hiyo ni ya zamani sana ambayo inaendea *diesel*, uzalishaji wake ni mdogo hauwezi kukidhi malengo ya kibiashara. Mashine hiyo ni miongoni mwa mashine nyingi zilizoletwa nchini wakati wa ujenzi wa nyumba za maendeleo ulipoanzishwa katika wakati wa uhai wake Mhe. Rais wa kwanza wa Zanzibar (Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, narudi tena kwako na suala la kuhusu nyumba nyingi zinazokaliwa na Viongozi Wastaafu, bado hazijarejeshwa serikalini. Nafikiri hata Mhe. Mahmoud nae alizungumza hili.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa baadhi ya nyumba za serikali zilizokuwa zinatumiwa na viongozi wa serikali ambao sasa ni wastaafu hazijarejeshwa serikalini. Jitihada kubwa imefanywa kuwasiliana na viongozi hawa ili wazirejeshe nyumba hizo serikalini na baadhi yao wameanza kurejesha na wengine bado hawajazirejesha. Hapa nilikuwa nina orodha ya nyumba hizo ambazo niliambiwa nizitaje ni ngapi na zinatumika vipi.

Mhe. Naibu Spika, orodha ilikuwa imezitaja nyumba zote hizi na zimefanyiwa kazi kila mahala zilipo, mpaka sasa nyumba ambazo zina matatizo kama hayo ni moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja na kumi na mbili. Kuna namba X7 iko Mazizini ambayo ina mgogoro aliyekuwa anakaa katika nyumba hii anasema kachukua *lease*. Kwa hivyo, wizara tunaifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, kuna nyumba nyengine namba 24 102/23, hii alipelekewa barua ya kwamba atoke katika nyumba tarehe 30/06/2011 ili nyumba hiyo irejee serikalini kwa matumizi ya viongozi. Ameandika barua ya kukubali kuhama na ameomba apewe muda wa miezi sita ili aweze kuhama katika nyumba hiyo, lakini miezi imekwisha na bado hayatoka. Kwa hiyo, mimi namuomba tu huyo anayekaa katika nyumba Nam. 24 102/23 ahame, tusije kumuadhiri kwa kumtoa kwa askari, si vizuri kusema kweli.

Mhe. Naibu Spika, kuna nyumba Nam. 24 102/26, huyu ameshahama hamna mtu, lakini ni mbovu inahitaji matengenezo nayo pia iko Mazizini. Pia, kuna Nam. 24 02/27, hii tumefanya mazungumzo na mtu aliyeihodhi amekubali kwamba atahama, lakini bado hajahama, namuomba aliyekuwa katika nyumba hii Nam.24 02/27, nae bora atupishe, si vizuri kungojea kusukumana sukumana.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kuna Nam. 24 102/27, huyu amepewa barua tarehe 30/06/2010 amesema hajajipanga vizuri. Hata hivyo, Idara tarehe 02/09/2011, Idara imeandika barua ya kumbukumbu na kumwita tena ili kumpa msisitizo kuhusu suala la kuhama katika nyumba hiyo hadi sasa bado hajahama wana ukaidi wa namna yake, namuomba bora angetoka ili tusije kuchukua hatua, maana mimi tukiambiwa tuchukue hatua tutachukua hapa, halafu wasije kulalamika wakasema mtu ananyanyaswa, hanyanyaswi mtu, mtu anayekaa ndani ya nyumba ya serikali alikaa nayo kwa wadhifa fulani na wadhifa umeondoka atoke na airejeshe serikalini.

Mhe. Naibu Spika, bado kuna Waheshimiwa wengi wanataka nyumba wengine ni Mawaziri na Manaibu Waziri sijaweza kuwapa nyumba, wengine wamekodi nyumba nje, sasa hiyo nyumba irejeshwe.

Mhe. Naibu Spika, kuna fleti nyengine vile vile, hii fleti Nam. 43, hii tutaifanyia kazi kujua kama anayekaa humu ndani ni Afisa au ni nani. Tumefanya kazi ili tuweze kujua mambo yalivyo.

Mhe. Naibu Spika, kuna nyumba Nam. 43B ni fleti, hii nayo tunaifanyia kazi, lakini huyu alifanyia matengenezo makubwa ya shilingi milioni nne (4,000,000) na kodi ya nyumba ikabidi ajifidie, lakini hata hivyo, nayo ndio ukishafidia kodi yako, ni vizuri utoke utupe nyumba yetu.Vile vile, kuna nyumba Nam. 45A, muhusika tumempa wito wa kumtaka afike ofisini na kukamilisha ulipaji wa deni, hii ina deni tu, lakini alishakodishwa kwa *lease*. Hii nyumba ya *Ecrotanal* vile vile tunaichukua moja kwa moja kwa sababu aliyemo ndani ni mlinzi wa *Ecrotanal* tutaichukua hii nyumba ya Nam. 5B.

Mhe. Naibu Spika, nimepata ki-*note* kinaniambia kwamba niwataje. Nasema kwa kuwa nimezitaja namba wenyewe wanajijua sina sababu ya kuwataja hapa watu wazima, maana wengine wamekaa juu ya viti humu humu. Kwa hiyo, sina haja kuwataja watu wazima hapa, lakini imekuja barua hapa inasema watajee! Sitawaji bwana kwa sasa hivi hawa, maana watu wazima wakati mwengine lazima umtumie busara usivamie tu mambo na nini kwa sababu unataka kufurahi, hapana, wengine wamo humu na wengine hawamo humu.

Mhe. Naibu Spika, lakini nasema hizi nyumba nazitaja nyumba Nam. KSMZ 33 hii vile vile, inaonesha kuwa bado inatumiwa na huyu anayeitumia, naye tunamuomba atupe nyumba. Ndio nazungumza hapa kwa taratibu hivyo, lakini baadae tutachukua hatua na kwa desturi yetu, sisi watu wa ardhi hatukawii kuchukua hatua. Tutachukua hatua

kwa sababu mimi sipendi tena nije hapa bajeti ijayo niendelee kutaja majina kama hivi, hata siku moja. Sitaki kuzitaja tena hizi. Hivyo, bora wajirekebishe wenyewe waondoke watupe nyumba hizi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hizo ndizo nyumba ambazo nimezitaja karibu kama kumi na zaidi ambazo moja ndio iko tupu na nyengine ndio hizo kama nilivyozitaja hapo. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, amehimiza sana kwamba watu hawa watoke katika maeneo haya. Vile vile, Mhe. Makame, alisema siku moja alikuwa juu *Roof Top* ya Hoteli ya Maru-Maru akaona jirani jengo limejengwa kwa matofali na kuweka *linter*. Hizo ndio sehemu zake Mhe. Makame Mshimba yeye *Roof Top* huko nae ndio hivyo mwanasheria wa kuzaliwa. Kwa hivyo, anapata mialiko mingi. *(Kicheko)*

Mhe. Naibu Spika, mamlaka kwa ujenzi wowote wa matofali hautowi kibali cha ruhusa.Mamlaka itaifuatilia nyumba hiyo na ikipatikana na kuthibitika kuwa kajenga kinyume na sheria hatua zitachukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Omar Ali Shehe, anasema nyumba ya serikali ni mbovu. Ni kweli nyumba ya serikali ni mbovu na jitihada zinafanywa kuzifanyia matengenezo. Pia, kuhusu uchakavu (ubovu) wa nyumba ya Chachani na anashauri ikibidi irejeshwe kwa mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, Nyumba ya Chachani Namba (T.60) ilikuwa ikimilikiwa na Bwana Taibali Ismail. Je, ilitaifishwa na serikali na kutumiwa kwa shughuli mbali mbali za kiserikali hasa katika ukumbi wa jengo hilo. Katika mwaka 2012, wizara yangu ilituma jopo la wataalamu ili kuweza kuifanyia tathmini ya maharibiko yaliyopo ili iweze kufanyiwa matengenezo na hatimae kutumika kwa baadhi ya maofisi ya serikali yaliyoko Pemba, ambayo hivi sasa yanakodi nyumba za watu binafsi. Gharama ya mategenezo iliyotolewa ni shilingi milioni mia nne na hamsini (450,000,000/=) kwa kazi za kuezeka, kujenga nguzo na milango na madirisha. Bado serikali ina nia ya kuitengeneza na kuitumia nyumba hiyo.

Mhe. Naibu Spika, lakini nasema mimi wizara yangu haijapokea barua ya huyu mhusika kwamba anaomba nyumba arejeshewe na hata ningeipokea hiyo barua, uwezo wa kurejesha mali iliyotaifishwa hauko kwa Mhe. waziri. Kwa hivyo, hata kama angeniletea barua mimi pengine ningetakiwa kutoa ushauri, lakini kwa kweli nyumba iliyokwishakutaifishwa inakuwa ni mali ya serikali, kwa sababu hati zipo na nambari yake ndio hiyo niliyoitaja T.60 kwamba hiyo nyumba imetaifishwa.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli tunahitaji gharama kubwa kuifanyia matengenezo ile nyumba pengine zaidi ya hizi zilizoandikwa hapa. Najua tu alitokea mtu mmoja akataka kuinunua hiyo nyumba na tulimfanyia tathmini ikaja kwenye shilingi 80 milioni, lakini tulipomwambia ainunue kwa shilingi 80 milioni akasema bei kubwa. Kwa hivyo, apunguziwe bei, bei haikupunguzwa, ndio maana mpaka leo bado hajaweza kuinunua. Sasa serikali imeshaamua kwamba nyumba ile ifanyiwe matengenezo, tujibane, tujivute na tuifanyie matengenezo tuitumie kwa matumizi ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, halafu jengine Mhe. Omar Ali Shehe, ameleta kasema kwa muda mrefu kulikuwa na Kamati ya Wananchi Wanaodai Kupewa Nyumba na Marehemu Mzee Karume, nataka kujua lini Ripoti ya Kamati itapatikana.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mimi nilipofika pale ofisini, nimeikuta hiyo Ripoti ya Kamati na mimi nikaiombea vikao serikalini ili ijadiliwe. Nimefanikiwa kupata vikao nikagundua kwamba yaliyoandikwa katika ile ripoti na uamuzi wa serikali ulioandikwa hapo nyuma wala sio kwa Mhe. Rais huyu aliyeko madarakani ni tafauti. Hapo nyuma kulitolewa uamuzi na serikali juu ya nyumba ya watu wake, lakini yaliyoandikwa mle na yaliyoandikwa na ripoti ilikuwa ni tofauti. Uamuzi wa serikali ulikuwa kwamba mtu yeyote aliyepewa nyumba na Marehemu Mzee Karume aendelee kukaa katika nyumba hiyo, lakini akae uhai wake, ndivyo ulivyo uamuzi wa serikali. Mwenyezi Mungu akimuhitaji wanaofuatia itabidi nyumba ile waikodi, lakini yule akae maisha yake kwa sababu ndio keshapewa na Mzee Karume.

Mhe. Naibu Spika, uamuzi huu nafikiri una msingi wake, nyumba zilizotolewa na Marehemu Mzee Karume nyingi sana sio hizi tunazozungumza peke yake, nyumba zote za maendeleo za Mtemani zilitolewa na Mzee Karume wakati huo, nyumba zote za maendeleo za Kengeja zilitolewa wakati huo na serikali bure, nyumba zote za Chake Chake zilitolewa wakati huo na Mzee Karume bure, nyumba zote za Mkoani zilitolewa wakati huo bure, nyumba za Michenzani zilitolewa na Mzee Karume wengine kwa fidia na wengine bure, ilikuwa tunatengeneza makaazi,

nyumba za Bambi zilitolewa wakati huo bure, nyumba za Makunduchi zilitolewa bure, nyumba za Chaani zilitolewa bure, serikali ikapitisha uamuzi wa kutoza kodi.

Mhe. Naibu Spika, sasa wale wote ambao hawakulipwa fidia nyumba zile wanatozwa kodi, waliolipwa fidia ni mali yake. Kwa hivyo, yeyote aliyepewa nyumba ambaye kama ni fidia hiyo, nyumba ni mali yake kabisa, hakuna hoja hapo, lakini nyumba ambayo ilitolewa kwa makaazi tu kupewa mtu njoo ukae hapa hizi zote zinatakiwa zilipwe kodi, lakini hawa waliopewa na Mzee Karume hawatatozwa kodi hawa wakae maisha yao, lakini baadae nyumba itabidi irudi serikalini.

Mhe. Naibu Spika, uamuzi huo hawataupenda watu, lakini ndio uamuzi uliofanywa na serikali, tena sio juzi tumeutafuta kwenye kumbukumbu mpaka tumeupata. Kwa hivyo, ile ripoti imejadiliwa na mwelekeo ndio huo, lakini hili halitolifanya kwa kuvamia walibisha watu, kwa nini uamuzi umekuja hivyo, watu watimue watu, sijui watoke kwenye majumba hatutafanya hivyo, tutakwenda kidogo kidogo mpaka tufike pahala tuelewane hatutafanya hivyo. Kwa sababu hawa ni wananchi wenzetu hatuwezi tukafanya *harassing* ya namna yoyote, lakini waliopewa na Mzee Karume wasiwe na wasiwasi waendelee kukaa na nyumba zile bure hakuna matatizo. Warithi sasa wachukue mkataba wakodi, wakubaliane maana warithi wanaweza kuwa mmoja, wawili, watatu, hawawezi wakawa watu wanne wakakaa nyumba moja. Kwa hivyo, mmoja wao wampe fursa aikodi ile nyumba.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Nassor Salim Ali, kuhusu tatizo la maji taka, Nyumba za Maendeleo Michenzani. Tatizo la maji taka katika Nyumba za Maendeleo Michenzani ni kweli lipo na linasababishwa na mambo mawili makubwa nayo ni:

1. Matumizi yasio sahihi yanayofanywa kwa baadhi ya wakaazi wa nyumba hizo. Hata hivyo, jitihada kubwa zimefanywa kwa kushirikiana na Afisi ya Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Mjini na Masheha kufanya vikao na wakaazi wa nyumba hizo na pia kuwapa vipeperushi vinavyoelekeza matumizi yalio sahihi kwa wakaazi wa nyumba hizo; na

2. Miundo mbinu ya maji taka ya nyumba hizi ni michakavu na inahitaji matengenezo makubwa ili kuirejesha katika hali yake ya kawaida. Hata hivyo, jitihada zinafanyika kwa mashirikiano makubwa na Baraza la Manispaa katika kutatua kero zinazojitokeza katika nyumba hizo za Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, hapa nasema kwamba kuna maeneo utakuta yanatiririka maji mengine kweli machafu, lakini mengine ni ubovu wa mitandao ya maji safi imepasuka na maji yanatiririka, lakini kwa sababu yanachomoza mbele ya nyumba zile inafikiriwa kwamba ni maji yanayotoka katika karo chafu, lakini hata hivyo, hiyo kazi ndio inaendelea kufanywa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuhusu maamuzi ya serikali juu ya ukarabati wa jengo la *train* (*Chawl Building)*, wananchi watumiaji wa jengo hilo hawajui ujenzi huo utafanywa na nani, kama serikali au watu binafsi na hatima ya wakaazi hao.

Mhe. Naibu Spika, tusiwatishe wafanyabiashara, si vizuri, wafanyabiashara tumewaorodhesha wote hatungependelea sisi ifike siku jengo lile liondoke tupate matatizo hapa kwenda kuzika watu. Jengo lile wamelifanyia matengenezo ya kujidanganya mtu anajenga duka halafu anatafuta *gypsum* anaziba ile dari mbovu. Sasa madhali dari ni mbovu, ni mbovu tu, hata ukijaribu kuiziba kwa *gypsum* ile dari ni mbovu, siku moja itafudikia, ikifudikia itakuwa maafa makubwa pale *Chawl Building.*

Mhe. Naibu Spika, serikali imejitolea jengo lile lifanyiwe matengenezo lote upya katika sura yake ile ile na *estimate* zimeshafanywa na wale ndio wapewe *priority* ya kuja kuingizwa tena mle na majina yao yapo, kwa mfano hata ukinunua *flat* katika *Chawl Building* utaitengenezaje peke yako, hilo ni tatizo huwezi kuitengeneza *flat* ile peke yako, shirikiana na serikali ukishashirikiana na serikali, jumba lifanywe matengenezo lile, urejeshwe katika duka lako kwa kipindi kile na hii itakuwa ni kwa mikataba maalum, ifanywe kwa mikataba maalum kabisa ili tutekeleze hivyo.

Mhe. Naibu Spika, jengo la *Chawl Building* kama mtaoneshwa picha zake kesho nyote mtaamua watu watoke mle ndani, bovu, limeshuka, madirisha yamepishana kwa njia ya kubomoka, jengine dirisha liko juu, jengine liko chini,

wala sivyo lilivyotiwa, lakini limeshuka tu. Kwa hivyo, lazima Waheshimiwa, tukubali jengo la *Chawl Building* lifanyiwe matengenezo upya, tutayafanya matengenezo upya na litaleta sura nzuri na litaupamba mji na waliomo mule ndio warejeshwe mwanzo katika jengo lile, huu ndio utaratibu.

Mhe. Naibu Spika, nilisema kujenga ni kazi ngumu sana, lazima wakati mwengine ukubali kwamba utaingia kwenye matatizo kwa sababu unajenga, hata nyumba yako mwenyewe ukiibadilisha wewe *formation*, basi lazima uhame kidogo utoe nafasi. Tukubaliane hatujawaambia watoke sasa hivi, lakini tukizipata pesa tutawaambia watoke. Tulitaka kabla ya masika tuanze kufanya matengenezo ya jengo lile kwa sababu *estimate* zote ziko tayari na ramani zote ziko tayari, tumekosa pesa, tukizipata pesa keshokutwa tutawaomba jamani nyee tupisheni na orodha zao zipo kwa jina mmoja mmoja kila mwenye duka. Jengo lile baya mtakuja kutukamata hapa likianguka, tusiende kwenye masuala ya meli tena tukaanza kwenda kutafuta ma-*crane* kufukua udongo pale, tunarudi tena Maisara a! Tuangalie jamani jengo bovu sana lile, bovu, bovu, bovu. Nasema kwa msisitizo suala hili, bwana tusirudi Maisara kila siku.

Mhe. Naibu Spika, kwenye meli hapa serikali imeamua juzi, bwana tusirudi Maisara tununuweni meli, tutakwenda Maisara kila kwenda kufanya nini pale kujenga mabanda na kutambua huyu ndiye maiti wangu haifai. Kwa hivyo, *Chawl Building* tunalifanyia matengenezo na waliomo mle ndio watakaorejeshwa katika jengo lile. Tusiwatishe maana yake tukiwatisha tutakuwa hatuwapendi, wafe mle ndani ya jingo, lile liko hali mbaya sana, picha ninazo zote, nishalipiga picha lote, mbaya nikikuonesheni hapa, nyote mtasema duu! watoke kesho kumbe!

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, amezungumza matumizi ya njia ya Mji Mkongwe kutoka Vuga kupitia Serena kuja Malindi kuwa ni ya upande mmoja.

Mhe. Naibu Spika, ili kupunguza msongamano (*Congestion*) ndani ya Mji wa Kihistoria kama Urithi wa Kimataifa (*UNESCO*) kwa upande wa serikali, umetakiwa Mji huo ufanyiwe matumizi bora ya njia kwa vyombo vya moto na wapita kwa miguu na kutakiwa kutayarishwa kwa mpango huu.

Mhe. Naibu Spika, tuna tatuzi sana na sheria hii tunayoitumia katika Mji Mkongwe, sisi wenyewe kama wizara tushakaa kitako tukasema jamani nyee, hebu tupendekezeni marekebisho, maana haya matatizo yamekuwa makubwa. Kwani Historia yake nini, Zanzibar ilipoomba kuifanya Mji Mkongwe kama ni urithi wa Kimataifa walichokisema *UNESCO*, ni kwamba kuna mambo katika urithi wa Kimataifa yanatakiwa yafuatwe. Kwa hivyo, tuonesheni sheria yenu imezingatia huu urithi wa Kimataifa kweli? Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikapeleka sheria ya Mji Mkongwe ni sheria iliyopitishwa humu ndani ya Baraza hili la Wawakilishi, *UNESCO* wakaitizama wakasema hii imefika hoja ya kuwa utangazwe mji ule urithi wa Kimataifa na imezingatia yale masharti ya urithi wa Kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, sasa kama tunaona haiwezekani sasa hivi, ni kuifanyia marekebisho ile sheria *UNESCO* hatusukumi kwa mambo yetu wenyewe na mambo yake yeye hapana, anatumia sheria yetu mpaka leo, ukienda anakwambia nipe sheria yako imeelezaje katika Mji Mkongwe. Sasa yametajwa upangaji wa barabara, ujenzi wa zile nyumba kurudi katiak sura yake, ndivyo sheria ilivyo, usimamizi wa marekebisho ya Mji Mkongwe, ndivyo sheria ilivyo tumetunga wenyewe haikutungwa na *UNESCO, UNESCO* wanaitumia sheria yetu tuliyoipeleka wenyewe imepitishwa humu katika Baraza la Wawakilishi kama hatuipendi tuifanyie marekebisho ile sheria yetu, ni sheria yetu wenyewe haikutungwa na *UNESCO* nasisitiza hili.

Mhe. Naibu Spika, kupata maelezo kwa kutokuwepo fedha katika vifungu vya matengenezo ya nyumba za maendeleo na nyengine za serikali. Idara ya Ujenzi na wizara imeliona hilo la kutokuwepo fedha katika kifungu cha matengenezo ya nyumba, hayo yanatokana na hali halisi ya upatikanaji wa fedha za miradi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, anasema je ni kweli kuna ukataji wa viwanja Tumbe? Kama ni kweli ni utaratibu gani unatumika katika kuvikata viwanja hivyo na utaratibu gani utatumika kuvigawa kwa wananchi?

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuna ukataji wa viwanja na upimaji wa viwanja unaoendelea Tumbe**.** Utaratibu unaotumika katika ukataji wa viwanja hivyo ni wa kawaida kwani eneo ni la kiserikali. Eneo hilo limefanyiwa ramani ya mapendekezo na mipango miji kwanza kabla ya kuanza upimaji huo na katika ramani hiyo ya mapendekezo kuna viwanja 365 na mpaka sasa hivi tumekata na kupima viwanja 155 sawa na asilimia 42.4. Hata

hivyo, viwanja hivyo vilivyopendekezwa ni pamoja na maeneo ambayo yameshavamiwa na wananchi. Utaratibu utakaotumika ni wa kawaida, ni kupokea maombi kutoka kwa wananchi wa eneo la Tumbe na baadae uongozi wa wizara kwa kushirikiana na Sheha wa Shehia ya Tumbe kufanya uamuzi wa mwisho kuvigawa viwanja hivyo kwa mujibu wa maombi yalivyopokelewa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu eneo la Mziwanda alilopewa mtu lina ukubwa gani? Eneo la Mziwanda lenye ukubwa wa eka 17 limetolewa kwa wananchi kwa shughuli za kilimo. Eneo hili likiwa ni miliki ya Wizara ya Kilimo na Maliasili ambalo pia waliazimwa wananchi kwa shughuli za kilimo. Wananchi walipewa taarifa ili wakabidhi eneo hilo la eka 17 kwa mwananchi. Hati ya matumizi ya Ardhi kwa shughuli za kilimo tayari imetolewa.

Mhe. Naibu Spika, nilikwambia Mhe. Bikame Yussuf Hamad, acha niende nikalione hilo eneo nitizame kama haki yake na akidhi hayo matumizi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma, hoja yake ilikuwa kuna malalamiko kwamba baadhi ya wananchi wanaruhusiwa kuwekwa madirisha ya vioo na wengine wanakataliwa.Wizara kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe haiamui kumruhusu mwananchi kutia madirisha ya vioo na wengine kuwakatalia. Bali baadhi ya madirisha ya vioo ambayo yanasanifiwa pembezoni kwa mbao na ubunifu maalum, hayo yanaruhusiwa. Baadhi ya madirisha ya vioo ambayo yakiwa hayana ubunifu na mwonekano wake hounekani wa kisasa huwa hayakubaliki, lakini kwa maelezo zaidi Mamlaka inaruhusu wahusika kufika ofisini.

Mhe. Naibu Spika, kuna wawekezaji ambao wana nia ya kuwekeza eneo la Mizingani kutoka Forodha Mchanga hadi Bustani ya Forodhani. Kwa hatua ya mwanzo ni vyema kwa wawekezaji hao wakafika Mamlaka ya Mji Mkongwe ili kufanya uwasilishaji wa Mradi na kuona kwamba kutokana na taratibu za Urithi wa Kimataifa kama mradi huo utawezekana au utahitajika maelekezo na vipi itawezekana.

Mhe. Naibu Spika, pia, ameishauri wizara kuanzisha Shirika la Nyumba kwani anaamini litakuwa ni mwokozi mkubwa kwa wananchi wa visiwa vyetu. Nasema kwamba hatua tayari zimechukuliwa na ni matarajio yetu kuwa Mswada wa Uanzishwaji wa Shirika la Nyumba unaletwa hapa Barazani kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya pili katika kikao kijacho.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salma, ametoa ushauri kuhusu nyumba karibu wa wastani 40 zilizo katika hali mbaya, Mamlaka inachukua juhudi za makusudi kuwahamisha wananchi wanaozitumia ili majengo hayo yasije yakaleta athari.

Mhe. Naibu Spika, hoja ni nyingi na niseme watu hii wizara wanaijua sana kwa sababu imewagusa, nimetoa hoja nyingi sana na naona nitakuwekeni muda mrefu sana kama nitazisoma hoja zote na kuzirejea tena na tena. Kwa hivyo, labda nigusie suala la Nungwi lililozungumzwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Nungwi kuna ardhi ambayo ilitakiwa kujengwa Ikulu na ilitolewa na watu kwamba ijengwe Ikulu, lakini Ikulu hiyo haikujengwa na sasa hapo katikati kabla ya kuja sisi hapa wizarani, ile ardhi alipewa mtu. Sasa yule aliyepewa ile ardhi ndio anayo na alikuja kuniona. Labda niseme kwamba nimechelewa kuwatekelezea, lakini adhma yangu hasa, kwa sababu pale alipewa mtu ile ardhi na yule mtu sababu za kumfutia inakuwa sina na nimezikosa sababu kwa nini? Yule anaedai pale naye pia kakosa hati, sasa yule aliyepewa anayo hati. Kwa hivyo, nikakusudia kubadilisha kumpa sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ananikumbusha kutokana na majukumu mengi niliyonayo eneo jengine ninalo kule kule Nungwi, tukijaaliwa bora nimpe eneo jengine kuliko kuwatia katika matatizo kuwapa ardhi, halafu wazee wale wakapelekwa Mahakamani wakaambiwa toweni hati hawana, inarudi tena kwa yule yule uliyemnyang'anya maana atakwenda Mahakamani yule aliyepewa. Kwa hivyo, hili nasema bora Mhe. Makame Mshimba, anipe nafasi nitekeleze hilo nililokusudia mimi kama anaona linafaa, nimekusudia kabisa na ardhi ninayo kule kule. Kwa hivyo, bora anipe nafasi.

Mhe. Naibu Spika, masuala haya yamejirejea rejea, lakini nataka nilizungumze la mwisho juu ya suala la uuzaji wa umeme. Mimi niliwaambia watu wangu kabla sijaja hapa na kila siku huwa ninawauliza jamani huu utaratibu wa kununua umeme kwenda katika kituo kile utakwisha lini? Kwa hivyo, wakanambia wanafanya kazi ili kuona

kwamba utaratibu huo unaondoka. Juzi wakanijuilisha kwamba wameshakubaliana, walinambia kwamba utaratibu wa kununua umeme kwa kutumia simu unaanza Julai ambapo ndio mwezi ujao, itabidi ununue kwa kutumia simu yako, simu yako unajaza pesa unanunua umeme kwa kutumia *password* ambazo watakupa. Hilo ndilo nililoelezwa, pamoja na kuwa humu hawakutaja, lakini mimi kwa sababu wameshanambia, basi nataka uanze Julai.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, mbio zao zote wende watu wa *ZECO*, lakini umeme uanze Julai na wake na sababu madhubuti kabisa kwa sababu wamekwisha kunambia kwamba utaratibu huu utaanza Julai na utafanyiwa uzinduzi rasmi kwamba sasa watu watanunua umeme kutumia simu zao. Kwa hiyo, naomba uanze Julai.

Mhe. Naibu Spika, halafu kuna suala la Mhe. Omar Ali Shehe la kuwa watu wanasomeshwa masuala ya mafuta na gesi. Katika hotuba yangu nilisema kwamba kuna wanafunzi 20 nje wanaochukua *field* hizo za mafuta na gesi tayari zimewapeleka kusomeshwa. Sio hiyo tu, lakini pia, siku hizi ukitaka wafanyakazi inabidi uende chuoni ukawatafute wanaosoma kule na uwafanyie kampeni wakubali kuja kushirikiana na wewe na hii kazi Idara ya Nishati inafanya inakwenda Dodoma kule kwa sababu hii *course* iko inawapata watu kule na wana ahadi, kuna wengine washaamua kabisa kwamba wakimaliza pale wako tayari kuajiriwa hapa Zanzibar katika suala la mafuta na gesi. Hiyo tunaendelea nayo na tumeshapata wataalamu wengine, kuna mmoja tulimpata kutoka Marekani pale kuhusiana na mafuta na gesi ambaye tunae sasa hivi pale katika Idara ya Nishati. Kwa hivyo, jitihada tunaifanya.

Mhe. Naibu Spika, masuala haya ni mengi na hapa hata ukisema maneno mengi kiasi gani, buti lipo lipo tu. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri, hoja imeungwa mkono, lakini Waheshimiwa kutokana na *quorum* yetu, siwezi kukuhojini kwamba mmekubaliana na hoja hii ama mmeikataa. Kwa sababu mkiikubali itabidi Mhe. Waziri aombe Baraza likae kama Kamati na kikanuni hatujatimia kufanya hivyo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, tutamwita siku ya Ijumaa pengine asubuhi wenzetu watakuwa wamesharudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa unasemaje? Mimi sijamaliza kuzungumza wewe unasimama. Kesho tukijaaliwa tutamwita Mhe. Waziri wa Fedha atakuja kusoma hotuba yake itajadiliwa kwa siku nzima, pengine na yeye Ijumaa jioni kama ataweza kufanya majumuisho tutamalizia ama Jumamosi asubuhi. Sasa kabla sijaakhirisha, nina tangazo nimepewa na watu wa UWAWAZA kwamba yale mafunzo ya kesho mchana hayatakuwepo, isipokuwa kutakuwa na Kamati ya Uongozi pamoja na hao wafundishaji saa saba mchana kwenye ukumbi wa juu na Wajumbe hao wanaohusika ni hawa wafuatao:- *(Makofi)*

Mhe. Mgeni Hassan Juma
Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
Mhe. Bikame Yussuf Hamad
Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
Mhe. Salma Mussa Bilali

Tangazo limeletwa na Ndugu Nasra Awadh Salmin, Katibu wetu. Mhe. Nassor Salim Ali.

TAARIFA

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, Ahsante sana, nilikuwa nataka muongozo wako kwamba hii hali itaendelea mpaka kesho, sasa hili Baraza sisi tunaendelea au hatuendelei. Kwa sababu hata tukiendelea kesho hali itakuwa ni hivi hivi na vile vile wananchi hawajui sababu ambazo za kuwa hatupitishi bajeti yetu, ni vyema ukawajuilisha Baraza pamoja na wananchi wakaelewa sababu ni nini.

Mhe. Naibu Spika: Watu tulioano tunaweza tukaendelea na michango na hotuba, tuko watu 36 sasa hivi. Kesho tutaelezana wafike 40. Baada ya hayo naakhirisha Baraza letu mpaka tarehe 26/06/2014 saa tatu asubuhi.

(Saa 12:45 Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 26/06/2014 saa 3:00 asubuhi)